ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 35*** ***29th Agost, 2025***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.35. Vol.106 dated 29th Agost, 2025*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

# KANUNI ZA KUDUMU ZA BUNGE

[*Zimetungwa chini ya ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977*]

[2025]

# YALIYOMO

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

| Kanuni | Kichwa cha Habari | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1. | Jina…………………………………………….… | 1 |
| 2. | Matumizi……………………..………………..… | 1 |
| 3. | Tafsiri……………………………………………… | 1 |

## SEHEMU YA PILI
## UONGOZI WA SHUGHULI ZA BUNGE

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Spika……………………………………………..… | 5 |
| 5. | Mamlaka ya Spika……………………………...….. | 6 |
| 6. | Naibu Spika na majukumu yake ………………… | 6 |
| 7. | Wenyeviti wa Bunge na majukumu yao…………... | 7 |
| 8. | Uadilifu kwa Kiongozi wa Bunge……………….... | 7 |

## SEHEMU YA TATU
## UCHAGUZI WA SPIKA, NAIBU SPIKA NA WENYEVITI WA BUNGE

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Uchaguzi wa Spika…………………………........... | 7 |
| 10. | Kiapo cha Spika……………………………………. | 8 |
| 11. | Uchaguzi wa Naibu Spika………………………........ | 9 |
| 12. | Kiapo cha Naibu Spika…………………………….. | 9 |
| 13. | Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge………………... | 10 |

## SEHEMU YA NNE
## UCHAGUZI WA WAJUMBE WA TUME, WABUNGE WANAOKWENDA KATIKA VYOMBO VINGINE VYA UWAKILISHI NA WAJUMBE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

| | | |
|---|---|---|
| 14. | Uchaguzi wa Wajumbe wa Tume……………………. | 11 |
| 15. | Uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine vya uwakilishi…………………..................... | 11 |
| 16. | Nafasi ya uwakilishi kuwa wazi………………………. | 11 |
| 17. | Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki.. | 11 |
| 18. | Taarifa ya kukosa sifa ya kuwa Mjumbe……….……… | 12 |

19. Bunge kumrejesha au kumsimamisha Mbunge au Mjumbe…………………………………………… 12
20. Kujaza nafasi iliyo wazi………………………..… 12

SEHEMU YA TANO
VIONGOZI WENGINE KATIKA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA BUNGE

21. Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni…......... 13
22. Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni……… 13
23. Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni…………………………………………… 13
24. Uteuzi wa Wanadhimu wa vyama Bungeni………. 14

SEHEMU YA SITA
KATIBU WA BUNGE NA SEKRETARIETI YA BUNGE

25. Katibu wa Bunge na majukumu yake…………….. 14
26. Sekretarieti ya Bunge…..………………………… 15
27. Mpambe wa Bunge ……………………………… 16
28. Majukumu ya Mpambe wa Bunge………………... 16

SEHEMU YA SABA
MIKUTANO NA VIKAO VYA BUNGE

29. Mkutano wa kwanza wa Bunge………………….. 16
30. Shughuli za mkutano wa kwanza wa Bunge……… 17
31. Kiapo cha uaminifu kwa Wabunge……………..… 17
32. Ahadi ya uzalendo ……………………………… 18
33. Kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu……………... 18
34. Ufunguzi rasmi wa Bunge Jipya………………… 19
35. Mikutano ya kawaida ya Bunge………………….. 19
36. Muda wa vikao vya Bunge……………………….. 19
37. Kuahirisha Bunge………………………………… 21

SEHEMU YA NANE
SHUGHULI ZA BUNGE

38. Mpangilio wa Shughuli za Bunge………………… 22
39. Dua ya kuiombea Nchi yetu na Bunge...………….. 23
40. Taarifa ya Rais……………………………………... 23
41. Taarifa ya Spika…………………………………… 24
42. Kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais …………. 24
43. Kuwasilisha ombi na taarifa ya ombi……………. 24
44. Masharti kuhusu ombi..…………………………... 25

45. Kuwasilisha nakala ya ombi……………………… 25
46. Hati za kuwasilisha Bungeni……………………… 25
47. Maswali kwa Waziri Mkuu……………………….. 26
48. Maswali na taarifa ya maswali………………… 27
49. Maswali kuhusu jambo lililojitokeza mapema …… 28
50. Masharti kuhusu maswali ……………………… 28
51. Kuondoa swali…………………………..………… 29
52. Jinsi ya kuuliza swali……...……………………. 29
53. Muda wa maswali………………………………… 29
54. Maswali ya nyongeza…………………………... 29
55. Maswali ya nyongeza yasiyoruhusiwa…………..…. 30
56. Maswali kujibiwa kikamilifu…………………….. 30
57. Kuahirisha Shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura……………………………………….. 30
58. Masharti ya jumla kuhusu jambo la dharura……… 31
59. Kauli za mawaziri………………………………… 32
60. Maelezo Binafsi ya Wabunge……..……………… 32
61. Masuala yanayohusu haki za Bunge……………… 32
62. Shughuli za Serikali…………………………….. 33
63. Hoja zitakazotolewa Bungeni……………………... 33
64. Jinsi ya kuwasilisha hoja……………………… 34
65. Taarifa ya hoja…………………………………… 35
66. Utaratibu wa kujadili hoja…………………..…….. 36
67. Kubadilisha hoja………………………………….. 37
68. Mabadiliko ya hoja na kuondoa hoja…………….. 37


SEHEMU YA TISA
KANUNI ZA MAJADILIANO


69. Nyakati za Mbunge kuzungumza Bungeni……….. 38
70. Jinsi ya kupata nafasi ya kuzungumza Bungeni…… 38
71. Maslahi binafsi ya kifedha...................................... 40
72. Muda wa kuzungumza Bungeni…………………… 41
73. Kutosema uongo Bungeni…………..……………. 42
74. Mambo yasiyoruhusiwa Bungeni………………….. 44
75. Kuzungumza zaidi ya mara moja…....…………….. 45
76. Staha ndani ya Bunge…………………………... 45
77. Mamlaka ya Spika kukatiza majadiliano………….. 46
78. Kuhusu utaratibu……………………………….. 46
79. Mwongozo wa Spika…………………………… 47
80. Taarifa…………………………………………... 47
81. Utaratibu, mwongozo na taarifa…………………... 47
82. Hoja ya kuahirisha mjadala……………………….. 47
83. Hoja ya kufunga mjadala………………………….. 48
84. Haki ya raia kujitetea na kujisafisha ……………... 48

SEHEMU YA KUMI
AMANI NA UTULIVU BUNGENI


85. Mamlaka ya Spika kusimamia utaratibu………… 50
86. Utovu wa nidhamu……………………………….. 50
87. Utovu mkubwa wa nidhamu…………………..... 51
88. Utovu wa nidhamu uliokithiri…………………… 52
89. Amani na utulivu kwenye Kamati……………… 53
90. Amani na utulivu Bunge linapokaa kama Kamati… 53
91. Masharti kwa Mbunge aliyesimamishwa kazi……. 53
92. Udhibiti wa fujo Bungeni………………………….. 54


SEHEMU YA KUMI NA MOJA
UHALALI WA SHUGHULI


93. Akidi ya Vikao vya Bunge………………………... 54
94. Uhalali wa Shughuli za Bunge……………………. 54
95. Uamuzi wa Bunge…………………………………… 55


SEHEMU YA KUMI NA MBILI
KUTUNGA SHERIA – MASHARTI YA JUMLA


96. Muswada wa Serikali……………………….……. 56
97. Muswada Binafsi…………………..……………... 57
98. Uwasilishaji wa Muswada…………………………. 57
99. Muswada Kusomwa Mara ya Kwanza…………… 57
100. Muswada kupelekwa kwenye Kamati…………….. 57
101. Taarifa ya Kamati……………………………….. 58
102. Muswada Kusomwa Mara ya Pili………………..….. 58
103. Kurejesha Muswada kwenye Kamati……………….. 60
104. Muswada katika Kamati ya Bunge Zima…………. 61
105. Taarifa baada ya Muswada Kusomwa Mara ya Pili… 62
106. Kuondoa Muswada Bungeni……………………… 63
107. Muswada Kusomwa Mara ya Tatu na kupitishwa na Bunge ……………………………………… 63
108. Ridhaa ya Rais na hifadhi ya sheria……………… 63
109. Utaratibu wa kusoma Muswada wa sheria…..…….. 63


SEHEMU YA KUMI NA TATU
UTARATIBU WA KURIDHIA MIKATABA YA KIMATAIFA


110. Hoja ya kuridhia mkataba……………………… 64
111. Spika kupeleka hoja kwenye Kamati…………….. 64
112. Taarifa ya Kamati……………………………….. 64
113. Hoja kuwasilishwa Bungeni…....………………… 64

114. Majadiliano na uamuzi wa hoja ……………….. 65
115. Hifadhi ya nakala ya Azimio …………………… 65

SEHEMU YA KUMI NA NNE
UTARATIBU WA KUTUNGA SHERIA KUHUSU MAMBO YA FEDHA

116. Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango………….. 65
117. Masharti kuhusu Muswada, hoja na maombi ya fedha……………………………………………. 66
118. Kuwasilisha dondoo na randama za vitabu vya Bajeti 67
119. Kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti …. 67
120. Kamati kukagua utekelezaji wa miradi na uchambuzi wa Bajeti………………..…………………….. 68
121. Kujadili utekelezaji wa Bajeti za wizara……..….. 68
122. Kamati ya Matumizi……………………………. 70
123. Mjadala katika Kamati ya Matumizi………………. 70
124. Kubadilisha Makadirio katika Kamati ya Matumizi.. 70
125. Hoja ya kuondoa shilingi kwenye Makadirio…….. 71
126. Kukamilika mjadala katika Kamati ya Matumizi… 71
127. Hotuba ya Bajeti ya Serikali kusomwa Bungeni…. 72
128. Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti………………… 73
129. Kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Serikali..... 73
130. Muswada wa Fedha za Matumizi………………… 74
131. Muswada wa Sheria ya Fedha…………………… 74
132. Makadirio ya matumizi ya nyongeza…………….. 74

SEHEMU YA KUMI NA TANO
KAMATI ZA BUNGE

133. Mkutano wa Wabunge wote……………………… 74
134. Kamati za vyama vya siasa……………………….. 75
135. Vikao vya Kamati za vyama vya siasa……………. 75
136. Bunge linapokaa kama Kamati…………………… 75
137. Kamati ya Bunge Zima na Kamati ya Matumizi…… 75
138. Muundo wa Kamati za Kudumu za Bunge……….... 76
139. Utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge……. 78
140. Kamati za Kudumu za Bunge……………………. 80
141. Majukumu ya nyongeza ya Kamati za Kudumu za Bunge…………………………………………… 80
142. Utaratibu wa kuunda Kamati Teule………………. 80
143. Akidi na utaratibu wa vikao vya Kamati Teule….. 81
144. Taarifa ya Kamati Teule……………………….. 81
145. Muundo wa taarifa za Kamati…………………… 82
146. Kamati ya Pamoja………………………………. 82
147. Kamati Maalum…………………………………. 82

SEHEMU YA KUMI NA SITA
UTARATIBU WA KUMWONDOA RAIS MADARAKANI

148. Taarifa ya hoja ya kumwondoa Rais…………….. 83
149. Hoja ya kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi.…. 83
150. Wajumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi…….. 84
151. Utaratibu wa kazi ya Kamati Maalum ya Uchunguzi.......…………………………………….. 84
152. Utaratibu katika Kamati ya Bunge Zima kuhusu mashtaka dhidi ya Rais….………………………… 85
153. Azimio la kumwondoa Rais……………………… 85

SEHEMU YA KUMI NA SABA
UTARATIBU WA KUMWONDOA MAKAMU WA RAIS MADARAKANI

154. Utaratibu wa kumwondoa Makamu wa Rais madarakani………………………………………… 85
155. Hoja ya kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi........ 86
156. Wajumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi……. 86
157. Utaratibu wa kazi ya Kamati Maalum ya Uchunguzi … 87
158. Utaratibu katika Kamati ya Bunge Zima kuhusu mashtaka dhidi ya Makamu wa Rais………………. 87
159. Azimio la kumwondoa Makamu wa Rais madarakani………………………………………… 88

SEHEMU YA KUMI NA NANE
HOJA YA KUTOKUWA NA IMANI NA WAZIRI MKUU

160. Taarifa ya hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu………………………………………………. 88

SEHEMU YA KUMI NA TISA
KUMWONDOA SPIKA AU NAIBU SPIKA MADARAKANI

161. Taarifa ya hoja ya kumwondoa Spika madarakani 89
162. Utaratibu wa Kumwondoa Naibu Spika madarakani... 90

SEHEMU YA ISHIRINI
MPANGILIO WA UKAAJI NA UTARATIBU KUHUSU WAGENI BUNGENI

163. Mpangilio wa ukaaji Bungeni……………………… 91
164. Ruhusa kwa wageni kuingia Bungeni…………….. 91
165. Utambulisho wa wageni .......................………… 92

166. Mamlaka ya kuwaondoa wageni Bungeni..………. 92
167. Ruhusa kwa waandishi wa habari..……………….. 92

SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA
USALAMA WA MAENEO YA BUNGE

168. Utaratibu wa kuingia maeneo ya Bunge………….. 93
169. Ukaguzi…………………………………………… 93

SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI
MASHARTI MENGINEYO

170. Wajibu wa Mbunge kuhudhuria Vikao vya Mikutano ya Bunge…………………………………………… 93
171. Lugha rasmi Bungeni………………………………. 94
172. Taarifa Rasmi za Bunge…………………………… 94
173. Mavazi Rasmi……………………………………… 94
174. Kutoingia Bungeni bila mavazi rasmi……………... 96
175. Utaratibu wa kupeperusha Bendera………………. 97
176. Kuahirisha Shughuli za Bunge Mbunge anapofariki 97
177. Kutengua Kanuni………………………………….. 98
178. Salamu za pongezi na pole……………………….. 98
179. Mabadiliko katika Kanuni za Bunge……………… 98
180. Kanuni kuanza kutumika………………………….. 99
181. Kufutwa kwa Kanuni za Bunge.………………… 99

---

**NYONGEZA YA KWANZA**

---

KANUNI ZA UCHAGUZI WA SPIKA NA NAIBU SPIKA

---

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina…………………………………………………… 100
2. Matumizi ……………………………………………..… 100
3. Tafsiri ………………………………………………… 100

SEHEMU YA PILI
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

4. Msimamizi wa uchaguzi…………………….…………... 101

SEHEMU YA TATU
KUWASILISHA JINA LA MGOMBEA

5. Kuwasilisha majina ya wagombea……………………….. 101

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA MGOMBEA WA UCHAGUZI

6. Masharti kwa mgombea……………………………..….. 101

SEHEMU YA TANO
UTARATIBU WA KUPIGA KURA

7. Kumpigia kura mgombea mmoja………………………... 102
8. Utaratibu wa kupiga kura................................................ 102

SEHEMU YA SITA
MATOKEO YA UCHAGUZI

9. Matokeo ya uchaguzi...................................................... 103

**NYONGEZA YA PILI**

KANUNI ZA UCHAGUZI WA WAJUMBE WA TUME NA WABUNGE WANAOKWENDA KWENYE VYOMBO VINGINE VYA UWAKILISHI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina …………………………………………………… 104
2. Matumizi …………………………………………….. 104
3. Tafsiri ………………………………………………… 104

SEHEMU YA PILI
UTEUZI WA WAGOMBEA

4. Uteuzi wa wagombea ………………………………… 105

SEHEMU YA TATU
UTARATIBU WA UCHAGUZI

5. Uchaguzi wa wagombea wa nafasi za uwakilishi ……. 105

SEHEMU YA NNE
UCHAGUZI WA KUJAZA NAFASI ZA NASIBU

6. Uchaguzi wa kujaza nafasi za nasibu ………………… 106

SEHEMU YA TANO
UTARATIBU WA KUPIGA KURA

7. Utaratibu wa kupiga kura …………………………..…… 107

SEHEMU YA SITA
KUPIGA KURA

8. Kupiga kura …………………………………………… 107

SEHEMU YA SABA
KUHESABU KURA

9. Kuhesabu kura ………………………………………… 108

SEHEMU YA NANE
KUTANGAZA MATOKEO YA KURA

10. Kutangaza matokeo ya kura ……………………..……. 109

SEHEMU YA TISA
UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU ZA KURA

11. Utunzaji wa kumbukumbu za kura …………………… 109

SEHEMU YA KUMI
MALALAMIKO DHIDI YA MATOKEO YA KURA

12. Malalamiko dhidi ya matokeo ya kura……………….. 110
13. Masharti ya jumla …………………………………..... 110

**NYONGEZA YA TATU**

THE EAST AFRICAN LEGISLATIVE ASSEMBLY ELECTION RULES

PART I
PRELIMINARY RULES


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Citation …………………………………………………… | 111 |
| 2. | Application…………………………………………….. | 111 |
| 3. | Interpretation ………………………………………... | 111 |


PART II
QUALIFICATION OF CANDIDATES


| | | |
|---|---|---|
| 4. | Qualification of candidates …………………………..... | 112 |


PART III
NOMINATION OF CANDIDATES


| | | |
|---|---|---|
| 5. | Nomination of candidates ……………………….......... | 112 |
| 6. | Validity of nomination ……..………………………… | 112 |
| 7. | Non-refundable deposit …………………………..….. | 113 |
| 8. | Rejection of nomination papers ……………………….. | 113 |


PARTI IV
ELECTION AND VOTING PROCEDURE


| | | |
|---|---|---|
| 9. | Election day …………………………….................... | 114 |
| 10. | Withdrawal of candidature …………………………… | 114 |
| 11. | Campaign by candidates …………………………..….. | 114 |
| 12. | Supervision of the voting process …………………… | 114 |
| 13. | Vote counting agents …………………………………. | 115 |
| 14. | Announcement of election results …………………… | 115 |
| 15. | Custody of ballot papers ……………………………… | 115 |


PART V
ANNULMENT AND AVOIDANCE OF ELECTION


| | | |
|---|---|---|
| 16. | Annulment and avoidance of election ………………... | 116 |
| 17. | Grounds for annulment and avoidance of election…… | 116 |

PART VI
MISCELLANEOUS PROVISIONS

18. Matters not provided for ……………………………… 116

FORMS

## NYONGEZA YA NNE

THE SUBMISSION OF REGULAR REPORTS TO THE PARLIAMENT OF TANZANIA BY THE TANZANIA MEMBERS OF THE EAST AFRICAN LEGISLATIVE ASSEMBLY REGULATIONS

1. Citation …………………………………….……….. 125
2. Interpretation …………………………………............... 125
3. Presentation of annual report ………………………........... 125
4. Time of presentation …………………............................ 125
5. Presentation of special report and consultations ……… 125
6. Attendance and laying of reports on the table ………..... 126

## NYONGEZA YA TANO

THE PAN – AFRICAN PARLIAMENT (TANZANIA MEMBERS) ELECTION RULES

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Citation ………………………………………………… 127
2. Interpretation ………………………………………….. 127

PART II
QUALIFICATION OF CANDIDATES


| | | |
|---|---|---|
| 3. | Qualification of candidates…………………………… | 128 |


PART III
NOMINATION PROCEDURE


| | | |
|---|---|---|
| 4. | Appointment of nomination day……………………….. | 128 |
| 5. | Nomination procedure …………….…..…………….. | 128 |
| 6. | Nomination of candidates ……………………………… | 129 |


PARTI IV
ELECTION PROCEDURE


| | | |
|---|---|---|
| 7. | Election day …………………………………………… | 130 |
| 8. | Voting process ………………………………………… | 130 |
| 9. | Candidates to address voters …………………………. | 130 |
| 10. | Voting procedure...……………………………….......... | 130 |
| 11. | Casting of votes ………………………………………. | 130 |
| 12. | Appointment of counting agents and counting of votes | 130 |
| 13. | Place for counting of votes …………………………... | 131 |
| 14. | Declaration of election results ………………………. | 131 |
| 15. | Custody of ballot papers ……………………………… | 131 |


PART V
MISCELLANEOUS


| | | |
|---|---|---|
| 16. | Matters not provided for …………………………… | 131 |


---

**NYONGEZA YA SITA**

---

MWONGOZO KUHUSU MASWALI KWA WAZIRI MKUU

---


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Maelezo ya jumla…………………………………….. | 132 |
| 2. | Utaratibu wa kupata fursa ya kumuuliza Waziri Mkuu swali………………………………………………… | 132 |
| 3. | Utaratibu wa kuuliza maswali kwa Waziri Mkuu……….. | 132 |
| 4. | Maswali na majibu kwa Waziri Mkuu…………………... | 133 |

## NYONGEZA YA SABA

### MWONGOZO WA KUSIMAMIA UKUSANYAJI NA UTOAJI WA HABARI ZA BUNGE

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Maelezo ya jumla …………………………….............. 134


### SEHEMU YA PILI
### MISINGI NA MASHARTI YA UTOAJI WA HABARI ZA BUNGE


2. Misingi ya ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge... 134
3. Matangazo ya moja kwa moja kurushwa na studio ya Bunge ……………………………………………… 134
4. Upigaji picha katika ukumbi na maeneo mengine ya Bunge...................................................................... 135
5. Maeneo yasiyoruhusiwa kupiga picha……………..... 135


### SEHEMU YA TATU
### MASHARTI KUHUSU UPATIKANAJI WA HABARI KUTOKA KWENYE VIKAO VYA KAMATI ZA BUNGE


6. Majukumu yatakayotekelezwa kwa uwazi ……………. 135
7. Majukumu yatakayotekelezwa kwa faragha ………….. 136
8. Kamati zinazotekeleza Majukumu kwa faragha………. 136
9. Utoaji wa taarifa baada ya kikao cha Kamati…............ 137


### SEHEMU YA NNE
### UKIUKWAJI WA MASHARTI YA MWONGOZO


10. Ukiukwaji wa Mwongozo................................................ 138

## NYONGEZA YA NANE

KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE

SEHEMU YA KWANZA
KAMATI ZA KUDUMU ZISIZO ZA KISEKTA

1. Kamati za Kudumu zisizo za kisekta ………………… 139
2. Muundo na majukumu ya Kamati ya Uongozi ………. 139
3. Muundo na majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge 140
4. Majukumu ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge……………………………………………… 140

SEHEMU YA PILI
KAMATI ZA KUDUMU ZA KISEKTA

5. Kamati za Kudumu za kisekta……….……………...… 141
6. Kamati na shughuli za wizara ………………………… 141
7. Majukumu ya jumla ya Kamati za Kisekta …………… 143

SEHEMU YA TATU
KAMATI ZA SEKTA MTAMBUKA

8. Kamati za Sekta Mtambuka ………………………….. 143
9. Majukumu ya Kamati ya Bajeti …………………….. 144
10 Majukumu ya Kamati ya Sheria Ndogo……………….. 144
11. Majukumu ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma………………………………………………….. 145

SEHEMU YA NNE
KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE ZINAZOSIMAMIA
MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA

12. Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma………………………… 145
13. Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali………… 145
14. Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa… 145
15. Msingi wa kazi za Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma …………………….……….............. 146

KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA YA MWAKA, 1977

(Sura ya 2)

# KANUNI

*[Zimetungwa chini ya ibara ya 89]*

KANUNI ZA KUDUMU ZA BUNGE, 2025

T.S. Na. 538 la mwaka 2025

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Matumizi

2.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Kanuni hizi zitatumika kwa mambo yote yanayohusu utaratibu wa uendeshaji wa Shughuli za Bunge.

(2) Iwapo jambo au shughuli yoyote haijawekewa masharti katika Kanuni, Spika ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo au shughuli hiyo kwa kuzingatia Katiba, sheria nyingine za nchi, kanuni nyingine zilizopo, uamuzi wa awali wa Maspika wa Bunge, pamoja na mila na desturi za uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge na uamuzi huo utaingizwa katika Kitabu cha Uamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadae wa uendeshaji wa Shughuli za Bunge.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vinginevyo: -

"akidi" ni idadi ya Wabunge inayoruhusu kufanya uamuzi wa Bunge kwa mujibu wa kanuni ya 93, 94 na 95;

"Azimio" ni tamko au uamuzi wa Bunge kuhusu hoja mahsusi;

"Bendera" ni Bendera rasmi ya Bunge ambayo ina rangi ya bluu katika umbo la mstatili na yenye umbo dogo la bendera ya Taifa ndani yake katika pembe ya juu ya upande wa kushoto na Siwa, kukiwa na utepe wenye maneno "Bunge la Tanzania";

"Bunge" ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililoanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 62 ya Katiba;

Sura ya 2

"Bunge Jipya" ni Mkutano wa Kwanza wa Bunge ulioitishwa na Rais kwa mujibu wa ibara ya 90(1) ya Katiba baada ya kutangazwa matokeo ya Uchaguzi Mkuu;

Sura ya 2

"chama" ni chama cha siasa chenye uwakilishi Bungeni;

"Gazeti" ni Gazeti la Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama lilivyotafsiriwa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria;

Sura ya 1

"hoja" ni pendekezo linalotolewa na Serikali, Kamati au Mbunge ili lipate uamuzi wa Bunge;

"Jamhuri ya Muungano" ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Tafsiri ya Sheria;

Sura ya 1

"Kamati" ni Kamati yoyote ya Bunge iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni;

"Kamati ya Bunge Zima" ni Kikao cha Wabunge wote wanapokaa kama Kamati wakati wa-

(a) kupitisha Muswada wa Sheria;
(b) kujadili taarifa ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kuhusu mashtaka dhidi ya Rais au Makamu wa Rais;
(c) kujadili hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu; au
(d) kujadili hoja ya kumwondoa madarakani Spika au Naibu Spika.

"Kamati Maalum" ni Kamati iliyoundwa na Spika kwa mujibu wa kanuni ya 147;

"Kamati ya Matumizi" ni kikao cha Wabunge wote wanapokaa kama Kamati kushughulikia Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Serikali;

"Kamati ya Mipango" ni kikao cha Wabunge wote wanapokaa kama Kamati katika Mkutano wa kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

"Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni" ni Kambi inayoundwa na Vyama Vyenye Wabunge Wachache Bungeni, kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 22;

"Kanuni" ni Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025;

"Katiba" ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

Sura ya 2 "Katibu" ni Katibu wa Bunge aliyetajwa katika ibara ya 87 ya Katiba na inajumuisha pia mtumishi mwingine yeyote wa Bunge

Sura ya 2 aliyeidhinishwa kutekeleza kazi yoyote ya Katibu;

"Kikao cha Bunge" ni kikao cha siku moja kinachoanza kwa kusomwa Dua na kumalizika kwa kuahirisha Bunge hadi siku itakayotajwa;

"Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni" ni Mbunge aliyeteuliwa au kuchaguliwa na Wabunge wanaounda Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni ili kuwa Kiongozi wa Kambi hiyo na inajumuisha Naibu Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni;

"Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni" ni Waziri Mkuu kama

Sura ya 2 ilivyoainishwa katika ibara ya 52(2) ya Katiba;

"Kitabu cha Uamuzi" ni kumbukumbu za uamuzi mbalimbali wa Spika kuhusu suala lolote la utaratibu Bungeni;

"Madaraka ya Bunge" ni haki**,** kinga na madaraka ya Bunge kama

Sura ya 2 yalivyofafanuliwa katika ibara ya 100 ya Katiba na katika

Sura ya 296 Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge;

"Maeneo ya Bunge" inajumuisha Ukumbi wa Bunge, sehemu zote za majengo zilipo kumbi, ofisi za Bunge, sehemu za ndani ya Ukumbi wa Bunge, bustani, eneo wazi linalomilikiwa au kutengwa kwa matumizi ya Bunge na inajumuisha maeneo yote yaliyorejewa kwenye tafsiri ya maeneo ya Bunge kwa

Sura ya 296 mujibu wa Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge;

"Maisha ya Bunge" ni muda wote unaoanzia tarehe ambapo Bunge Jipya limeitishwa na Rais kukutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kuishia tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge kwa ajili ya kuwezesha Uchaguzi Mkuu mwingine wa

Sura ya 2 kawaida kufanyika kama ilivyotafsiriwa na ibara ya 65 ya Katiba;

"Mbunge" ni mtu aliyechaguliwa au aliyeteuliwa kwa mujibu wa

Sura ya 2 ibara ya 66 ya Katiba kuwa mjumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano;

"Mkutano wa Bunge" ni mfululizo wa vikao vya Bunge, kuanzia kikao cha kwanza hadi cha mwisho ambapo hoja ya kuahirisha mkutano wa Bunge hutolewa chini ya kanuni ya 37;

"mgeni" ni mtu yeyote ambaye si Rais, Mbunge, Katibu au mtumishi yeyote na ambaye hatekelezi kazi rasmi zinazohusu Bunge;

"Mnadhimu wa Chama Kinachounda Serikali" ni Mbunge aliyeteuliwa na chama cha siasa kinachounda Serikali kwa ajili ya kuratibu na kusimamia maslahi na nidhamu ya Wabunge wa chama au Kambi hiyo Bungeni;

"Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni" ni Mbunge aliyechaguliwa au aliyeteuliwa na Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni kwa ajili ya kuratibu na kusimamia maslahi na nidhamu ya Wabunge wa Kambi hiyo Bungeni;

"Mpambe wa Bunge" ni mtumishi wa Ofisi ya Bunge anayetekeleza majukumu yaliyoainishwa katika kanuni ya 28;

"Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni" ni Mbunge aliyeteuliwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Walio Wachache Bungeni kwa moja ya Wizara za Serikali;

"Muswada wa Sheria" ni mapendekezo kwa ajili ya kutunga sheria yanayowasilishwa Bungeni na Serikali chini ya kanuni ya 96 au Kamati ya Bunge au Mbunge chini ya kanuni ya 97;

"Mwenyekiti" ni Mbunge aliyechaguliwa kuongoza Shughuli za Bunge na pia ina maana ya Spika, Naibu Spika au Mbunge mwingine anapokuwa anaongoza Kamati ya Bunge Zima, Kamati ya Matumizi au Kamati ya Mipango na inajumuisha Mbunge yeyote anayeongoza Kamati iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni au Mkutano wa Uchaguzi wa Spika;

"Naibu Spika" ni Mbunge aliyetajwa kuwa Naibu Spika wa Bunge kwa mujibu wa ibara ya 85 ya Katiba na kuchaguliwa kwa mujibu wa kanuni ya 11;

Sura ya 2 "Naibu Waziri" ni Mbunge aliyeteuliwa na Rais kuwa Naibu Waziri kwa mujibu wa ibara ya 55(2) na (3) ya Katiba;

Sura ya 2 "Ombi" ni wasilisho mahsusi linaloletwa Bungeni na Mbunge kwa niaba ya watu kwa mujibu wa kanuni ya 43;

"Orodha ya Shughuli" ni mpangilio mahsusi wa Shughuli za Bunge katika kila kikao cha Bunge na inajumuisha Orodha ya Nyongeza ya Shughuli;

"Rais" ni mtu anayeshika madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyetajwa katika ibara ya 33 ya Katiba;

Sura ya 2

"Randama" ni kitabu kinachofafanua majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika fungu husika, fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha unaoisha, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na inajumuisha fedha zilizotengwa na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaofuata;

Sura ya 1

"sheria ndogo" ni amri, tamko, taarifa na kanuni mbalimbali kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria;

"Shughuli za Serikali" ni shughuli zinazowasilishwa Bungeni na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

"Siwa" ni rungu la dhahabu ambalo ni kielelezo cha Mamlaka ya Bunge;

Sura ya 2

"Spika" ni Spika wa Bunge aliyetajwa katika ibara ya 84 ya Katiba na kuchaguliwa kwa mujibu wa kanuni ya 9;

"Taarifa Rasmi za Bunge" ni taarifa za majadiliano ya Bunge au Kamati zilizoandaliwa kwa mujibu wa kanuni ya 172;

Sura ya 115

"Tume" ni Tume ya Utumishi wa Bunge iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uendeshaji Bunge;

"vyombo vingine vya uwakilishi" vinajumuisha Bunge la Afrika (PAP), Jukwaa la Mabunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC-PF), Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA), Jukwaa la Mabunge ya Nchi Wanachama wa Maziwa Makuu (ICGRL) na chombo kingine ambacho Bunge litajiunga;

"Wabunge Walio Wachache" ni Wabunge wa chama au vyama ambavyo haviundi Serikali;

Sura ya 2

"Waziri" ni Mbunge aliyeteuliwa na Rais kuwa Waziri wa Serikali kwa mujibu wa ibara ya 55 ya Katiba;

"Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki" ni Wimbo rasmi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

"Wimbo wa Taifa" ni Wimbo wa Taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## SEHEMU YA PILI
## UONGOZI WA SHUGHULI ZA BUNGE

Spika

4. Spika atakuwa Kiongozi wa Bunge na atatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni.

Mamlaka ya Spika
Sura ya 2

5.-(1) Katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo, Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, kanuni nyingine zilizopo, uamuzi wa awali wa Maspika wa Bunge, pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.

(2) Spika atatilia nguvu Kanuni zote za Bunge, na Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kumwarifu Spika kuwa Mbunge fulani amekiuka Kanuni.

(3) Spika anaweza kumtaka Mbunge yeyote anayekiuka Kanuni kujirekebisha mara moja.

(4) Mbunge yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza, ndani ya siku moja tangu uamuzi unaolalamikiwa kutolewa, kuwasilisha kwa maandishi malalamiko na sababu za kutoridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika.

(5) Spika ataitisha Kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge kwa ajili ya kushughulikia uamuzi unaolalamikiwa.

(6) Pale ambapo uamuzi unaolalamikiwa utakuwa umetolewa na Spika, Naibu Spika ataongoza kikao cha Kamati kitakachoitishwa na Spika kushughulikia malalamiko dhidi ya uamuzi uliotolewa na Spika.

(7) Spika anaweza wakati wowote bila kutoa taarifa rasmi kwa Bunge kumtaka Naibu Spika au Mwenyekiti wa Bunge kuongoza Shughuli za Bunge.

(8) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba na Kanuni, wakati wowote ambapo Spika hayupo Bungeni au kwa sababu nyingine yoyote hawezi kutekeleza madaraka au majukumu ya Spika, basi madaraka au majukumu ya Spika yatatekelezwa na Naibu Spika.

(9) Endapo Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge wote hawapo, Wabunge watamchagua mmoja wa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kuendesha Shughuli za Bunge kufuatana na utaratibu uliowekwa na Kanuni.

Naibu Spika na majukumu yake
Sura ya 2

6.-(1) Naibu Spika aliyetajwa katika ibara ya 85(1) ya Katiba, atachaguliwa kwa mujibu wa kanuni ya 11 ya kutoka miongoni mwa Wabunge na kushika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba na Kanuni.

(2) Naibu Spika atakuwa msaidizi wa Spika katika kuliongoza Bunge na atatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba na Kanuni, wakati wowote ambapo Spika na Naibu Spika wote hawapo Bungeni au kwa sababu nyingine yoyote, hawawezi kutekeleza madaraka au majukumu yao, basi madaraka au majukumu hayo yatatekelezwa na Mwenyekiti wa Bunge.

(4) Naibu Spika anaweza wakati wowote, bila kutoa taarifa rasmi kwa Bunge, kumtaka Mwenyekiti wa Bunge kuongoza Shughuli za Bunge.

Wenyeviti wa Bunge na majukumu yao

7. Kutakuwa na Wenyeviti watatu wa Bunge ambao wataongoza vikao vya Bunge kwa utaratibu na maelekezo ya Spika au Naibu Spika kwa mujibu wa Kanuni.

Uadilifu kwa Kiongozi wa Bunge

8. Kwa kuzingatia matakwa na masharti yaliyowekwa na kiapo cha kazi zake na kwa madhumuni ya utoaji wa uamuzi na uendeshaji wa Shughuli za Bunge kwa haki na bila upendeleo, Spika-

(a) ataendesha shughuli za Bunge na kutoa uamuzi kwa haki, uadilifu na bila chuki wala upendeleo wowote, kwa kuongozwa na Katiba, sheria za nchi, Kanuni, kanuni nyingine zilizopo, uamuzi wa maspika wa Bunge waliotangulia na pia kwa kuzingatia uzoefu pamoja na mila na desturi za mabunge mengine yanayofuata utaratibu wa kibunge unaofanana na unaofuatwa na Bunge la Tanzania; na

(b) hatafungwa na msimamo utakaowekwa au makubaliano yatakayofikiwa na Kamati yoyote ya chama cha siasa kinachowakilishwa Bungeni.

## SEHEMU YA TATU
## UCHAGUZI WA SPIKA, NAIBU SPIKA NA WENYEVITI WA BUNGE

Uchaguzi wa Spika
Sura ya 2

9.-(1) Kutakuwa na Uchaguzi wa Spika utakaofanyika kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 86(1) ya Katiba kwa utaratibu uliowekwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni.

(2) Chama cha Siasa kitakuwa na haki ya kupendekeza jina moja la Mbunge wa Chama hicho ambaye atakuwa mgombea wa nafasi ya Spika kwa mujibu wa Katiba.

(3) Majina ya wagombea wasio Wabunge yatawasilishwa na vyama husika kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi siku tano kabla ya uchaguzi na Tume itayachambua na kisha kuyawasilisha majina ya wagombea wenye sifa kwa Katibu siku mbili kabla ya uchaguzi.

(4) Uchaguzi wa Spika utafanyika katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge Jipya mara baada ya Katibu kusoma Tangazo la Rais na kikao hicho kitageuka kuwa Mkutano wa Uchaguzi wa Spika au katika kikao kinachofuata cha Mkutano wowote wa Bunge mara baada ya Kiti cha Spika kuwa wazi.

(5) Uchaguzi wa Spika utasimamiwa na Mwenyekiti ambaye atatoka miongoni mwa Wabunge ambao wamekuwa Wabunge mfululizo kwa muda mrefu na asiye mgombea wa nafasi ya Spika baada ya kuombwa na Katibu kuongoza kikao cha uchaguzi wa Spika.

Sura ya 258

(6) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

Kiapo cha Spika

10.-(1) Mara baada ya uchaguzi wa Spika kukamilika na muda wa Spika kuapishwa kuwadia, Mwenyekiti atamwita Spika ajongee mbele ya Bunge ili aape viapo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.

(2) Wakati wa kuapa, Spika anayeamini kuwa kuna Mungu, atalazimika kushika Biblia au Kurani au kitabu kingine kinachotambuliwa na imani ya dini yake.

(3) Iwapo Spika haamini kuwa kuna Mungu, atalazimika kuinua mkono wake wa kuume juu na baada ya kiapo hatalazimika kusema maneno *"Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie"*.

(4) Kabla ya kushika madaraka yake, Spika ataapa mbele ya Bunge Kiapo cha Uaminifu na Kiapo cha Spika vitakavyokuwa na maneno yafuatayo:

Kiapo cha Uaminifu:

*"Mimi, …………, Naapa/Nathibitisha kwamba, nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa. Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie."*

Kiapo cha Spika:

*"Mimi, …………., Naapa/Nathibitisha kwamba, nitaitumikia vema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi zangu kama Spika wa Bunge, na katika kutimiza wajibu wa cheo hicho nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba, Kanuni za Bunge, na Sheria, Mila na Desturi za Jamhuri ya Muungano na kwa vyovyote vile sitatoa siri za Bunge. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie."*

(5) Baada ya Spika kuapishwa atakalia kiti chake na kutoa hotuba fupi ya shukrani kwa Bunge na kisha ataliahirisha Bunge hadi wakati mwingine atakaoutaja ambapo shughuli za kuapisha Wabunge wote Kiapo cha Uaminifu zitaanza.

Uchaguzi wa Naibu Spika Sura ya 2

11.-(1) Kutakuwa na uchaguzi wa Naibu Spika wa Bunge katika nyakati zilizowekwa na ibara ya 86(2) ya Katiba na utaratibu uliowekwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni.

(2) Uchaguzi wa Naibu Spika utafanyika katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, au mapema iwezekanavyo baada ya wakati huo au katika Kikao cha kwanza cha Bunge mara baada ya nafasi ya Naibu Spika kuwa wazi, au mapema iwezekanavyo baada ya kikao hicho.

(3) Uchaguzi wa Naibu Spika katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya utafanyika mara baada ya Bunge kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu.

(4) Uchaguzi wa Naibu Spika utaendeshwa kwa utaratibu ule ule unaotumika kumchagua Spika, isipokuwa kwamba, Mbunge hawezi kushiriki katika uchaguzi wa Naibu Spika iwapo hajaapa Kiapo cha Uaminifu.

Kiapo cha Naibu Spika

12.-(1) Mbunge yeyote atakayechaguliwa kuwa Naibu Spika, kabla ya kushika madaraka yake, ataapishwa na Spika mbele ya Bunge Kiapo cha Naibu Spika**.**

(2) Wakati wa kuapa, Naibu Spika anayeamini kuwa kuna Mungu, atalazimika kushika Biblia au Kurani au kitabu kingine kinachotambuliwa na imani ya dini yake.

(3) Iwapo Naibu Spika haamini kuwa kuna Mungu, atalazimika kuinua mkono wake wa kuume juu na baada ya kiapo hatalazimika kusema maneno *"Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie"*.

(4) Kiapo cha Naibu Spika kitakuwa na maneno yafuatayo:

*"Mimi, …………., Naapa/Nathibitisha kwamba, nitaitumikia vema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi zangu kama Naibu Spika wa Bunge, na katika kutimiza wajibu wa cheo hicho nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba, Kanuni za Bunge na Sheria, Mila na Desturi za Jamhuri ya Muungano na kwa vyovyote vile sitatoa siri za Bunge. "Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie."*

Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge

13.-(1) Wenyeviti wa Bunge waliotajwa katika kanuni ya 7 watachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge.

(2) Wenyeviti wa Bunge watachaguliwa na Wabunge kwa nyakati zifuatazo:

(a) katika Mkutano wa Bunge utakaofanyika baada ya Kamati za Bunge kuundwa au mapema zaidi baada ya wakati huo; na

(b) baada ya Kiti cha Mwenyekiti wa Bunge kuwa wazi kwa sababu yoyote isiyohusiana na Bunge kuvunjwa.

(3) Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge utafanyika kwa kuzingatia jinsi na pande za Muungano na kwa kufuata utaratibu kwamba:

(a) Kamati ya Uongozi itapendekeza majina ya Wabunge wasiozidi sita na karatasi ya kura itakuwa na majina ya Wabunge hao;

(b) kila Mbunge atapiga kura kwa kuchagua majina matatu katika karatasi ya kura; na

(c) wagombea watatu watakaopata kura nyingi kuliko wenzao ndio watakuwa wamechaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge.

(4) Iwapo Kamati ya Uongozi itapendekeza majina kwa idadi sawa na nafasi zilizopo, Bunge litathibitisha majina hayo kwa utaratibu uliowekwa chini ya kanuni ya 95.

(5) Wenyeviti wa Bunge waliochaguliwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1), watashika madaraka yao kwa muda ambao wataendelea kuwa wenyeviti au makamu wenyeviti wa Kamati zao za Kudumu za Bunge mpaka mwisho wa Mkutano unaofuata mara baada ya Mkutano wa Kumi wa Bunge, ambao ndio hukamilisha nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge, utakaofanyika baada ya kuchaguliwa kwao, lakini wanaweza kuchaguliwa tena

kuwa wenyeviti wa Bunge katika kipindi cha pili kilichobaki cha maisha ya Bunge kwa kipindi kinachohusika iwapo watachaguliwa tena kuwa wenyeviti au makamu wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge.

## SEHEMU YA NNE
## UCHAGUZI WA WAJUMBE WA TUME, WABUNGE WANAOKWENDA KATIKA VYOMBO VINGINE VYA UWAKILISHI NA WAJUMBE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

Uchaguzi wa Wajumbe wa Tume

14. Uchaguzi wa Wajumbe wa Tume utafanywa kwa kuzingatia, kwa kadri iwezekanavyo, uwiano wa idadi ya Wabunge wa Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni, uwakilishi wa jinsi na pande mbili za Muungano, kwa kuzingatia utaratibu wa kanuni za uchaguzi uliowekwa katika Nyongeza ya Pili ya Kanuni.

Uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine vya uwakilishi

15. Uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine vya Uwakilishi ambavyo kwa mujibu wa mikataba inayounda vyombo hivyo vinatakiwa viwe na wawakilishi wa Bunge utafanywa kwa kuzingatia, kwa kadri iwezekanavyo, uwiano wa idadi ya Wabunge wa Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni, uwakilishi wa jinsi na pande mbili za Muungano, kwa kuzingatia utaratibu wa kanuni za uchaguzi wa Wabunge hao uliowekwa katika Nyongeza ya Pili na Nyongeza ya Tano ya Kanuni.

Nafasi ya uwakilishi kuwa wazi

Sura ya 296

16. Nafasi ya uwakilishi wa Bunge katika chombo kingine cha uwakilishi itakuwa wazi iwapo Mbunge anayeshikilia nafasi hiyo atajiuzulu nafasi yake, atafariki dunia au ataadhibiwa na Bunge kwa mujibu wa Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge au kanuni ya 86, 87 au 88.

Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki

17. Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki utafanyika kwa kuzingatia, kwa kadri iwezekanavyo, uwiano wa idadi ya Wabunge wa Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni, uwakilishi wa jinsi na pande mbili za Muungano kwa kuzingatia utaratibu wa uchaguzi uliowekwa katika Nyongeza ya Tatu ya Kanuni.

Taarifa ya kukosa sifa ya kuwa Mjumbe
Sura ya 2

18. Kwa madhumuni ya utekelezaji wa ibara ya 52 ya Mkataba wa Kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999, Spika atamtaarifu Spika wa Bunge la Afrika Mashariki kwamba, Mjumbe wa Bunge hilo amekoma kuwa Mjumbe na anapaswa kuacha kiti chake kwa mujibu wa Mkataba huo na Kanuni.

Bunge kumrejesha au kumsimamisha Mbunge au Mjumbe

19.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya mikataba inayounda vyombo vya uwakilishi, Spika anaweza kumuita au kumrejesha Mbunge au Mjumbe ikiwa:

(a) imethibitishwa kuwa ameshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na ugonjwa;
(b) amekuwa na mwenendo usiofaa na unaodhalilisha hadhi ya nafasi anayoitumikia; au
(c) ameshindwa kuzingatia na kutetea maslahi ya Taifa wakati anapotekeleza majukumu yake.

(2) Spika atapeleka jina la Mbunge au Mjumbe aliyemuita au kumrejesha kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 1(b) au (c) kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili Kamati hiyo ifanyie kazi na kulishauri Bunge ipasavyo.

(3) Wakati Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge inashughulikia shauri kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), Mbunge au Mjumbe huyo, isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo, itachukuliwa kuwa amesimamishwa kutekeleza majukumu katika chombo cha uwakilishi hadi uamuzi wa shauri lake utakapotolewa.

(4) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itashughulikia shauri hilo na ikithibitika kuwa Mbunge au Mjumbe husika ametenda kosa inaweza kulishauri Bunge liazimie kama ifuatavyo:

(a) kumpa onyo; au
(b) kumuondoa kwenye nafasi anayoitumikia.

(5) Bunge linaweza kuzingatia ushauri mwingine wowote utakaotolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu hatua nyingine yoyote ambayo Mbunge au Mjumbe huyo anastahili kuchukuliwa.

Kujaza nafasi iliyo wazi

20. Mara baada ya nafasi ya Mbunge au Mjumbe kuwa wazi kwa mujibu wa Kanuni, Bunge litafanya uchaguzi wa kujaza nafasi hiyo kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Sehemu hii.

## SEHEMU YA TANO
## VIONGOZI WENGINE KATIKA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA BUNGE

Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni Sura ya 2

21.-(1) Waziri Mkuu atakuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa mujibu wa ibara ya 52(2) ya Katiba.

(2) Endapo Waziri Mkuu hatakuwepo Bungeni kwa kipindi kinachozidi siku moja, basi atamteua Waziri mwingine kuwa Kiongozi wa muda wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni

22. Wabunge wa Vyama vyenye Wabunge Walio Wachache Bungeni wanaweza kuunda Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni iwapo idadi yao itakuwa si chini ya asilimia kumi na mbili na nusu ya Wabunge wote.

Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni

23.-(1) Kutakuwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni ambaye atachaguliwa chini ya utaratibu ulioainishwa katika kanuni ndogo zinazofuata za kanuni hii.

(2) Chama chenye Wabunge Wachache Bungeni hakitakuwa na haki ya kuchagua Kiongozi wa Walio Wachache Bungeni, isipokuwa tu kama kina idadi ya Wabunge wasiopungua asilimia kumi na mbili na nusu ya Wabunge wote.

(3) Chama chenye haki ya kumchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni kinaweza pia kuchagua Naibu Kiongozi wa Kambi hiyo.

(4) Endapo kutakuwa na vyama vyenye Wabunge Wachache zaidi ya kimoja ambavyo kila kimoja kina Wabunge asilimia kumi na mbili na nusu au zaidi, basi Chama chenye idadi kubwa zaidi ya Wabunge kuliko vingine ndicho kitakuwa na haki ya kuchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni, lakini, ikiwa kutakuwa na vyama viwili au zaidi vyenye idadi sawa ya Wabunge ambao ni zaidi ya asilimia kumi na mbili na nusu, Wabunge wa vyama vinavyohusika watachagua Kiongozi wa Walio Wachache Bungeni chini ya utaratibu watakaokubaliana wenyewe.

(5) Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni atateua Wabunge wa Kambi hiyo ambao watakuwa wasemaji wakuu wa Kambi hiyo kwa Wizara zilizopo za Serikali.

Uteuzi wa Wanadhimu wa vyama Bungeni

24.-(1) Chama kinachounda Serikali na chama chenye haki ya kuchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni, vitateua wanadhimu wa vyama hivyo Bungeni ambao watajulikana kwa jina la Mnadhimu wa Serikali na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni.

(2) Vyama hivyo vitateua pia wanadhimu wasaidizi ambao idadi yao itaamuliwa na vyama vyenyewe.

(3) Mnadhimu wa Chama Kinachounda Serikali atakuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni na Wabunge wa Chama kinachounda Serikali na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni atakuwa ni kiungo cha mawasiliano kati ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni na Wabunge Walio Wachache Bungeni.

(4) Vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni vinaweza kutunga kanuni za vyama kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za vyama hivyo Bungeni.

## SEHEMU YA SITA
## KATIBU WA BUNGE NA SEKRETARIETI YA BUNGE

Katibu wa Bunge na majukumu yake
Sura ya 2

25.-(1) Katibu wa Bunge kama alivyotajwa kwenye ibara ya 87(1) ya Katiba, atawajibika kuhakikisha utekelezaji bora wa shughuli za Bunge na kwa madhumuni hayo-

(a) atahudhuria au atawakilishwa katika vikao vyote vya Bunge na vikao vya Kamati;
(b) atawajibika kuweka kumbukumbu zinazotakiwa ziwekwe kwa mujibu wa Kanuni;
(c) atatayarisha Taarifa Rasmi za Bunge kwa mujibu wa Kanuni; na
(d) atatayarisha siku hadi siku, Kitabu cha Shughuli za Bunge na kukihifadhi Ofisini kwake, kikiwa kinaonesha-
    (i) maagizo yote yaliyotolewa na Bunge;
    (ii) shughuli zote zilizopangwa kufanywa siku yoyote ya baadae; na
    (iii) taarifa zote za maswali na hoja zilizokubaliwa na Spika.

(2) Pamoja na majukumu yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), majukumu mengine ya Katibu yatakuwa ni-

(a) kutoa ushauri wa kisheria kuhusu Miswada yote ya Sheria inayowasilishwa Bungeni;

(b) kuchambua Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni na kuwasaidia Wabunge kupata uelewa sahihi wa Miswada hiyo;
(c) kutoa ushauri kwa Bunge kupitia Kamati ya Kanuni za Bunge kuhusu marekebisho yoyote yanayohitajika kufanyika katika Kanuni;
(d) kutoa huduma za ushauri wa kisheria kwa Kamati za Bunge na Wabunge kila atakapohitajika kufanya hivyo;
(e) kusaidia kuandaa Miswada Binafsi ya Sheria ya Kamati au Wabunge na Hoja Binafsi za Wabunge;
(f) kuchambua mikataba yote ya Kimataifa iliyowasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 63(3) (e) ya Katiba, na kutoa ushauri wa kisheria kwa Bunge, Kamati za Bunge na Wabunge kuhusu mikataba husika;

Sura ya 2

(g) kusaidia Wabunge kutayarisha marekebisho ya Muswada wa Sheria unaowasilishwa Bungeni;
(h) kuhakikisha kuwa Muswada wowote wa Sheria uliopitishwa na Bunge unachapishwa kama ulivyopitishwa na Bunge na kuwasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake; na
(i) kushughulikia masuala yote ya sheria yatakayopelekwa kwake na Spika.

(3) Katibu atawajibika kutunza Kitabu cha Uamuzi wa Spika, Kitabu cha Shughuli, Taarifa Rasmi, Miswada ya Sheria na Hati nyingine zilizowasilishwa Bungeni, na Mbunge au mtu yeyote anaweza kukagua kumbukumbu hizo wakati wowote unaofaa kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na Spika.

(4) Katibu ataweka kumbukumbu za uamuzi wa mara kwa mara wa Spika kuhusu masuala ya utaratibu Bungeni.

(5) Katibu atawajibika kuhakikisha kuwa, Ukumbi wa Mikutano ya Bunge na mazingira yake, huduma kwa Wabunge na vifaa vingine vinavyohusika na Shughuli za Bunge, viko katika hali inayofaa kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Sekretarieti ya Bunge
Sura ya 2
Sura ya 115

26.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 88 ya Katiba, Sheria ya Uendeshaji Bunge na Kanuni kuhusu uwekaji wa nafasi na ngazi za utumishi, Ofisi ya Bunge itakuwa na Sekretarieti itakayoundwa na Idara, Sehemu na Vitengo mbalimbali kwa namna na idadi ambayo itaiwezesha kutoa huduma bora na kamilifu kwa Bunge, Wabunge na Kamati za Bunge.

Sura ya 2

(2) Katibu wa Bunge atakuwa Kiongozi wa Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa ibara ya 88(3) ya Katiba.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya kanuni hii, kutakuwa na Makatibu Wasaidizi na Waandishi wa Taarifa Rasmi za Bunge, kwa idadi na ngazi mbalimbali kadri itakavyoamuliwa na Tume.

(4) Kutakuwa na watumishi wengine wa Bunge ambao nyadhifa, kazi na idadi yao itaamuliwa na Tume.

Mpambe wa Bunge

27. Kutakuwa na Mpambe wa Bunge ambaye atatekeleza shughuli mbalimbali za Bunge kwa kufuata maagizo atakayopewa na Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti au Katibu, kwa kadri itakavyokuwa.

Majukumu ya Mpambe wa Bunge

28.-(1) Pamoja na kutekeleza shughuli mbalimbali kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 27, Mpambe wa Bunge-

(a) atasimamia masuala yote ya ulinzi na usalama wa ofisi, mali, vifaa na majengo yote ya Bunge;
(b) atahakikisha utulivu na amani katika sehemu wanayokaa wageni na atawawekea utaratibu maalum wa kuingia na kutoka Bungeni; na
(c) atautangulia msafara wa Spika, akiwa amebeba Siwa, wakati Spika anaingia ukumbini kabla ya kikao na anapotoka baada ya kikao kuahirishwa.

(2) Mpambe wa Bunge atawajibika kuratibu na kushauri juu ya usalama wa Ukumbi, majengo na vyumba vyote vya Bunge na sehemu zote za majengo yanayotumiwa na Bunge, Kamati za Bunge, Wabunge au watumishi wa Bunge.

(3) Mpambe wa Bunge atakuwa na uwezo wa kutoa maagizo kwa askari yeyote aliyekabidhiwa kutekeleza majukumu kwenye Ukumbi wa Bunge na mazingira yake au kwenye majengo, vyumba au sehemu nyingine zinazotumiwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Bunge kwa mujibu wa Kanuni.

## SEHEMU YA SABA
## MIKUTANO NA VIKAO VYA BUNGE

Mkutano wa kwanza wa Bunge

29.-(1) Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya utafanyika mahali, tarehe na saa ambayo Rais atatamka kupitia tangazo litakalochapishwa katika Gazeti wakati akiitisha Mkutano wa Bunge Jipya.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni kuhusu kuanza, kusitishwa au kuahirishwa kwa vikao vya Bunge, Mkutano wa Kwanza wa Bunge utaendelea kwa muda wowote ambao utahitajika kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha shughuli zote za Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya.

Shughuli za Mkutano wa kwanza wa Bunge

30. Shughuli za Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya zitakuwa kama ifuatavyo:
- (a) kusomwa Tangazo la Rais la kuitisha Bunge;
- (b) uchaguzi wa Spika;
- (c) Kiapo cha Spika;
- (d) Dua, Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (e) Kiapo cha Uaminifu kwa Wabunge wote;
- (f) Ahadi ya Uzalendo;
- (g) hoja ya kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu;
- (h) uchaguzi wa Naibu Spika;
- (i) ufunguzi rasmi wa Bunge Jipya utakaofanywa na Rais;
- (j) hoja ya kujadili Hotuba ya Rais; na
- (k) shughuli yoyote ambayo Bunge litaona inafaa kushughulikiwa kwa wakati huo.

Kiapo cha uaminifu kwa Wabunge
Sura ya 2

31.-(1) Kwa kuzingatia ibara ya 68 ya Katiba, kila Mbunge, kabla ya kuanza kushiriki katika shughuli za Bunge, ataapishwa na Spika katika Bunge Kiapo cha Uaminifu.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), endapo Mbunge atachaguliwa au kuteuliwa baada ya Uchaguzi Mkuu, Spika atamwapisha katika-
- (a) kikao chochote cha Bunge iwapo kuna Mkutano wa Bunge; au
- (b) eneo litakalopangwa na Spika iwapo hakuna Mkutano wa Bunge unaoendelea na baadae Spika atatoa taarifa Bungeni kwenye Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge unaofuata.

(3) Wakati wa kuapa, Mbunge anayeamini kuwa kuna Mungu, atalazimika kushika Biblia au Kurani au kitabu kingine kinachotambuliwa na imani ya dini yake.

(4) Iwapo Mbunge haamini kuwa kuna Mungu, atalazimika kuinua mkono wake wa kuume juu na baada ya kiapo hatalazimika kusema maneno *"Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie"*.

(5) Kiapo cha uaminifu cha Mbunge kitakuwa na maneno yafuatayo:

*"Mimi, ……….., Naapa/Nathibitisha kwamba, nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa. Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie."*

Ahadi ya Uzalendo

32.-(1) Katika kila Kikao cha kwanza cha kila Mkutano wa Bunge, isipokuwa Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, Wabunge watatamka kwa pamoja Ahadi ya Uzalendo kwa nchi kwa kuongozwa na Spika mara baada ya kusomwa Dua.

(2) Katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya kila Mbunge atatamka Ahadi ya Uzalendo mara baada ya kuapa Kiapo cha Uaminifu.

(3) Ahadi ya uzalendo kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii itakuwa na maneno yafuatayo:

"*AHADI YA UZALENDO*

*Mimi ……………..kwa heshima kubwa ninaahidi mbele ya Bunge Tukufu kuwa, nitakuwa mtiifu na mwaminifu kwa nchi yangu Tanzania na kwamba ninaahidi kuilinda, kuitumikia na kuitetea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nguvu zangu zote na moyo wangu wote. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie*."

Kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu

33.-(1) Baada ya shughuli ya kuwaapisha Wabunge kukamilika, Spika atalitaarifu Bunge kuhusu uteuzi wa Waziri Mkuu uliofanywa na Rais kwa kulitaja jina la Mbunge anayependekezwa na Rais kuwa Waziri Mkuu.

(2) Baada ya Spika kutaja jina la Mbunge anayependekezwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa hoja ya kuliomba Bunge lithibitishe uteuzi wa Mbunge husika kuwa Waziri Mkuu.

(3) Iwapo Bunge litakataa kumthibitisha Waziri Mkuu, Spika atamjulisha Rais kuhusu uamuzi huo wa Bunge.

Ufunguzi rasmi wa Bunge Jipya

34.-(1) Baada ya uchaguzi wa Naibu Spika, Spika atalitangazia Bunge mahali, siku, tarehe na saa ambayo Rais atalihutubia na kulifungua rasmi Bunge Jipya na baada ya Tangazo hilo, Spika anaweza-

(a) kuahirisha Shughuli za Bunge hadi wakati huo; au

(b) kuahirisha Kikao cha Bunge hadi siku na saa atakayoitaja.

(2) Rais atakapowasili katika viwanja vya Bunge, atapokelewa na Spika akifuatana na Waziri Mkuu na atakaribishwa kulihutubia na kisha kulifungua Rasmi Bunge Jipya.

(3) Baada ya hotuba ya Rais, Waziri Mkuu atatoa hoja ya kuahirisha Bunge hadi siku, tarehe, mahali na saa atakayoitaja.

Mikutano ya kawaida ya Bunge

35.-(1) Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo, kila Mkutano wa Bunge utafanyika katika Ukumbi wa Bunge Dodoma.

(2) Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zitapigwa na kuimbwa katika kila kikao cha kwanza na cha mwisho kwa Mikutano yote ya Bunge kufuatana na utaratibu utakaowekwa na Bunge.

(3) Bila ya kuathiri masharti yanayofuata ya kanuni hii, kila Mkutano isipokuwa Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, utaanza tarehe itakayotajwa na Bunge.

(4) Endapo manufaa ya Taifa yatahitaji kuwa Bunge lisikutane tarehe ile iliyowekwa kwa Mkutano utakaofuata, bali likutane tarehe ya mbele zaidi au ya nyuma zaidi, basi Spika anaweza, kuliita Bunge likutane tarehe hiyo ya mbele zaidi au nyuma zaidi.

(5) Iwapo Bunge litatakiwa kukutana tarehe ya mbele zaidi kuliko tarehe iliyotangazwa awali, basi tarehe hiyo mpya haitakuwa mbele zaidi ya siku kumi na nne kutoka tarehe iliyotangazwa hapo awali.

Muda wa Vikao vya Bunge

36.-(1) Vikao vya Mikutano ya Bunge, isipokuwa Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, vitaanza saa tatu kamili asubuhi, ila tu, kama Bunge litaamua vinginevyo.

(2) Bunge litakutana hadi saa saba kamili mchana ambapo Spika atasitisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa kumi na moja kamili jioni, isipokuwa kama Spika akiona inafaa, Bunge linaweza kuendelea kukutana kwa muda usiozidi dakika thelathini au kusitishwa wakati wowote kabla ya saa saba kamili mchana bila kulihoji Bunge, au Kamati ya Bunge Zima, au Kamati ya Matumizi, au Kamati ya Mipango ili kukamilisha shughuli zilizobaki.

(3) Hoja ya kubadilisha nyakati za vikao itatolewa na Waziri na itaamuliwa kama hoja nyingine yoyote na haitahitaji kutolewa taarifa.

(4) Bunge litaendelea kukaa hadi saa moja na dakika arobaini na tano usiku wakati ambapo Spika atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake au siku nyingine atakayoitaja.

(5) Iwapo Shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa moja na dakika arobaini na tano usiku, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji, lakini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao na Bunge, au Kamati ya Bunge Zima, au Kamati ya Matumizi, au Kamati ya Mipango bado haijamaliza shughuli zake, Spika anaweza kuongeza muda, kwa kadri atakavyoona inafaa, bila kulihoji Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi ili kukamilisha shughuli zilizobaki.

(6) Iwapo wakati wa kusitisha shughuli umefika na Spika atakuwa analihoji au yupo karibu kulihoji Bunge, basi hatasitisha shughuli mpaka hoja iwe imeamuliwa.

(7) Baada ya hoja kuamuliwa, Spika ataahirisha Kikao cha Bunge hadi kesho yake au siku nyingine itakayotajwa.

(8) Endapo Spika atakuwa amepokea taarifa ya Mbunge yeyote anayetaka kutoa maelezo binafsi, basi Spika hataliahirisha Bunge bali ataongeza muda usiozidi dakika thelathini bila ya kulihoji Bunge ili kutoa nafasi kwa Mbunge huyo aweze kutoa maelezo yake:

Isipokuwa kwamba maelezo hayo sharti yawe yameandikwa na kuwasilishwa kwa Spika angalau siku moja kabla hayajatolewa na Mbunge anayehusika atalazimika kuyasoma kama yalivyowasilishwa.

(9) Baada ya kusitisha shughuli za Bunge, hakuna shughuli nyingine yoyote itakayofanywa katika kikao hicho na Spika ataliahirisha Bunge hadi kesho yake au siku nyingine itakayotajwa.

(10) Endapo majadiliano yoyote katika Bunge au katika Kamati ya Bunge Zima yatasitishwa na Spika kwa mujibu wa masharti ya kanuni hii, wakati yatakaporudiwa katika Bunge au katika Kamati, yataendelezwa kuanzia hapo yalipositishwa na Mbunge yeyote ambaye hotuba yake ilikatizwa na Spika atakuwa na haki ya kuendelea na maelezo yake katika marudio ya mjadala huo na endapo Mbunge hakuitumia haki yake hiyo, basi atahesabiwa kuwa alikuwa amemaliza hotuba yake.

(11) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni hii, wakati Spika anapotaka kuliahirisha Bunge, wakati huo unaweza kutumiwa kama fursa kwa Mbunge yeyote kutaka ufafanuzi utolewe na Waziri juu ya jambo lolote lililo chini ya madaraka ya Waziri huyo au kuanzisha mjadala juu ya jambo lolote la dharura kwa idhini ya Spika, isipokuwa kwa jambo ambalo haliwezi kujadiliwa bila hoja maalum kutolewa kwanza kwa ajili hiyo.

(12) Jambo lolote haliwezi kuwasilishwa na kujadiliwa kwa mujibu wa kanuni hii, isipokuwa tu kama Mbunge amewasilisha kwa Spika Taarifa ya maandishi siyo chini ya saa ishirini na nne kabla ya kutolewa kwa jambo hilo Bungeni akieleza kwa ufupi msingi wa jambo analotaka kuzungumzia.

(13) Jumla ya dakika zisizozidi thelathini zitatumika kwa mtoa hoja kuwasilisha Bungeni hoja yake pamoja na majadiliano na uamuzi wa Bunge kwa hoja husika.

(14) Iwapo dakika thelathini zitapita tangu Spika alipotaka kuliahirisha Bunge chini ya kanuni ndogo ya (8) na (11) ya kanuni hii basi Spika atasitisha majadiliano yanayoendelea.

(15) Endapo shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya kikao hazijamalizika na kuna jambo limejitokeza linalolazimu shughuli za Bunge kutoendelea, Spika atalihoji Bunge kuhusu hoja ya kuahirisha kikao cha Bunge na baada ya hoja hiyo kuafikiwa, atakiahirisha kikao hicho hadi kikao kinachofuata ambacho kitakuwa ni siku itakayofuata, isipokuwa tu kama itakuwa ni siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya mapumziko.

Kuahirisha Bunge

37.-(1) Kila Mkutano wa Bunge utafungwa kwa kuliahirisha Bunge hadi Mkutano utakaofuata.

(2) Endapo Shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli ya Mkutano zimekamilika, Katibu atatoa taarifa Bungeni kuhusu kukamilika kwa shughuli hizo kwa maneno yafuatayo:

*"Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa ……… wa Bunge sasa zimemalizika."*

(3) Baada ya Taarifa ya Katibu kutolewa, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni atatoa hoja ya kuahirisha Bunge itakayotaja siku, tarehe, mahali na saa ambapo Mkutano unaofuata utaanza.

(4) Mara tu baada ya Bunge kupitisha hoja ya kuahirisha Mkutano wa Bunge, Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zitapigwa na kuimbwa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Bunge.

## SEHEMU YA NANE
## SHUGHULI ZA BUNGE

Mpangilio wa Shughuli za Bunge
Sura ya 2

38.-(1) Rais anaweza kulihutubia Bunge siku yoyote ambayo Bunge linakutana na wakati mwingine wowote kwa mujibu wa ibara ya 91 ya Katiba.

(2) Wakati wa kuanza Kikao cha Kwanza cha Mkutano wowote wa Bunge baada ya Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupigwa na kuimbwa na Dua kusomwa au kwa vikao vinavyofuata Dua pekee kusomwa na Spika kukalia kiti chake-

(a) kama Spika amepata taarifa kuwa Rais anakusudia kulihutubia Bunge siku hiyo, Spika atalitangazia Bunge ni wakati gani Rais atafanya hivyo;
(b) wakati uliopangwa kwa ajili ya Rais kulihutubia Bunge utakapofika, Spika atampokea Rais na kumkaribisha alihutubie Bunge; na
(c) baada ya hotuba ya Rais, Spika anaweza ama kusitisha kikao kwa muda ili amsindikize Rais au kuliahirisha Bunge hadi siku nyingine itakayotajwa.

(3) Baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi, Spika atatenga muda kwa ajili ya kujadili hotuba ya Rais.

(4) Shughuli za Bunge zitaendeshwa kwa mpangilio ufuatao:

(a) kuapisha Mbunge mpya Kiapo cha Uaminifu;
(b) Mbunge mpya kutamka Ahadi ya Uzalendo;
(c) taarifa ya Rais;
(d) taarifa ya Spika;
(e) hoja ya kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais;
(f) kuwasilisha ombi;
(g) hati za kuwasilisha Bungeni;
(h) maswali kwa Waziri Mkuu;
(i) maswali ambayo taarifa zake zimetolewa;
(j) hoja za kuahirisha shughuli ili kujadili mambo muhimu ya dharura;
(k) kauli za Mawaziri;
(l) maelezo binafsi ya Mbunge;

(m) mambo yanayohusu haki za Bunge, ikiwa ni pamoja na kuzifanyia mabadiliko Kanuni;
(n) shughuli za Serikali;
(o) hoja au taarifa za Kamati;
(p) hoja binafsi za Wabunge; na
(q) shughuli yoyote ambayo Bunge litaona inafaa kushughulikiwa kwa wakati huo.

(5) Bila ya kuathiri masharti mengine ya kanuni hii na baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi, katika kila Mkutano wa Bunge Spika atatenga muda mahsusi kwa ajili ya Bunge kushughulikia Hoja Binafsi na Miswada ya Kamati na Miswada Binafsi ya Wabunge kama itakuwepo.

(6) Shughuli za Bunge katika kila kikao zitatekelezwa kwa kufuata Orodha ya Shughuli za siku hiyo au kwa kufuata utaratibu mwingine ambao Spika ataagiza ufuatwe kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Bunge.

Dua ya kuiombea Nchi yetu na Bunge

39.-(1) Katika kila kikao cha Bunge, Spika au Kiongozi wa Bunge anayefungua Kikao cha siku, kabla ya kukalia Kiti cha Spika, atasoma Dua ya kuiombea nchi na Bunge kabla ya kuanza kwa Shughuli za Bunge zilizopangwa.

(2) Dua ya kuiombea nchi na kuliombea Bunge itakuwa na maneno yafuatayo:

*"Ewe MWENYEZI MUNGU Mtukufu, Muumba Mbingu na Dunia, umeweka katika Dunia Serikali za Wanadamu na Mabunge ya Mataifa ili haki yako itendeke. Tunakuomba, uibariki nchi yetu idumishe uhuru, umoja, haki na amani, umjalie Rais wetu..... hekima, afya njema na maisha marefu ili pamoja na wanaomshauri, wadumishe utawala bora. Utuongezee hekima na busara, sisi Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utupe uwezo wa kujadili kwa dhati, mambo yatakayoletwa mbele yetu leo, ili tufanye uamuzi sahihi wenye manufaa kwa watu wote na ustawi wa nchi yetu. Amina."*

Taarifa ya Rais

40.-(1) Taarifa ya Rais, kama ipo, itasomwa na Spika.

(2) Kila inapowezekana, taarifa ya Rais itasomwa Bungeni kwa kufuata mpangilio wa Shughuli za Bunge, lakini Spika anaweza, wakati wowote, kusitisha shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kuwezesha taarifa hiyo isomwe.

Taarifa ya Spika

41.-(1) Spika atatoa taarifa Bungeni kuhusu Miswada yote iliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wake uliotangulia kuwa imekubaliwa au Rais ametoa uamuzi mwingine.

(2) Spika anaweza kutoa taarifa nyingine katika kikao chochote kadri atakavyoona inafaa.

Kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais Sura ya 2

42. Katika kutekeleza jukumu la kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais chini ya ibara ya 50(4) ya Katiba, Bunge litafuata utaratibu ufuatao:

(a) Spika, atalitaarifu Bunge kuhusu uteuzi wa Makamu wa Rais na kulitaja jina la Mbunge au mtu anayependekezwa na Rais kuthibitishwa na Bunge kuwa Makamu wa Rais;
(b) Baada ya Spika kutaja jina la Makamu wa Rais anayependekezwa, Waziri Mkuu atatoa Hoja ya kuliomba Bunge lithibitishe uteuzi huo;
(c) Iwapo kutakuwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni, Spika anaweza kumpa fursa ya kutoa maoni kuhusu hoja ya kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais;
(d) Kwa idadi ambayo Spika ataona inafaa, anaweza kuruhusu Wabunge kuchangia Hoja iliyotolewa na Waziri Mkuu;
(e) Spika ataongoza utaratibu wa kupiga kura kwa masharti yaliyoanishwa katika Kanuni na uamuzi utakuwa ni wa kura za Wabunge walio wengi;
(f) Endapo Bunge litakataa kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais, Spika atamjulisha Rais kuhusu uamuzi huo wa Bunge; na
(g) Endapo, Makamu wa Rais aliyethibitishwa ni Mbunge, Spika atamwita kusema neno lolote na baada ya kumaliza Spika atamuelekeza kutoka ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Kuwasilisha ombi na taarifa ya ombi

43.-(1) Mbunge yeyote anaweza kuwasilisha Bungeni ombi kuhusu jambo lolote kwa niaba ya watu wanaotoa ombi hilo na ombi hilo halitawasilishwa Bungeni mpaka taarifa ya ombi hilo iwe imetolewa kwa maandishi na kupokelewa na Katibu si chini ya siku mbili za kazi kabla ya Mkutano ambapo ombi hilo linakusudiwa kuwasilishwa.

(2) Ombi lolote linaweza kuwasilishwa Bungeni na Mbunge, likionesha jina la Mbunge anayeliwasilisha.

(3) Mbunge anayewasilisha ombi atatoa maelezo mafupi ya

kutambulisha watu wanaotoa ombi hilo, idadi yao, saini zilizoambatishwa kwenye ombi hilo, madai ya msingi yaliyomo na madhumuni ya ombi hilo.

(4) Baada ya kutimiza masharti ya kanuni ndogo ya (3) ya kanuni hii, Mbunge anayewasilisha ombi anaweza kutoa hoja kwamba, Bunge lijadili ombi hilo, isipokuwa kwamba hoja hiyo haitahitaji kutolewa taarifa na inaweza kuamuliwa bila mjadala wowote.

(5) Mbunge yeyote hataruhusiwa kuwasilisha ombi linalomhusu yeye mwenyewe au ambalo yeye amelitia saini yake au ambalo linakiuka masharti yanayohusu utaratibu wa kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha.

Masharti kuhusu ombi

44. Ombi lolote halitawasilishwa Bungeni isipokuwa tu kama Spika ataridhika kuwa limezingatia masharti yafuatayo:

(a) limeandikwa katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
(b) limeandikwa kwa lugha fasaha na ya heshima; na
(c) limehitimishwa kwa maelezo ya jumla kuhusu madhumuni ya ombi hilo.

Kuwasilisha nakala ya ombi

45. Nakala ya ombi itawasilishwa na Mbunge kwa Katibu si chini ya siku mbili za kazi kabla ya siku ya kuwasilishwa Bungeni.

Hati za kuwasilisha Bungeni

46.-(1) Hati inaweza kuwasilishwa Bungeni wakati wa Kikao cha Bunge na-

(a) Waziri;
(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(c) Kamati yoyote ya Bunge; au
(d) Mbunge yeyote.

(2) Nakala za matoleo yote ya Gazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri na kugawiwa kwa Wabunge.

(3) Hati zote zitawasilishwa Bungeni bila kutolewa hoja yoyote kwa ajili hiyo.

(4) Baada ya hati kuwasilishwa Bungeni, Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge, anaweza kutoa hoja kwamba Bunge lijadili hati hiyo.

(5) Hoja inayotolewa kwa mujibu wa kanuni hii haitahitaji kutolewa taarifa na itaamuliwa bila ya mabadiliko au mjadala wowote.

(6) Hoja ya kujadili hati iliyowasilishwa Bungeni ikikubaliwa, itashughulikiwa kwa kufuata Mpangilio wa Shughuli za Bunge.

(7) Taarifa zinazowasilishwa Bungeni na Kamati yoyote ya Kudumu, Kamati Teule, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Mapendekezo ya Matumizi ya Nyongeza ya Fedha zitatengewa muda wa kujadiliwa Bungeni bila hoja kutolewa.

(8) Taarifa ambazo sheria inaelekeza ziwasilishwe Bungeni zitajadiliwa na Kamati husika za Kudumu za Bunge.

(9) Mjadala unaweza kuzingatia kila jambo lililomo katika hati, isipokuwa kama Spika, kwa kuzingatia uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge, ataamua vinginevyo.

Maswali kwa Waziri Mkuu

47.-(1) Waziri Mkuu anaweza kuulizwa maswali na Mbunge yeyote ambayo yatazingatia masharti kuhusu maswali ya Bunge pamoja na Mwongozo uliowekwa na Nyongeza ya Sita ya Kanuni.

(2) Maswali atakayoulizwa Waziri Mkuu hayatakuwa na taarifa ya awali kama maswali mengine.

(3) Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu kitakuwa kila siku ya Alhamisi na hakitazidi dakika thelathini.

(4) Waziri Mkuu anaweza kutumia Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu kutoa taarifa au ufafanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma kwa muda usiozidi dakika kumi, ikifuatiwa na maswali ya Wabunge kwa dakika ishirini kuhusu taarifa yake au masuala mengine yoyote ya Serikali.

(5) Iwapo siku hiyo, kwa sababu maalum, Waziri Mkuu hatakuwepo Bungeni hakutakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu.

(6) Pamoja na kutawaliwa na masharti kuhusu maswali ya Bunge yaliyowekwa na Kanuni, maswali kwa Waziri Mkuu yatatawaliwa pia na Mwongozo uliowekwa na Nyongeza ya Sita ya Kanuni.

(7) Maswali kwa Waziri Mkuu yatafuatiwa na maswali mengine kwa Mawaziri kwa dakika sitini wakati wa vikao vya kawaida vya Bunge na kwa dakika thelathini wakati wa Mkutano wa Bunge la Bajeti, kama yatakavyokuwa yamepangwa kwenye Orodha ya Shughuli ya siku hiyo.

Maswali na taarifa ya maswali Sura ya 2

48.-(1) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya ibara ya 63(2) na (3) (a) ya Katiba, kutakuwa na Kipindi cha Maswali Bungeni ambapo, Waziri anaweza kuulizwa maswali kuhusu masuala yoyote ya umma au jambo lingine lolote ambalo linasimamiwa na Wizara yake, na vilevile Mbunge yeyote anaweza kuulizwa maswali kuhusu mambo yoyote anayohusika nayo kutokana na kuteuliwa na Bunge kushughulikia mambo hayo.

(2) Maswali yanayoulizwa kwa mujibu wa kanuni hii yatakuwa mafupi kwa kadri inavyowezekana na kila swali litahusu jambo moja tu mahsusi.

(3) Taarifa ya swali itatolewa kwa maandishi na itapelekwa na kumfikia Katibu si chini ya siku ishirini na moja kabla ya tarehe ya Mkutano unaofuata kuanza.

(4) Taarifa zote za maswali zitaingizwa kwenye Kitabu cha Shughuli za Bunge kuonesha kuwa zimepokelewa na maswali yote yaliyopangwa kujibiwa yatawekwa kwenye Orodha ya Shughuli za siku inayohusika.

(5) Waziri aliyeulizwa swali atatoa jibu lake papo hapo wakati wa kipindi cha Maswali.

(6) Endapo swali halikujibiwa siku hiyo kwa sababu ya muda wa maswali kumalizika, litapangiwa nafasi ya kujibiwa siku nyingine katika Mkutano huo, kama swali hilo lilipangwa kujibiwa siku ambayo Mkutano wa Bunge unaahirishwa, swali hilo linaweza kupangwa kujibiwa katika Mkutano unaofuata.

(7) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), endapo swali lililoulizwa limeelekezwa kwa Mbunge, basi kwa idhini ya Spika, Mbunge ambaye swali limeelekezwa kwake atapewa fursa ya kujibu swali hilo.

(8) Maswali yatajibiwa Bungeni kwa mdomo na endapo Mbunge mwenye swali hayupo Bungeni kuuliza swali lake, na Spika hakutoa ruhusa kwa swali hilo kuulizwa na Mbunge mwingine, basi Waziri aliyeulizwa swali atapeleka kwa Katibu jibu la maandishi naye Katibu ataliingiza jibu hilo kwenye Taarifa Rasmi.

(9) Katika hali ya kawaida, Mbunge haruhusiwi kuuliza zaidi ya maswali manne yanayohitaji majibu ya mdomo katika Mkutano mmoja wa Bunge.

(10) Endapo kwa maoni ya Spika, swali lililoulizwa na Mbunge siyo la sera na majibu yake ni marefu au linahitaji takwimu, basi swali hilo litajibiwa kwa maandishi na litaorodheshwa kwenye Orodha ya Shughuli na kuonesha kwamba limejibiwa kwa maandishi na Wabunge wote watagawiwa nakala.

(11) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (5), swali aliloulizwa Waziri yeyote linaweza kujibiwa na Waziri mwingine au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(12) Maswali yote katika Mkutano mmoja yatapewa namba zinazofuatana kwa mfululizo na namba zilizotolewa kwa kila swali zitaingizwa kwenye Kitabu cha Shughuli za Bunge.

(13) Maswali yote ambayo yamepangwa kujibiwa katika Kikao kimoja, yanaweza kuwekwa pamoja kwenye Orodha ya Shughuli na kujibiwa kwa zamu kadri itakavyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli.

(14) Bunge linapovunjwa, maswali yote ambayo hayakuwahi kujibiwa katika uhai wa Bunge hilo yatatenguka.

Maswali kuhusu jambo lililojitokeza mapema

49.-(1) Spika, kwa kuzingatia uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, anaweza kuteua siku moja katika juma ambapo Wabunge watapewa nafasi ya kuuliza maswali kuhusu jambo lolote lililojitokeza mapema linaloihusu jamii.

(2) Mbunge anayekusudia kuuliza swali atawasilisha swali lake siku moja kabla ya siku ya kuuliza swali.

(3) Mbunge anayeuliza swali anaweza, kwa ruhusa ya Spika, kuuliza swali moja la nyongeza linaloendana na swali la msingi.

(4) Maswali yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) na hayakupata fursa ya kujibiwa Bungeni, majibu yake yatawasilishwa kwa Mbunge husika kwa maandishi.

(5) Masharti mengine kuhusu utaratibu wa maswali yaliyoainishwa katika Kanuni yatazingatiwa katika utekelezaji wa masharti ya kanuni hii.

Masharti kuhusu maswali

50. Swali lolote halitaruhusiwa kuulizwa Bungeni kama-

(a) linakiuka Kanuni za Bunge;

(b) linashutumu tabia ya mwenendo wa mtu ambaye mwenendo wake unaweza tu kujadiliwa kwa hoja maalum;

(c) linahitaji habari ambazo zinapatikana katika hati ambazo Mbunge anaweza kujisomea mwenyewe kama vile nakala za Sheria au maandiko ya kumbukumbu za kawaida;

(d) limekusudiwa kupata maoni ya kisheria ya kinadharia au kutoa mapendekezo juu ya jambo la kubahatisha tu;

(e) lina maelezo ya dhihaka, uongo, sifa zisizolazimu, au linatokana na habari za kubahatisha tu;

(f) lina madhumuni ya kutoa habari, au linaulizwa kwa njia inayoonesha jibu lake au kutambulisha mkondo fulani wa maoni;
(g) linahusu jambo zaidi ya moja na ni refu kupita kiasi; au
(h) linamtaja mtu yeyote kwa jina au kutoa maelezo mahsusi juu yake ila tu kama ni lazima ili kulifanya lieleweke.

Kuondoa swali

51. Mbunge anayeuliza swali anaweza kuliondoa swali lake wakati wowote kabla halijajibiwa-
(a) kwa kuwasilisha barua ya kufanya hivyo kwa Katibu iwapo siku iliyopangwa kwa swali hilo kujibiwa haijafika; au
(b) iwapo swali husika tayari limewekwa kwenye Orodha ya Shughuli, kwa kusimama mahali pake jina lake linapoitwa wakati wa maswali na kutamka kuwa analiondoa swali lake na kueleza kwa kifupi sababu za kufanya hivyo.

Jinsi ya kuuliza swali

52.-(1) Wakati swali linalohusika litakapofikiwa katika Orodha ya Shughuli, Spika atamwita Mbunge mwenye swali hilo au kama hayupo, Spika atamwita Mbunge mwingine yeyote aulize swali hilo kwa niaba ya Mbunge mwenye swali.

(2) Mbunge atakayeitwa atasimama na kuuliza swali, pamoja na masahihisho (kama yapo), kwa kutamka maneno yafuatayo bila ya kuongeza jambo lingine lolote:

*"Naomba swali langu (atataja namba ya swali lake lililopo kwenye Orodha ya Shughuli) sasa lijibiwe."*

Muda wa maswali

53.-(1) Muda wa Maswali Bungeni utakuwa dakika tisini, isipokuwa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti, ambapo muda utakuwa dakika sitini.

(2) Spika anaweza kuweka kiwango cha juu cha maswali yatakayowekwa katika Orodha ya Shughuli ambayo anaona yanaweza kujibiwa katika muda uliowekwa.

Maswali ya nyongeza

54.-(1) Maswali ya nyongeza yanaweza kuulizwa na Mbunge yeyote kwa madhumuni ya kupata ufafanuzi zaidi juu ya jambo lolote lililotajwa katika jibu lililotolewa.

(2) Mbunge anayeuliza swali la msingi ataruhusiwa kuuliza maswali ya nyongeza yasiyozidi mawili na Mbunge yeyote atakayepewa nafasi ataruhusiwa kuuliza swali moja tu la nyongeza.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii, swali la nyongeza ambalo litaulizwa katika vipengele zaidi ya kimoja litahesabiwa kuwa ni swali zaidi ya moja.

(4) Isipokuwa kama Spika ataamua vinginevyo, Wabunge watakaouliza maswali ya nyongeza hawatazidi watatu kwa swali moja la msingi, na Mbunge hataruhusiwa kusoma swali lake.

(5) Mbunge ambaye siyo muuliza swali la msingi akipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na iwapo hataridhika na majibu ya Serikali anaweza kuleta swali la msingi kwa ajili hiyo.

(6) Kwa swali la nyongeza ambalo jibu lake ni refu au lenye takwimu nyingi, Waziri, kupitia Ofisi ya Bunge, atampatia Mbunge muuliza swali nakala ya jibu hilo.

Maswali ya nyongeza yasiyoruhusiwa

55.-(1) Swali lolote la nyongeza linaloleta mambo yasiyotokana au kuhusiana na swali la msingi au linalokiuka masharti yanayohusiana na taratibu za kuulizwa maswali litakataliwa.

(2) Endapo Spika atakataa swali la nyongeza linalokiuka masharti ya Kanuni, swali hilo halitajibiwa wala halitaoneshwa kwenye Taarifa Rasmi.

Maswali kujibiwa kikamilifu

56.-(1) Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kikamilifu na Waziri, kupitia Ofisi ya Bunge, atampatia Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza, kabla ya muda wa kujibu swali hilo haujafikiwa.

(2) Waziri Mkuu au Waziri mwingine yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu yaliyotolewa na Waziri.

(3) Iwapo Spika ataridhika kuwa, swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha, ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge.

Kuahirisha Shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura

57.-(1) Baada ya muda wa Maswali kuisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

(2) Hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalum na inaweza kutolewa wakati wowote hata kama majadiliano yatakuwa yanaendelea.

(3) Hoja itatolewa na Mbunge kwa kusimama mahali pake na kuomba idhini ya Spika kutoa hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

(4) Iwapo Spika atajiridhisha kwamba jambo hilo ni la dharura, halisi na lina maslahi kwa umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda ambao Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala linalojadiliwa.

Masharti ya jumla kuhusu jambo la dharura

58.-(1) Masharti ya jumla yafuatayo yatatumika vilevile kuhusu hoja ya kujadili suala la dharura-

(a) hoja hiyo haitaruhusiwa iwapo inahusu jambo ambalo kwalo taarifa ya hoja imekwisha kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli;
(b) hoja zaidi ya moja katika kikao kimoja zenye kutaka kuahirisha Shughuli za Bunge kwa kutumia kanuni hii hazitaruhusiwa; au
(c) jambo ambalo litakuwa limejadiliwa katika hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge iliyotolewa kwa mujibu wa kanuni hii, halitaletwa tena Bungeni katika Mkutano ambao uamuzi ulitolewa.

(2) Jambo linaloletwa kwa hoja chini ya kanuni hii litahesabiwa tu kuwa ni jambo halisi, iwapo -

(a) ni jambo mahsusi;
(b) halikuwekwa katika lugha ya jumla sana au lina mambo mengine mchanganyiko;
(c) limetolewa kwa kutegemea habari za uhakika au habari halisi juu ya jambo hilo zinapatikana; au
(d) halihusu mambo ya kinadharia.

(3) Jambo linaloletwa kwa hoja chini ya kanuni hii litahesabiwa kuwa ni jambo la dharura, iwapo-

(a) athari zake ni dhahiri na linaweza kutokea wakati wowote;
(b) limetokea siku hiyo au siku za karibuni na limeletwa bila kuchelewa; au
(c) hakutatokea fursa ya kulijadili siku za karibuni kwa njia ya kawaida ya kushughulikia mambo ya Bunge.

(4) Jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa Sheria peke yake.

Kauli za Mawaziri

59.-(1) Waziri anaweza kutoa kauli Bungeni kuhusu jambo lolote linaloihusu Serikali.

(2) Kauli inayotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) inaweza kutolewa kwa idhini ya Spika katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge na itahusu jambo mahsusi, halisi na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi thelathini, isipokuwa kwamba kauli hiyo haitajadiliwa.

(3) Waziri mwenye kutoa kauli atawajibika kutoa nakala ya kauli yake kwa Wabunge wote wakati anapoiwasilisha Bungeni.

Maelezo binafsi ya Wabunge

60.-(1) Mbunge yeyote anaweza, kwa idhini ya Spika kutoa maelezo binafsi Bungeni yanayolenga kufafanua kuhusu jambo lolote linalomhusu na lililoifikia jamii.

(2) Mbunge anayekusudia kutoa maelezo binafsi anapaswa kuwasilisha maelezo hayo mapema kwa Spika na akiruhusiwa muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi kumi na tano, na maelezo hayo hayatakuwa na mjadala kuhusu jambo hilo.

Masuala yanayohusu haki za Bunge

61.-(1) Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusu haki za Bunge atafanya hivyo wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge uliowekwa na Kanuni na atakuwa amemwarifu Spika mapema kuhusu kusudio lake hilo na jambo ambalo anataka kuliwasilisha.

(2) Spika akimwita Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusu haki za Bunge, Mbunge huyo ataeleza kwa kifupi sababu zinazofanya aamini kwamba jambo analoliwasilisha linahusu haki za Bunge zilizotajwa kwenye Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge.

Sura ya 296

(3) Endapo Spika ataamua kwamba jambo hilo linahusu haki za Bunge, basi atampa nafasi Mbunge husika kutoa hoja yake kisha hoja hiyo itapewa kipaumbele katika kupanga shughuli nyingine zote za kikao kinachohusika.

(4) Mambo yanayohusu haki za Bunge yatawasilishwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa katika Kanuni.

(5) Endapo wakati wa kikao chochote cha Bunge jambo lolote litazuka ghafla ambalo litaonekana linahusu haki za Bunge, shughuli zitasitishwa kwa madhumuni ya kuliwezesha jambo hilo kuwasilishwa na kuamuliwa, isipokuwa tu kama wakati huo kura inapigwa.

Shughuli za Serikali

62.-(1) Shughuli za Serikali zitaanza wakati Spika atakapomwita Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyetoa taarifa ya kuwasilisha Muswada au ya kutoa hoja Bungeni baada ya Katibu kusoma jambo linalohusika kwenye Orodha ya Shughuli.

(2) Baada ya Spika kutoa wito huo, Mbunge yeyote binafsi hataruhusiwa kutoa hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge wala kuuliza swali.

Hoja zitakazotolewa Bungeni

63.-(1) Isipokuwa kama Kanuni zimeagiza vinginevyo, hakuna mjadala wowote utakaoendeshwa Bungeni ila tu kuhusu shughuli iliyoingizwa kwenye Kitabu cha Orodha ya Shughuli za Bunge na kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli za kikao hicho.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba na ya Kanuni, Waziri au Mbunge mwingine anaweza, kwa kutoa hoja, kupendekeza kwamba, suala lolote lijadiliwe Bungeni na hoja hiyo itaamuliwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni.

(3) Isipokuwa kama Spika ataamua vinginevyo, kila hoja ambayo taarifa yake imekubaliwa itapelekwa kwanza kwenye Kamati husika.

(4) Endapo hoja itapelekwa kwenye Kamati inayohusika, Kamati hiyo itaanza kuifanyia kazi hoja hiyo mapema iwezekanavyo, na haitatolewa Bungeni mpaka Mwenyekiti wa Kamati hiyo atakapokuwa amemtaarifu Spika kwamba, Kamati imekamilisha kuifanyia kazi hoja hiyo.

(5) Kamati iliyopelekewa hoja kwa mujibu wa kanuni hii inaweza kufanya mabadiliko katika hoja hiyo kwa kushauriana na mtoa hoja.

(6) Endapo hoja haikupelekwa kwenye Kamati na imewekwa kwenye Orodha ya Shughuli au kama ilipelekwa kwenye Kamati na Kamati hiyo imemaliza kuishughulikia na imewekwa kwenye Orodha ya Shughuli, hoja itawasilishwa na kuamuliwa Bungeni kwa kufuata masharti yafuatayo:

(a) baada ya hoja kutolewa na inapobidi kuungwa mkono, hoja hiyo itajadiliwa kwa ruhusa ya Spika;

(b) mara baada ya mtoa hoja kuwasilisha hoja yake, Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekewa hoja hiyo atatoa maoni ya Kamati; na

(c) kama hoja inayohusika ni hoja ya Serikali, Msemaji wa Kambi ya Walio Wachache atapewa nafasi ya kutoa maoni juu ya hoja hiyo na kama hoja inayohusika siyo ya Serikali, Msemaji wa Serikali atapewa nafasi ya kutoa maoni ya Serikali juu ya hoja hiyo, isipokuwa masharti ya kanuni ndogo hii hayatahusu hoja za Kamati.

(7) Baada ya mjadala kumalizika, Spika atawahoji Wabunge ili kupata uamuzi wa Bunge.

(8) Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwisha kuliamua ama katika Mkutano uliopo au ule uliotangulia, wala kuwahisha shughuli ya Mkutano unaoendelea, isipokuwa kwa kufuata masharti ya Kanuni au kuwahisha shughuli ambayo itazingatiwa katika Mkutano unaoendelea.

Jinsi ya kuwasilisha hoja

64.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba au ya Kanuni, Mbunge yeyote anaweza kupendekeza jambo lolote lijadiliwe Bungeni kwa kuwasilisha hoja, yaani kwa kutoa pendekezo lililokamilika ili lipate uamuzi wa Bunge.

(2) Jambo lolote litakalowasilishwa kwa mujibu wa Kanuni hii litawekwa katika lugha ambayo italiwezesha Bunge kufanya uamuzi ambao ni bayana.

(3) Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo katika Kanuni, mfumo wa maneno ya hoja inayowasilishwa Bungeni utakuwa kama ifuatavyo:

*"KWA KUWA, ................................................*
*NA KWA KUWA, ..........................................*
*KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba."*

(4) Hoja ambayo kwa maoni ya Spika ina lengo la kutaka jambo ambalo lilikwisha amuliwa na Bunge katika kipindi cha miezi kumi na miwili iliyopita kabla ya kikao kinachoendelea lifikiriwe tena, haitakubaliwa na Spika, isipokuwa tu kama ni hoja ya kutaka uamuzi wa Bunge uliokwisha fanyika ubadilishwe.

(5) Hoja yoyote inayokiuka masharti ya Katiba, Sheria au ya Kanuni haitakubaliwa.

Taarifa ya hoja

65.-(1) Isipokuwa kama Kanuni zitaruhusu vinginevyo au kama Spika atatoa idhini yake kwa kutilia maanani udharura wa jambo lenyewe, hoja yoyote haitatolewa Bungeni mpaka taarifa ya hoja hiyo iwe imewasilishwa na kupokelewa na Katibu angalau siku moja ya kazi kabla ya Mkutano ambao hoja hiyo inakusudiwa kutolewa, na Mbunge anayetoa taarifa ya hoja ataambatisha maelezo kuhusu msingi na madhumuni ya hoja yake.

(2) Taarifa ya hoja yoyote itatolewa kwa maandishi na itawekwa saini na Mbunge anayeitoa kabla ya kupokelewa na Katibu kufuatana na masharti ya Kanuni.

(3) Hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila taarifa:
(a) kutengua kanuni yoyote kati ya Kanuni;
(b) kuahirisha Bunge au kuahirisha mjadala;
(c) kutaka wageni waondoke Bungeni;
(d) kutaka ombi lililowasilishwa Bungeni lijadiliwe;
(e) kuahirisha Shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo la dharura;
(f) kuhusu jambo lolote linalohusiana na haki za Bunge; na
(g) kutaka Hati iliyowasilishwa Bungeni ijadiliwe.

(4) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, iwapo anayetoa taarifa ni Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, taarifa hiyo itawekwa saini na Waziri anayehusika au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini hoja hiyo inaweza kuwasilishwa na Waziri mwingine au Naibu Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(5) Endapo hoja ambayo kwayo taarifa iliyotolewa haitajadiliwa katika Mkutano alioutaja mtoa hoja, basi taarifa ya hoja hiyo itatenguka lakini inaweza kutolewa tena katika Mkutano mwingine.

(6) Isipokuwa tu kwa idhini maalum ya Spika, taarifa kuhusu jambo lolote linalohitaji taarifa itolewe kwa mujibu wa Kanuni, lazima taarifa hiyo itolewe.

(7) Hoja zitaingizwa kwenye Kitabu cha Shughuli mapema baada ya kupokelewa na Katibu na zitawekwa kwenye Orodha ya Shughuli ya kikao cha Bunge kulingana na maelekezo ya Spika.

(8) Kila hoja itawekwa kwenye Orodha ya Shughuli ikiwa kama ilivyowasilishwa au kama ilivyofanyiwa marekebisho au mabadiliko ambayo Spika ataagiza yafanyike.

(9) Spika hataruhusu hoja yoyote inayokiuka Katiba au Sheria au Kanuni za Bunge na Katibu atairudisha hoja hiyo pamoja na vielelezo vyake vyote kwa Mbunge mhusika na maelezo ya sababu za kukataliwa kwa hoja hiyo.

(10) Iwapo Mbunge anapenda kufanya mabadiliko ya maneno aliyoyatumia katika hoja anayokusudia kuitoa, anaweza kufanya hivyo kwa kutoa taarifa ya kutaka kufanya mabadiliko angalau siku moja kabla ya siku ile ambapo hoja hiyo imepangwa kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli ili ijadiliwe.

(11) Mbunge ambaye hakutoa taarifa ya kutaka kufanya marekebisho au mabadiliko katika hoja yake, anaweza kumuomba Spika afanye marekebisho au mabadiliko katika hoja hiyo wakati anawasilisha hoja yake bila ya kutoa taarifa.

(12) Pamoja na kuwa taarifa ya kutaka kufanya marekebisho au mabadiliko itakuwa imetolewa, marekebisho au mabadiliko yoyote hayatakubaliwa kama, kwa maoni ya Spika, mabadiliko hayo yanabadilisha mambo ya msingi yaliyomo katika hoja au yanabadilisha makusudio au upeo wa hoja hiyo.

Utaratibu wa kujadili hoja

66.-(1) Mbunge atakapoitwa na Spika kutoa hoja, atasimama mahali panapohusika na kutoa hoja yake.

(2) Hoja au marekebisho au mabadiliko ya hoja yoyote yatahitaji kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua kumi na endapo hayataungwa mkono, hoja au marekebisho au mabadiliko hayo yatatenguka na Katibu ataweka kumbukumbu kwenye Taarifa Rasmi kwamba, kwa kuwa hoja au marekebisho au mabadiliko hayo hayakuungwa mkono, basi hayakujadiliwa.

(3) Mbunge anaweza kuunga mkono hoja kwa kusimama tu mahali pake bila kusema lolote kuhusu hoja hiyo, kisha akakaa; lakini Mbunge aliyefanya hivyo bado atakuwa na haki ya kuizungumzia hoja hiyo hapo baadae.

(4) Iwapo hoja imewekwa katika Orodha ya Shughuli na Mbunge mtoa hoja anapoitwa na Spika anashindwa kuitoa, hoja hiyo itatenguka, isipokuwa kama kuna Mbunge mwingine aliyeidhinishwa na mtoa hoja, anaweza kuitoa kwa niaba yake au kama mtoa hoja ametoa taarifa ya kutaka kuiahirisha, hoja hiyo itaahirishwa.

(5) Hoja inayohusu shughuli za Serikali inaweza kutolewa na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(6) Hoja iliyotenguka yaweza kutolewa tena baadae, baada ya taarifa mpya kutolewa kwa mujibu wa Kanuni.

(7) Ikiwa muda uliotengwa kujadili hoja umekwisha wakati Bunge liko kwenye Kamati ya Bunge Zima kujadili vifungu vya Muswada wa Sheria au katika Kamati ya Matumizi kujadili Makadirio ya Matumizi ya Serikali, basi Mwenyekiti, bila kulihoji Bunge, ataongeza muda kwa kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kupitisha ibara za Muswada wa Sheria au mafungu ya fedha yaliyobaki.

Kubadilisha hoja

67.-(1) Hoja ikishatolewa ili iamuliwe inaweza kubadilishwa kwa-

(a) kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine;
(b) kuondoa maneno fulani bila kuongeza maneno mengine; au
(c) kuingiza au kuongeza maneno mapya.

(2) Kabla ya kutoa hoja hiyo, mtoa hoja atamkabidhi Katibu maandishi yenye saini yake na yanayoonesha mabadiliko anayotaka yafanywe.

(3) Kila badiliko linalopendekezwa sharti liwiane na hoja inayokusudiwa kufanyiwa mabadiliko na pia liungwe mkono na lisiingize jambo lolote ambalo, kwa maoni ya Spika, linaweza kuwasilishwa kwa hoja maalum.

(4) Badiliko lolote halitaruhusiwa kama, kwa maoni ya Spika, linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa.

(5) Iwapo hoja ya mabadiliko inapendekeza kuondoa maneno fulani na kuingiza maneno mengine, basi mjadala juu ya suala la kufanya mabadiliko unaweza kuangalia kwa pamoja yale maneno yanayopendekezwa yaondolewe na maneno yanayopendekezwa yaingizwe.

(6) Iwapo hoja inapendekeza kuondoa au kuingiza maneno, mjadala utahusu tu uondoaji au uingizaji wa maneno mapya, kadri itakavyokuwa.

(7) Hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja nyingine ya mabadiliko sharti ihusiane na hoja ya kwanza ya mabadiliko na itatolewa, itajadiliwa na kuamuliwa kabla ya ile hoja ya kwanza ya mabadiliko kufanyiwa uamuzi.

Mabadiliko ya hoja na kuondoa hoja

68.-(1) Endapo Mbunge anapenda kupendekeza mabadiliko yafanywe katika hoja kwa kufuata masharti ya Kanuni, anaweza kutoa hoja yake ya kufanya mabadiliko wakati wowote baada ya hoja anayotaka kuibadilisha kutolewa, lakini kabla ya Bunge halijahojiwa liifanyie uamuzi.

(2) Endapo kuna mapendekezo mawili au zaidi ya kubadilisha hoja moja, Spika atawaita watoa hoja hizo kwa kufuata mpangilio atakaoamua.

(3) Iwapo mapendekezo yote ya mabadiliko yameamuliwa, Spika ataitoa tena hoja ya awali ili ijadiliwe kama itakavyokuwa imebadilishwa.

(4) Hoja yoyote inaweza kuondolewa wakati wowote kabla hoja hiyo haijafikishwa Bungeni iwapo Mbunge mtoa hoja atatoa kwa Katibu, taarifa ya maandishi ya kuiondoa hoja hiyo.

(5) Endapo hoja imefikishwa Bungeni, mtoa hoja anaweza tu kuiondoa hoja yake kwa kusimama mahali pake na kusema *"Ninaomba ruhusa kuondoa hoja"* na papo hapo Spika ataliuliza Bunge kama linaafiki hoja hiyo kuondolewa na inapotokea Wabunge walio wengi watakubali, Spika atasema *"Hoja inaondolewa kwa idhini ya Bunge"* na hoja hiyo itakuwa imeondolewa na Bunge litaendelea na shughuli inayofuata.

## SEHEMU YA TISA
## KANUNI ZA MAJADILIANO

Nyakati za Mbunge kuzungumza Bungeni

69. Kwa idhini ya Spika, Mbunge yeyote anaweza kusimama na kuzungumza Bungeni wakati-

(a) wa kuchangia mjadala wa hoja yoyote iliyowasilishwa Bungeni ambayo Kanuni zinaruhusu ijadiliwe;
(b) anatoa hoja ili ijadiliwe;
(c) anawasilisha mabadiliko yoyote ya hoja;
(d) amesimama kutaka kuzungumzia jambo lolote linalohusu utaratibu;
(e) amesimama kuzungumzia jambo linalohusu haki za Bunge;
(f) wa kutoa hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo la dharura na muhimu kwa Umma;
(g) wa kutoa maelezo binafsi;
(h) wa kuuliza au kujibu swali; au
(i) wa kutoa taarifa.

Jinsi ya kupata nafasi ya kuzungumza Bungeni

70.-(1) Mbunge akitaka kuzungumza anaweza-

(a) kumpelekea Spika ombi la maandishi;
(b) kusimama kimya mahali pake; au

(c) kubofya kitufe cha kuomba kuzungumza kilichopo kwenye mfumo wa Bunge mtandao:

Isipokuwa kwamba Mbunge yeyote hataanza kuzungumza hadi aitwe na Spika ama kwa jina au wadhifa wake na kumruhusu kusema na wakati wa kusema ataelekeza maneno yake kwa Spika.

(2) Mbunge akimaliza kutoa maelezo yake atakaa kwenye nafasi yake na hapo Spika atamwita Mbunge mwingine aliyempelekea ombi la maandishi au kama Spika hakupata ombi lolote la maandishi, basi Mbunge mwingine yeyote anayetaka kujadili hoja anaweza kusimama mahali pake na kusubiri Spika amwone.

(3) Iwapo Wabunge wawili au zaidi watasimama wakati mmoja, Spika atamwita Mbunge atakayemwona kwanza.

(4) Isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo, endapo maombi ya kuchangia hoja fulani yatakuwa mengi zaidi ya muda uliotengwa kwa hoja hiyo, Spika atatoa nafasi ya kwanza kwa Wabunge ambao:

(a) hawajachangia katika hoja zilizotangulia kujadiliwa katika Mkutano unaoendelea; au

(b) wamechangia mara chache.

(5) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (4), Spika atahakikisha kuwa, nafasi za kuchangia zinatolewa kwa uwiano unaofaa baina ya aina zote za Wabunge walioomba kuchangia hoja hiyo.

(6) Masharti yaliyotangulia katika Kanuni hii, hayatamzuia Spika kutoa nafasi ya kuchangia kwa Mbunge mwingine yeyote iwapo ataona kuwa, taaluma au uzoefu fulani wa Mbunge huyo utaboresha hoja inayojadiliwa.

(7) Mbunge hatasoma maelezo, isipokuwa, kwa madhumuni ya kutilia nguvu maelezo yake, anaweza kusoma dondoo kutoka kwenye kumbukumbu zilizoandikwa au kuchapishwa na anaweza pia kujikumbusha kwa kuangalia kwenye kumbukumbu alizoziandika.

(8) Kila Mbunge atalisemea jambo ambalo liko katika mjadala tu na hatarudiarudia maneno yake au yale yaliyokwisha kusemwa na Wabunge wengine na iwapo itatolewa hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja inayojadiliwa, mjadala sharti uwe juu ya hoja hiyo ya mabadiliko mpaka imalizike ndipo mjadala urudie kwenye hoja ya msingi.

(9) Kila Mbunge atasema akiwa amesimama na atatoa maelezo yake kwa kutumia vyombo vilivyowekwa kwa madhumuni ya kutafsiri, kukuza na kurekodi sauti.

(10) Kwa ruhusa ya Spika, Mbunge yeyote aliye na ulemavu au ugonjwa anaweza kuzungumza akiwa ameketi.

(11) Endapo Spika atasimama wakati Waziri au Mbunge anatoa hotuba Bungeni au atakuwa amesimama mahali pake akisubiri kuanza kuzungumza, Waziri au Mbunge huyo ataketi mahali pake na Bunge litabaki kimya ili Spika aweze kutoa maelekezo au taarifa yake.

(12) Mbunge hataruhusiwa kuzungumzia suala lililokuwa likijadiliwa baada ya Spika kuwahoji Wabunge na hoja hiyo kutolewa uamuzi.

(13) Mbunge yeyote anaweza kutoa maoni yake kwa maandishi na kumpelekea Waziri au Mbunge mtoa hoja inayohusika, wakati ambapo hoja inaendelea kujadiliwa.

(14) Mtoa hoja atayakabidhi maoni hayo kwa Katibu ili yaweze kuingizwa katika Taarifa Rasmi za Bunge.

(15) Katika mjadala wowote, Mawaziri watatajwa kwa majina ya nyadhifa zao na Wabunge watatajwa kwa kutumia neno *"Mheshimiwa"* kabla ya majina yao.

Maslahi binafsi ya kifedha

71.-(1) Wakati wa majadiliano Bungeni, Mbunge hataruhusiwa kuzungumzia jambo lolote ambalo ana maslahi nalo binafsi ya kifedha, isipokuwa baada ya Mbunge huyo-

(a) kusema jinsi anavyohusika na jambo hilo; na

(b) kutaja kiwango cha maslahi ya kifedha aliyonayo katika jambo hilo.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, Mbunge au mwananchi yeyote anaweza kumuarifu Spika, kwa maandishi, akitoa ushahidi kuwa, Mbunge amezungumzia jambo ambalo ana maslahi nalo binafsi ya kifedha bila kusema jinsi anavyohusika nalo wala kutaja kiwango cha maslahi hayo.

(3) Baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa kwake kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, Spika ataipeleka taarifa hiyo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

(4) Baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Spika chini ya kanuni ndogo ya (3), Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itaichunguza taarifa hiyo na kumpa Mbunge husika fursa ya kusikilizwa.

(5) Endapo itadhihirika kwamba ni kweli Mbunge amezungumzia jambo ambalo ana maslahi nalo binafsi ya kifedha bila kusema jinsi anavyohusika nalo wala kutaja kiwango cha maslahi hayo, Kamati hiyo inaweza kulishauri Bunge kwamba, Mbunge huyo aadhibiwe kwa ukiukwaji wa masharti ya kanuni hii kama ifuatavyo:

(a) ikiwa hilo ni kosa lake la kwanza, asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi kumi; au

(b) ikiwa hilo ni kosa lake la pili au zaidi, asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi ishirini.

(6) Bunge linaweza kuzingatia ushauri mwingine wowote uliotolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu adhabu anayostahili kupewa Mbunge aliyekiuka masharti ya Kanuni hii.

(7) Bunge linaweza kupitisha Azimio la kumwadhibu au kutomwadhibu Mbunge kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge utakaotolewa chini ya kanuni ndogo ya (5) na (6) ya kanuni hii.

Muda wa kuzungumza Bungeni

72. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo kwenye Kanuni-

(a) kila Mbunge anayejadili hoja, ataruhusiwa kuzungumza kwa muda usiozidi dakika kumi;

(b) Waziri anayetoa hoja ataiwasilisha hoja yake kwa muda usiozidi dakika thelathini na wakati anahitimisha hoja yake atasema kwa muda usiozidi dakika thelathini;

(c) Mwenyekiti anayewasilisha maoni ya Kamati atayawasilisha kwa muda usiozidi dakika thelathini;

(d) Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni anayewasilisha maoni ya Kambi hiyo atayawasilisha maoni hayo kwa muda usiozidi dakika kumi na tano;

(e) Mwenyekiti anayetoa hoja ya Kamati ataiwasilisha hoja hiyo kwa muda usiozidi dakika thelathini na wakati anahitimisha hoja hiyo, atasema kwa muda usiozidi dakika thelathini; na

(f) Mbunge anayetoa hoja binafsi ataiwasilisha hoja yake kwa muda usiozidi dakika thelathini na wakati wa kuhitimisha hoja yake atasema kwa muda usiozidi dakika thelathini.

Kutosema uongo Bungeni
Sura ya 2

73.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu.

(2) Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni hatachukuliwa kuwa anasema uongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa au lililoandikwa na vyombo vya habari.

(3) Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka "Kuhusu Utaratibu" na baada ya kuruhusiwa na Spika, kudai kwamba, Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisema Bungeni.

(4) Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) ya kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

(5) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo zilizotangulia za kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yeyote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotiliwa mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi au maelezo yake hayo.

(6) Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni, atawajibika kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge, papo hapo au katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili ya kufanya hivyo.

(7) Endapo Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni atashindwa kufanya hivyo, anaweza kujirekebisha kwa kufuta kauli au usemi au maelezo yake hayo, papo hapo au katika muda atakaokuwa amepewa na Spika kwa ajili ya kuthibitisha kauli au usemi au maelezo yake.

(8) Endapo hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa, Mbunge aliyetakiwa kutoa uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni atakataa au atashindwa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge na kama atakataa kujirekebisha kwa kufuta kauli au usemi au maelezo yake, basi Spika atamwadhibu kwa kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi kumi.

(9) Endapo Mbunge mwingine ataona kwamba uongo uliosemwa na Mbunge huyo Bungeni ni mkubwa kiasi cha kuathiri heshima ya Bunge, anaweza kutoa hoja kwamba, Mbunge huyo-

(a) ikiwa ni kosa lake la kwanza, asihudhurie vikao vya Bunge visivyopungua kumi au visivyozidi kumi na tano; au

(b) ikiwa ni kosa lake la pili au zaidi, asihudhurie vikao vya Bunge visivyopungua kumi na tano au visivyozidi thelathini.

(10) Hoja ya aina hiyo inaweza kutolewa bila taarifa na itajadiliwa na kuamuliwa kwa utaratibu ufuatao:

(a) mtoa hoja atatoa hoja yake;

(b) Mbunge anayetuhumiwa kusema uongo Bungeni chini ya kanuni ndogo ya (9) ya kanuni hii, atapewa nafasi ya kujitetea;

(c) Wabunge, kwa idadi itakayoamuliwa na Spika kulingana na muda uliopo, watachangia hoja hiyo kwa dakika zitakazopangwa na Spika;

(d) mtoa hoja atahitimisha hoja yake;

(e) Mbunge anayetuhumiwa kusema uongo Bungeni au Mbunge mwingine yeyote anaweza kutoa maombi ya adhabu iliyopendekezwa kwa kosa la kusema uongo Bungeni ipunguzwe kwa kiwango au namna atakayoipendekeza;

(f) Spika atawahoji Wabunge ili kupata uamuzi wa Bunge kuhusu ombi la kupunguziwa adhabu kama litatolewa na Mbunge anayetuhumiwa au Mbunge mwingine yeyote; na

(g) iwapo pendekezo la kupunguziwa adhabu litakataliwa, basi Spika atalihoji Bunge ili kupata uamuzi kuhusu adhabu iliyopendekezwa na Mtoa hoja.

Mambo yasiyoruhusiwa Bungeni
Sura ya 2

74.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge-

(a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli;
(b) hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala;
(c) hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama;
(d) hatazungumzia jambo ambalo lilijadiliwa na kutolewa uamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia;
(e) hatazungumzia jambo ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahsusi;
(f) hatazungumzia jambo ambalo linapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahsusi inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya;
(g) hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala, au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani;
(h) hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki, isipokuwa tu kama imetolewa hoja mahsusi kuhusu jambo husika;
(i) hatatumia jina la nchi nyingine au jina la kiongozi au raia wa nchi nyingine kwa dhihaka;
(j) hatatoa lugha ya matusi au ishara inayoashiria matusi au kumsema vibaya Mbunge au mtu mwingine;
(k) hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine; au
(l) hatafanya vitendo vya ujeuri au uchokozi.

(2) Mbunge yeyote anayeamini kuwa Mbunge mwingine amevunja au amekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, atasimama mahali pake na kumwambia Spika *"Kuhusu Utaratibu"* na atakaporuhusiwa na Spika kusema, atalazimika kutaja masharti ya kanuni hii yaliyovunjwa au kukiukwa na Mbunge huyo mwingine, na kama Mbunge huyo mwingine atakuwa anasema wakati huo, atakaa chini kusubiri maelekezo na mwongozo wa Spika kuhusu jambo hilo.

Kuzungumza zaidi ya mara moja

75.-(1) Isipokuwa tu kwa idhini ya Spika, Mbunge yeyote hataruhusiwa kuzungumza zaidi ya mara moja juu ya hoja, ila tu kama-

(a) wakati huo Bunge liko kwenye Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi;
(b) anatumia haki yake ya kujibu; au
(c) anasema kuhusu utaratibu.

(2) Mbunge ambaye amezungumza juu ya hoja anaweza kuzungumza tena juu ya hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja aliyoisemea na Mbunge ambaye amependekeza kufanya mabadiliko katika hoja ya awali, anaweza kuzungumza tena juu ya hoja ya awali baada ya mabadiliko kufanyika.

(3) Mbunge mtoa hoja ya msingi au mtoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika hoja iliyokwisha kutolewa, atakuwa na haki ya kujibu kabla uamuzi juu ya hoja hiyo haujatolewa.

(4) Wakati wa kujibu, mtoa hoja atapaswa kujibu mambo yale tu yaliyozungumzwa na Wabunge waliochangia hoja yake na hataruhusiwa kutoa maelezo yoyote mapya, isipokuwa kama maelezo hayo ni ya lazima kwa madhumuni ya kufafanua jambo lililochangiwa na Wabunge.

(5) Mbunge yeyote hataruhusiwa kusema Bungeni baada ya Spika kuwahoji Wabunge na kura ya sauti, ya kielektroniki au ya siri ya *"Ndiyo"* au *"Siyo"* au ya *"sipigi kura"* au kura ya uamuzi ya aina nyingine yoyote kupigwa, isipokuwa pale ambapo itaonekana kuwa kuna mashaka kuhusu matokeo ya kura kwa kufuata wingi wa sauti kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (5) ya kanuni ya 95.

Staha ndani ya Bunge

76.-(1) Wakati wa Vikao vya Bunge, Spika anapokuwa anaingia au kutoka katika Ukumbi wa Bunge, Wabunge, watumishi wa Bunge na wageni wote waliopo kwenye Ukumbi huo watasimama kwa utulivu mahali pao na kubaki kimya hadi Spika atakapokuwa ameketi katika kiti chake au atakapokuwa ametoka kwenye Ukumbi wa Bunge.

(2) Wakati Bunge linaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi, Wabunge, watumishi wa Bunge na wageni wote waliopo kwenye Ukumbi wa Bunge watasimama kwa utulivu mahali pao na kubaki kimya ili kutoa heshima kwa mchakato wa Bunge kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi na baadae Bunge kurejea.

(3) Mbunge, mtumishi wa Bunge au mgeni aliyepo Bungeni wakati wa mjadala atatakiwa-

(a) kuingia au kutoka kwenye Ukumbi wa Bunge kwa staha na atainamisha kichwa kuelekea kwa Spika au kufanya mkunjo wa magoti kwa heshima, kila mara atakapokuwa akienda au kutoka mahali pake;

(b) kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake, na hatatangatanga kwenye ukumbi wa Mikutano bila sababu;

(c) kutopita mbele, pembeni au kwa kuizunguka Siwa au kati ya Kiti cha Spika na Mbunge anayesema;

(d) kutosoma kitabu chochote, gazeti au barua, isipokuwa kama vitu hivyo vinahusu shughuli za mjadala unaoendelea wakati huo; na

(e) kuondoa mlio wa simu na kutozungumza na simu.

Mamlaka ya Spika kukatiza majadiliano

77.-(1) Spika anaweza kulihutubia Bunge wakati wowote na kwa ajili hiyo, anaweza kumkatiza Mbunge yeyote anayezungumza.

(2) Endapo Spika atasimama wakati wa mjadala, na kuanza kuzungumza, Mbunge yeyote ambaye atakuwa anazungumza wakati huo au ambaye atakuwa amesimama mahali pake akisubiri kuanza kuzungumza, ataketi mahali pake, na Bunge litabaki kimya ili Spika aweze kutoa maelekezo au taarifa yake.

Kuhusu utaratibu

78.-(1) Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno "*Kuhusu Utaratibu*", ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa.

(2) Mbunge aliyedai utaratibu atalazimika kutaja Kanuni au sehemu ya Kanuni ya Bunge iliyokiukwa.

(3) Baada ya kutaja kanuni au sehemu ya Kanuni za Bunge iliyokiukwa, Mbunge aliyesimama kuomba kuhusu utaratibu, ataketi mahali pake kusubiri maelekezo na uamuzi wa Spika.

(4) Spika anaweza, ama papo hapo kutoa uamuzi wake juu ya jambo la utaratibu lililotajwa au kuahirisha uamuzi ili alifikirie zaidi jambo hilo na kutoa uamuzi baadae au kutoa uamuzi na baadae kutoa sababu za uamuzi huo, vyovyote atakavyoamua.

(5) Katika kufikia uamuzi wake, Spika anaweza kuitaka Kamati ya Kudumu ya Kanuni za Bunge au Kamati nyingine yoyote ya Bunge impe ushauri kuhusu jambo husika.

(6) Mbunge aliyekuwa anazungumza wakati jambo la utaratibu lilipohojiwa anaweza kuendelea na hotuba yake baada ya Spika kutoa uamuzi juu ya jambo hilo.

Mwongozo wa Spika

79. Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba *"Mwongozo wa Spika"* kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadae, kadri atakavyoona inafaa.

Taarifa

80.-(1) Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema *"Taarifa"* na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa au ufafanuzi kwa muda wa dakika zisizozidi mbili kwa Mbunge anayesema, ambapo Spika atamtaka Mbunge anayesema aketi kusikiliza taarifa hiyo.

(2) Mtoa taarifa atakapomaliza kutoa taarifa na kuketi, Spika atamuuliza Mbunge aliyekuwa akisema mwanzo kama anaikubali au haikubali taarifa hiyo kabla ya kumruhusu kuendelea kuchangia hoja.

Utaratibu, mwongozo na taarifa

81. Uamuzi wa Spika kuhusu suala lolote la utaratibu, mwongozo au taarifa utakuwa ni wa mwisho.

Hoja ya kuahirisha mjadala

82.- (1) Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadae, anaweza kutoa hoja *"Kwamba mjadala sasa uahirishwe"* na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala huo uahirishwe.

(2) Kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, atakataa kuitoa ili iamuliwe; vinginevyo, papo hapo atawahoji Wabunge juu ya hoja hiyo kadri atakavyoona inafaa.

(3) Endapo hoja iliyowasilishwa haitapata kibali cha Bunge, mjadala kuhusu hoja iliyoko mbele ya Bunge utaendelea.

(4) Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja iliyotolewa kwa mujibu wa kanuni hii.

Hoja ya kufunga mjadala

83.-(1) Utaratibu utakaotumika kufunga mjadala ni kutoa hoja ya kufunga mjadala endapo bado kuna Wabunge wanaopenda kuzungumza juu ya jambo lililoko katika mjadala lakini muda uliotengwa umekwisha au endapo Bunge limewekewa kiwango cha juu cha muda wa kujadili hoja inayohusika na muda huo bado haujaisha.

(2) Hoja ya kufunga mjadala inaweza kutolewa baada ya hotuba yoyote kukamilika au ikiwa Spika ataruhusu hoja ya kufanya mjadala, mara tu au muda mfupi baada ya hoja hiyo kutolewa ili iamuliwe.

(3) Mbunge anayetoa hoja ya kufunga mjadala, anaweza kusimama mahali pake na kutoa hoja "Kwamba mtoa hoja sasa apewe nafasi ya kujibu".

(4) Endapo Spika ataona kuwa hoja ya kufunga mjadala inakiuka mwenendo bora wa Shughuli za Bunge au inavunja haki za Wabunge, basi ataikataa.

(5) Endapo hoja *"Kwamba mtoa hoja sasa apewe nafasi ya kujibu"* itakubaliwa, mtoa hoja atajibu kama akipenda na baada ya hotuba ya kujibu kukamilika au kama mtoa hoja hapendi kujibu basi Spika atawahoji Wabunge ili kuamua hoja hiyo.

Haki ya raia kujitetea na kujisafisha Sura ya 2

84.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 na 101 ya Katiba, mtu yeyote asiye Mbunge, ambaye atajisikia kuwa amepata athari hasi kutokana na kauli au maneno au shutuma zilizotolewa Bungeni kumhusu yeye binafsi, anaweza kupeleka malakamiko pamoja na maelezo yake ya kujitetea kwa Spika yakiwa-

(a) yameandikwa kwa lugha fasaha na ya heshima na yanahitimishwa kwa maelezo ya jumla kuhusu madhumuni yake;
(b) yamewasilishwa katika kipindi cha siku kumi na nne baada ya kauli au maneno yanayolalamikiwa kutolewa;
(c) yamewasilishwa na mtu binafsi ambaye ni raia wa Tanzania na hayajawasilishwa na au kwa niaba ya Kampuni, Shirika au Taasisi;
(d) yanaonesha wazi kuwa, kwa dhahiri mhusika aliathirika yeye binafsi kutokana na kauli au maneno au shutuma zilizotolewa Bungeni;

(e) yanaeleza kwa ufasaha ni jinsi gani mhusika amepata athari hasi, kama vile kuchafuliwa jina lake na heshima yake katika jamii au kuharibu sifa, mahusiano na ushirikiano wake na wengine au kazi yake anayoifanya katika jamii au kuingilia uhuru na maisha yake binafsi na familia yake isivyo halali kutokana na kauli au shutuma zilizotolewa Bungeni; na

(f) yanatoa ombi kwamba, endapo kwa utaratibu uliowekwa na Kanuni yatakubalika, basi maelezo ya utetezi au ufafanuzi yaliyotolewa na mhusika kwa ajili ya kusafisha jina na kurejesha heshima yake yachukuliwe na Bunge kuwa ndiyo majibu sahihi ya kauli au shutuma zilizotolewa Bungeni.

(2) Mara baada ya kupokea malalamiko yaliyowasilishwa kwake kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii na kujiridhisha kuwa malalamiko hayo yameandikwa katika lugha ya heshima na ya kistaarabu na yanatoa hoja mahsusi na ambayo si ya uzushi, uongo, uchochezi au chuki binafsi; na kwamba yanastahili kufikiriwa au kufanyiwa kazi na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Spika atayapeleka malalamiko hayo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili kuyatafakari na kulishauri Bunge.

(3) Katika kuyafanyia kazi malalamiko yaliyopelekwa kwake na Spika kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge-

(a) itakutana katika kikao cha faragha;

(b) inaweza kumhoji mtu aliyewasilisha malalamiko yake kwa Spika au Mbunge au Waziri aliyetoa Bungeni kauli au shutuma zinazolalamikiwa;

(c) haitajadili wala kutoa uamuzi kuhusu ukweli wa kauli au shutuma zilizotolewa Bungeni au ukweli wa maelezo yaliyotolewa kwenye malalamiko husika; na

(d) haitatangaza maelezo yaliyomo kwenye malalamiko husika wala mwenendo wa majadiliano yake kuhusiana na malalamiko husika.

(4) Baada ya kukamilisha kazi yake, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itawasilisha Bungeni, taarifa ya uamuzi wake kuhusu malalamiko husika, pamoja na maelezo yote au sehemu ya maelezo ya malalamiko husika, kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge.

(5) Taarifa itakayowasilishwa Bungeni na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge inaweza kupendekeza mojawapo ya yafuatayo:

(a) maelezo ya utetezi au ufafanuzi ya mlalamikaji, kama yalivyoelezwa kwenye taarifa hiyo, yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge; au

(b) Bunge lisichukue hatua nyingine yoyote.

SEHEMU YA KUMI
AMANI NA UTULIVU BUNGENI

Mamlaka ya Spika kusimamia utaratibu

85.-(1) Spika atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa, utaratibu bora unafuatwa Bungeni, na uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho.

(2) Mbunge atakayekiuka utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi anaweza papo hapo kutakiwa na Spika afuate utaratibu au Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama na kumfahamisha Spika kuhusu ukiukwaji wa utaratibu huo na katika kufanya hivyo, atalazimika kutaja kanuni iliyoweka utaratibu uliokiukwa.

(3) Endapo Mbunge yeyote atatakiwa kuthibitisha ukweli wa jambo au suala alilolisema Bungeni na hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa amekataa au ameshindwa kutoa uthibitisho huo, Spika anaweza kumsimamisha Mbunge huyo kuhudhuria vikao vya Bunge visivyozidi kumi.

Utovu wa nidhamu

86.-(1) Mbunge atakuwa ametenda kosa la utovu wa nidhamu ikiwa-

(a) atatishia kutumia nguvu dhidi ya Mbunge au mtu mwingine ndani ya Ukumbi wa Bunge au kwenye Kamati;

(b) atakiuka maelekezo na mwongozo wa Spika uliotolewa chini ya kanuni ya 74(2); au

(c) atakiuka Kanuni kwa namna yoyote ambayo, kwa maoni ya Spika, ataona kuwa ni utovu wa nidhamu.

(2) Endapo Mbunge atatenda kosa la utovu wa nidhamu kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Spika anaweza-

(a) kumuonya Mbunge huyo na kumtaka ajirekebishe;

(b) kumuamuru Mbunge huyo kutoka nje ya Ukumbi wa Bunge mara moja na abaki huko kwa muda wote uliosalia wa kikao; au

(c) kumsimamisha Mbunge huyo kuhudhuria vikao visivyozidi kumi mfululizo.

Utovu mkubwa wa nidhamu

87.-(1) Mbunge atakuwa ametenda kosa la utovu mkubwa wa nidhamu ikiwa-

(a) atapuuza uamuzi au maelekezo ya Spika au Mwenyekiti wa Kamati;
(b) atasababisha vurugu zinazoweza kuvuruga shughuli za Bunge;
(c) atafanya kosa ambalo aliwahi kuadhibiwa kwa mujibu wa kanuni ya 85 au kanuni ya 86;
(d) atapiga kura zaidi ya mara moja kwenye hoja moja kinyume na Kanuni;
(e) atakataa kufafanua au kuondoa matamshi yasiyo ya kibunge au atakataa kuomba radhi licha ya Spika kumtaka kufanya hivyo;
(f) atadhihirisha au kutoa matamshi ya ubishi dhidi ya uamuzi wa kumsimamisha Mbunge mwingine kutohudhuria vikao;
(g) atajaribu kutenda au atatenda kosa la utovu wa nidhamu wa namna yoyote wakati wa hotuba ya mgeni mashuhuri ndani ya Bunge;
(h) atamshambulia Mbunge au mtu mwingine ndani ya Bunge au kwenye Kamati;
(i) atajaribu kuvuruga au atavuruga msafara wa Spika unapoingia au unapotoka katika Ukumbi wa Bunge;
(j) atatenda jambo ambalo kwa namna nyingine yoyote linashusha hadhi ya Bunge; au
(k) atakiuka Kanuni kwa namna nyingine yoyote ambayo, kwa maoni ya Spika, ataona kuwa ni utovu mkubwa wa nidhamu.

(2) Spika anaweza kutaja jina la Mbunge ambaye ametenda kosa la utovu mkubwa wa nidhamu chini ya kanuni ndogo ya (1) na kisha kupeleka jina hilo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili Kamati hiyo ifanyie kazi shauri hilo na kulishauri Bunge ipasavyo.

(3) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itashughulikia shauri hilo na ikithibitika kuwa Mbunge husika ametenda kosa inaweza kushauri kwamba: -

(a) ikiwa ni kosa lake la kwanza Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyopungua kumi au visivyozidi kumi na tano; au

(b) ikiwa ni kosa lake la pili au zaidi Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyopungua kumi na tano au visivyozidi ishirini.

(4) Bunge linaweza kuzingatia ushauri mwingine wowote utakaotolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu adhabu anayostahili kupewa Mbunge aliyekiuka masharti ya kanuni hii.

(5) Adhabu yoyote itakayotolewa kwa Mbunge aliyekiuka masharti ya kanuni hii itatolewa kupitia Azimio la Bunge ambalo litataja adhabu hiyo pamoja na sababu zake.

(6) Kwa madhumuni ya Sehemu hii-

"matamshi yasiyo ya Kibunge" maana yake ni kutumia maneno ambayo, kwa maoni ya Spika, yanaashiria ujeuri, kukosa adabu, matusi au kutozingatia utaratibu au desturi za kibunge; na

"mgeni mashuhuri" inajumuisha Rais au kiongozi mwingine yeyote aliyealikwa na Bunge.

Utovu wa nidhamu uliokithiri

88.-(1) Mbunge atakuwa ametenda kosa la utovu wa nidhamu uliokithiri ikiwa-

(a) atajaribu kumshambulia au atamshambulia Spika au mgeni mashuhuri;
(b) atajaribu kuondoa au ataondoa siwa mahali pake ukumbini;
(c) atatukana au kutoa ishara ya matusi dhidi ya Spika au mgeni mashuhuri;
(d) ataanzisha, atasababisha au atafanya vurugu ambazo zitasababisha shughuli za Bunge kuahirishwa;
(e) atavuruga msafara wa Spika au mgeni mashuhuri anapongia au kutoka ukumbini;
(f) atarudia kutenda kosa ambalo aliwahi kuadhibiwa kwa mujibu wa kanuni ya 87; au
(g) atakiuka Kanuni kwa namna nyingine yoyote ambayo kwa maoni ya Spika ni utovu wa nidhamu uliokithiri.

(2) Spika atapeleka jina la Mbunge aliyetenda kosa la utovu wa nidhamu uliokithiri kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili Kamati hiyo ifanyie kazi shauri hilo na kulishauri Bunge ipasavyo.

(3) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itashughulikia shauri hilo na ikithibitika kuwa Mbunge husika ametenda kosa inaweza kushauri kwamba Mbunge huyo asihudhurie Mikutano ya Bunge mfululizo isiyopungua miwili au isiyozidi mitatu.

(4) Bunge linaweza kuzingatia ushauri mwingine wowote utakaotolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu adhabu anayostahili kupewa Mbunge aliyekiuka masharti ya kanuni hii au kuazimia kwamba shauri hilo lishughulikiwe kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Sura ya 398

(5) Adhabu yoyote itakayotolewa kwa Mbunge aliyekiuka masharti ya kanuni hii itatolewa kupitia Azimio la Bunge ambalo litataja adhabu hiyo pamoja na sababu zake.

Amani na utulivu kwenye Kamati

89.-(1) Pale ambapo Mbunge atakuwa kwenye Kamati na akatenda kosa lolote miongoni mwa makosa yaliyotajwa kwa mujibu wa kanuni ya 86, 87 au 88, Mwenyekiti wa Kamati atawasilisha kwa Spika jina la Mbunge huyo pamoja na ufafanuzi wa kosa kwa maandishi.

(2) Mbunge ambaye jina lake limewasilishwa kwa Spika kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), atachukuliwa kuwa ametenda kosa ndani ya Bunge na masharti ya kanuni ya 86, 87 au 88 yatazingatiwa.

Amani na utulivu Bunge linapokaa kama Kamati

90. Ikiwa maneno au vitendo vya Mbunge vilivyoainishwa katika kanuni ya 86, 87 au 88 vimetokea wakati Bunge likiwa katika Kamati ya Bunge Zima, Kamati ya Matumizi au Kamati ya Mipango, basi Mwenyekiti atasitisha shughuli za Kamati kwa muda na Bunge litarejea ili kumpatia Spika fursa ya kutoa taarifa kwa Bunge kuhusu mwenendo wa Mbunge huyo na kuchukua hatua kwa mujibu wa Kanuni.

Masharti kwa Mbunge aliyesimamishwa kazi

91.-(1) Mbunge aliyesimamishwa kazi atatoka katika Bunge na hataingia tena katika sehemu yoyote ya Ukumbi wa Bunge na maeneo ya Bunge kwa muda wote atakapokuwa amesimamishwa, na atalipwa nusu mshahara na nusu posho zinazoambatana na mshahara huo.

(2) Masharti ya kanuni ndogo ya (1) kuhusu malipo ya mshahara na posho yatatumika kwa Mbunge aliyewekwa mahabusu kwa kipindi chote atakachokuwa mahabusu.

(3) Endapo Mbunge amehukumiwa na mahakama kutumikia adhabu ya kifungo kwa kosa lolote, Mbunge huyo hatalipwa mshahara wala posho zinazoambatana na mshahara kwa kipindi chote atakachokuwa anatumikia adhabu ya kifungo.

Udhibiti wa fujo Bungeni

92.-(1) Endapo itatokea fujo ndani ya Ukumbi wa Bunge na Spika ataona kuwa kuna haja ya kutumia nguvu kwa madhumuni ya kudhibiti fujo hiyo, anaweza kuahirisha Shughuli za Bunge bila ya hoja yoyote kutolewa au kusitisha kikao kwa muda atakaoutaja ili fujo hiyo iweze kudhibitiwa.

(2) Baada ya utulivu kurudia, Spika atalipeleka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge suala ambalo lilisababisha kutokea kwa fujo ikiwa ni pamoja na jina la Mbunge au majina ya Wabunge waliohusika na fujo hiyo ili Kamati hiyo iweze kulishauri Bunge kuhusu adhabu inayostahili kutolewa.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## UHALALI WA SHUGHULI

Akidi ya Vikao vya Bunge

Sura ya 2

Sura ya 2

93.-(1) Akidi kwa kila kikao cha Bunge wakati wa kufanya uamuzi itakuwa ni nusu ya Wabunge wote kama ilivyofafanuliwa katika ibara ya 94 ya Katiba, isipokuwa kwamba, idadi hiyo haitahusu hoja kuhusu uamuzi wa kubadilisha masharti yoyote ya Katiba kwa mujibu wa ibara ya 98 ya Katiba.

(2) Mbunge yeyote aliyehudhuria anaweza kumjulisha Spika kwamba, Wabunge waliopo ni pungufu ya akidi inayohitajika kwa ajili ya shughuli inayoendelea.

(3) Endapo Spika ataridhika kwamba ni kweli idadi ya Wabunge walio ndani ya Ukumbi wa Bunge ni pungufu ya akidi inayohitajika, basi atasimamisha Shughuli za Bunge kwa muda atakaoutaja na atamwagiza Katibu kupiga kengele.

(4) Bunge litakaporudia baada ya wakati uliotajwa kukamilika, Spika atahakikisha kama idadi ya Wabunge waliopo inafikia akidi inayohitajika ili kuruhusu uamuzi kufanyika.

(5) Endapo Spika ataridhika kwamba bado idadi ya Wabunge waliomo ndani ya Ukumbi wa Bunge haifikii akidi inayohitajika basi ataahirisha Shughuli za Bunge hadi muda mwingine atakao utaja.

Uhalali wa Shughuli za Bunge

94. Shughuli za Bunge hazitakuwa batili kwa sababu tu kwamba nafasi yoyote ya Mbunge ipo wazi.

Uamuzi wa Bunge Sura ya 2

95.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara za 46A, 50(3), 53A na 98 za Katiba, kila hoja itakayotolewa kwa ajili ya kupata uamuzi wa Bunge, itaamuliwa kwa kufuata wingi wa kura za Wabunge waliohudhuria na kupiga kura Bungeni.

(2) Spika, wakati amekalia kiti cha Spika, hatakuwa na kura ya kawaida bali atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura za *"Ndiyo"* na *"Siyo"* zitalingana.

(3) Wakati mjadala kuhusu hoja unapomalizika, Spika atawahoji Wabunge ili kupata uamuzi juu ya hoja hiyo kama ilivyo au baada ya kufanyiwa marekebisho au mabadiliko, Spika kwanza atataka uamuzi wa wale wanaoafiki kwa kusema: - *"Wale wanaoafiki waseme Ndiyo"* na baadae atataka uamuzi wa Wabunge wasioafiki kwa kusema: - *"Wale wasioafiki waseme Siyo.*

(4) Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo katika Kanuni, uamuzi juu ya mambo yote utapatikana kwa kufuata wingi wa sauti za Wabunge za *"Ndiyo"* au *"Siyo"* na Spika atatangaza matokeo ya kura kwa kusema *"Naamini Walioafiki Wameshinda"* au *"Naamini Wasioafiki Wameshinda."*

(5) Endapo itaonekana kuna mashaka kuhusu matokeo ya kura kwa kufuata wingi wa sauti kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (4) ya kanuni hii, Spika ataruhusu muda upite ili kutoa nafasi kuhakikisha uamuzi wa Bunge juu ya jambo hilo na kwa muda huo, ikionekana kuwa kuna mashaka kuhusu matokeo ya kura, Mbunge yeyote anaweza kusimama na kusema "Kura zihesabiwe."

(6) Endapo hakuna Mbunge aliyeomba kura zihesabiwe, Spika atatoa kauli ya uamuzi wa mwisho kwa kusema "Walioafiki Wameshinda" au "Wasioafiki Wameshinda", kulingana na hali itakavyokuwa.

(7) Endapo Mbunge yeyote ataomba kura zihesabiwe, basi Spika ataamuru kura zihesabiwe ikiwa Wabunge wengine kumi au zaidi watasimama mara moja kuunga mkono maombi ya kura kuhesabiwa.

(8) Endapo Spika ataamuru kura zihesabiwe, Katibu atapiga kengele ya kuwaita Wabunge kwa muda wa dakika moja na baada ya muda huo, Spika atamwagiza Katibu kumwita Mbunge mmoja mmoja kwa jina lake na kumuuliza anapiga kura yake upande gani na kurekodi kura ya anayeafiki kwa kusema NDIYO, asiyeafiki kwa kusema HAPANA au asiyetaka kupiga kura kwa kusema SIPIGI KURA.

(9) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo zilizotangulia za kanuni hii, Mbunge yeyote atakayepiga kura juu ya jambo lolote ambalo yeye binafsi ana maslahi nalo ya kifedha atahesabiwa kuwa hakupiga kura.

(10) Baada ya Katibu kukamilisha shughuli ya kuhesabu kura, atamjulisha Spika kuhusu kura zote za NDIYO, HAPANA na SIPIGI KURA na Spika atatangaza matokeo ya hesabu hiyo ya kura.

(11) Orodha kamili itaandaliwa ikionesha namna kura zilivyopigwa na itarekodiwa katika Taarifa Rasmi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya uamuzi wa Bunge.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## KUTUNGA SHERIA – MASHARTI YA JUMLA

Muswada wa Serikali

96.-(1) Kila Muswada wa Sheria wa Serikali utatangazwa kwenye Gazeti.

(2) Tangazo la Muswada wa Sheria litatolewa na kumfikia Katibu katika muda usiopungua siku ishirini na moja kabla ya Muswada huo Kusomwa Mara ya Kwanza Bungeni, na litaonesha Muswada mzima, ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu sababu na madhumuni ya Muswada husika yaliyotiwa saini na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(3) Muswada wowote wa Sheria wa Serikali wa dharura hautaingizwa kwenye shughuli za Bunge bila ya kuwa na hati iliyowekwa saini na Rais inayoeleza kuwa Muswada uliotajwa katika hati hiyo ni wa dharura.

(4) Muswada huo utawasilishwa kwanza kwenye Kamati ya Uongozi ukiwa umeambatishwa na hati ya dharura ili Kamati hiyo iweze kujiridhisha iwapo Muswada husika wa sheria unastahili kuwasilishwa kwa dharura au la.

(5) Iwapo Kamati ya Uongozi itaona kuwa Muswada wa Sheria wa Serikali uliowasilishwa kwa hati ya dharura haustahili kuwasilishwa kwa dharura, Kamati hiyo itaishauri Serikali ipasavyo.

(6) Haitakuwa lazima kwa Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa taarifa ya Muswada wa Serikali ambao unakusudiwa kuwasilishwa Bungeni iwapo Muswada huo umekwishatangazwa kwenye Gazeti.

(7) Katibu atagawa kwa kila Mbunge nakala ya kila Muswada wa Sheria kama ulivyochapishwa na kutangazwa kwenye Gazeti.

Muswada Binafsi
Sura ya 2

97.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 99 ya Katiba,

Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge au Mbunge yeyote anaweza kuwasilisha Bungeni Muswada Binafsi wa Sheria.

(2) Taarifa ya kuwasilisha Muswada Binafsi wa Sheria itapelekwa kwa Katibu na taarifa hiyo itaeleza jina la Muswada unaopendekezwa pamoja na madhumuni na sababu zake.

(3) Baada ya taarifa kutolewa, Muswada Binafsi wa Sheria utatangazwa katika Gazeti kama ilivyo kwa Miswada ya Sheria ya Serikali, isipokuwa kwamba, madhumuni na sababu yatawekwa saini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge au Mbunge anayehusika.

(4) Masharti kuhusu muda wa utangazaji wa Miswada ya Sheria yanaweza kuwekwa kando na kutenguliwa kwa hoja kutolewa na kuamuliwa kama kutawasilishwa Bungeni hati iliyowekwa saini na theluthi mbili ya Wajumbe wote wa Kamati kama ni Muswada wa Kamati na kwa Muswada wa Mbunge hati iliyowekwa saini na Wabunge wasiopungua kumi inayoeleza kuwa Muswada Binafsi uliotajwa katika hati hiyo ni wa dharura.

(5) Masharti ya kujadili hoja hii yatakuwa kama yalivyo kwa upande wa Miswada ya Sheria ya Serikali.

Uwasilishaji wa Muswada

98.-(1) Muswada wa Sheria wa Serikali utawasilishwa Bungeni na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(2) Muswada Binafsi wa Sheria unaweza kuwasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge au Mbunge.

Muswada Kusomwa Mara ya Kwanza

99.-(1) Muswada wowote wa Sheria ambao umetangazwa kwenye Gazeti, unaweza kuwasilishwa Bungeni kufuatana na Orodha ya Shughuli ili Kusomwa Mara ya Kwanza na katika hatua hiyo Katibu atasoma jina refu la Muswada wa Sheria unaohusika bila hoja yoyote kutolewa kwa ajili hiyo.

(2) Hakutakuwa na mjadala wowote wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Kwanza.

Muswada kupelekwa kwenye Kamati

100.-(1) Spika atapeleka Muswada wa Sheria kwenye Kamati inayohusika na Kamati itaanza kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo.

(2) Kamati iliyopelekewa Muswada itatoa matangazo au itatoa barua ya mwaliko kumwalika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya Kamati hiyo kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa Muswada huo.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 99 ya Katiba, Kamati iliyopelekewa Muswada itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho katika Muswada wa Sheria kwa kumshauri Waziri au Mbunge anayehusika na Muswada huo kufanya mabadiliko, vilevile Serikali itakuwa na uwezo wa kuishauri Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu kufanya marekebisho au mabadiliko juu ya Muswada Binafsi.

(4) Kabla Muswada wa Sheria uliofanyiwa mabadiliko haujawasilishwa Bungeni kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Pili, utapelekwa kwenye Kamati inayohusika kwa madhumuni ya kuzingatia mabadiliko hayo.

Taarifa ya Kamati

101.-(1) Kamati iliyopelekewa Muswada wa Sheria itakapokamilisha kuujadili Muswada huo, Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika kwa maandishi kwamba Kamati imemaliza kujadili Muswada husika.

(2) Spika ataagiza Muswada huo uwekwe kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Pili.

Muswada Kusomwa Mara ya Pili

102.-(1) Siku ambayo Muswada wa Sheria umepangwa kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya kusomwa Mara ya Pili-

(a) Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mwenyekiti wa Kamati yenye Muswada binafsi au Mbunge mwenye Muswada binafsi ataweka Mezani maelezo kuhusu Muswada huo;
(b) Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe yeyote atakayeteuliwa kwa niaba yake ataweka Mezani nakala za taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada husika;
(c) Endapo Muswada unaosomwa ni Muswada Binafsi, msemaji wa Serikali ataweka Mezani nakala za taarifa ya maoni ya Serikali kuhusu Muswada huo; na
(d) Iwapo Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni atakuwa na maoni, ataweka Mezani nakala za taarifa ya maoni ya Kambi hiyo kuhusu Muswada husika.

(2) Hoja ya Muswada wa Sheria kusomwa Mara ya Pili itakuwa kama ifuatavyo:

*"Kwamba, Muswada wa Sheria uitwao ……………….. sasa usomwe Mara ya Pili."*

au kadri itakavyokuwa;

*"Kwamba, Muswada wa Sheria uitwao …………….. kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa jedwali la marekebisho au*

*kama ulivyochapishwa upya, sasa usomwe Mara ya Pili."*

(3) Haitakuwa halali katika hatua hii kuleta hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja isipokuwa tu kwamba-

(a) mabadiliko bila kutoa sababu yanaweza kutolewa kwa kusema-

> *"Kwamba, Muswada huu usisomwe Mara ya Pili sasa na badala yake usomwe baada ya .... kuanzia .....", na hapo muda ambao Muswada huo unaokusudiwa kusomwa utatajwa.*

(b) mabadiliko yenye kutoa sababu yanaweza kutolewa kwa kusema:-

> *"Kwamba, Bunge hili likatae Muswada huu Kusomwa Mara ya Pili kwa sababu zifuatazo ……..", na hapo sababu za kupinga Muswada Kusomwa Mara ya Pili zitatajwa kwa ukamilifu.*

(4) Iwapo hoja itatolewa chini ya kanuni ndogo ya 3(a) na (b) ya kanuni hii, Spika atalihoji Bunge ili kufikia uamuzi.

(5) Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekewa Muswada wa Sheria au Mjumbe mwingine wa Kamati aliyeteuliwa kwa ajili hiyo, atatoa maoni ya Kamati kuhusu Muswada husika.

(6) Ikiwa Muswada wa Sheria unaohusika ni Muswada wa Serikali Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache atatoa maoni yake juu ya Muswada husika na endapo ni Muswada Binafsi au Muswada wa Kamati, msemaji wa Serikali atatoa maoni yake.

(7) Mjadala wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili utahusu ubora na misingi ya Muswada huo tu.

(8) Majadiliano juu ya hoja kuhusu Muswada kama yapo yatahusu maneno yanayohusiana na hoja tu.

(9) Mbunge yeyote au Waziri anaweza, wakati wa mjadala huo, kumshauri Mtoa hoja afanye mabadiliko katika Muswada, ama mabadiliko ya jumla au yale atakayoyataja Mbunge.

(10) Katika hatua hii iwapo mtoa hoja anataka kufanya marekebisho au mabadiliko katika Muswada wa Sheria kutokana na ushauri uliotolewa ama katika Kamati au wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili au kwa sababu nyingine yoyote, iwapo Muswada huo ni wa Serikali atamjulisha Mwanasheria Mkuu wa

Serikali na iwapo Muswada husika ni wa Kamati au Binafsi atamjulisha Katibu.

(11) Muswada wa Sheria uliochapishwa upya ukiwa na marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika au Jedwali la Marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika utagawiwa na Katibu kwa Wabunge.

(12) Kamati iliyoshughulikia Muswada au Mbunge yeyote ambaye si mtoa hoja, mwenye Marekebisho ya Muswada husika, atawasilisha Jedwali la Marekebisho kwa Katibu wakati wowote kabla ya kuanza kwa kikao cha siku ambayo Muswada huo utapitishwa, isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo.

Kurejesha Muswada kwenye Kamati

103.-(1) Endapo Muswada ulikwishasomwa Mara ya Pili na haukuwa na mabadiliko, lakini kuna jambo au suala jipya limetokea na linahitaji kuzingatiwa, Mtoa hoja anaweza kumuomba Spika wakati wowote kabla Muswada haujapelekwa katika Kamati ya Bunge Zima kwamba, Muswada huo urejeshwe tena kwenye Kamati inayohusika.

(2) Endapo Muswada wa sheria utapelekwa tena kwenye Kamati inayohusika, Mbunge yeyote ambaye wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili alimuomba mtoa hoja kufanya mabadiliko katika Muswada huo, anaweza kuhudhuria mkutano wa Kamati na kushiriki katika majadiliano, isipokuwa kwamba, Mbunge huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura kuhusu uamuzi wowote wa Kamati hiyo.

(3) Kamati itakutana mapema iwezekanavyo ili kujadili mabadiliko yaliyopendekezwa.

Sura ya 2

(4) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 99 ya Katiba, Kamati inayohusika itakuwa na mamlaka ya kufanya mabadiliko katika Muswada uliopelekwa kwake kwa mujibu wa Kanuni hii kwa-

(a) kumshauri Waziri, Kamati au Mbunge anayehusika na Muswada kufanya mabadiliko katika Muswada huo; au
(b) kupitisha Azimio la kutoa Bungeni, taarifa maalum kuhusu Muswada huo.

(5) Baada ya Kamati kukamilisha kuujadili Muswada kwa mara ya pili, Muswada huo utapelekwa katika Kamati ya Bunge Zima.

(6) Endapo Kamati iliyojadili Muswada kwa mara ya pili itaazimia kuwa taarifa maalum juu ya Muswada huo itolewe Bungeni, basi Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika na taarifa hiyo itatolewa na Mwenyekiti au Mjumbe mwingine wa Kamati kwa niaba

ya Mwenyekiti, kabla Muswada huo haujawasilishwa katika Kamati ya Bunge Zima.

Muswada katika Kamati ya Bunge Zima

104.-(1) Mtoa hoja au Mbunge mwingine anayekusudia kuwasilisha mabadiliko katika Muswada unaojadiliwa, anaweza kumuomba Spika kwamba, hatua ya kuingia katika Kamati ya Bunge Zima iahirishwe hadi wakati atakaoutaja katika ombi lake na Spika atatoa uamuzi wake kadri atakavyoona inafaa.

(2) Mabadiliko yote yaliyopendekezwa kufanyika katika Muswada wa Sheria sharti yawekwe katika Jedwali la Mabadiliko litakaloandaliwa kwa ajili hiyo na kugawiwa kwa Wabunge na katika kujadili na kuyapitisha au kutoyapitisha, vyovyote itakavyokuwa, mabadiliko hayo yatashughulikiwa kwa mpangilio utakaofuata na kwa kuzingatia mtiririko wa ibara za Muswada wa Sheria unaohusika.

(3) Kwa madhumuni ya Bunge kujadili na kupitisha au kutopitisha mabadiliko yaliyopendekezwa, Mtoa hoja atapewa fursa ya kwanza kueleza mapendekezo yake kabla ya mabadiliko mengine yatakayokuwa yamependekezwa na Wabunge wengine.

(4) Mabadiliko yoyote yaliyopendekezwa kufanyika katika Muswada wa Sheria na kuwekwa katika Jedwali la Mabadiliko hayataondolewa na Mtoa hoja, isipokuwa tu kwa idhini ya Spika.

(5) Mtoa hoja anayependekeza kufanya mabadiliko katika Muswada wa Sheria atawasilisha hoja yake ya mabadiliko hayo kwa muda wa dakika tano.

(6) Endapo kuna mabadiliko mengine yamependekezwa kufanyika katika Jedwali la Mabadiliko, basi mabadiliko hayo yaliyopendekezwa awali na ambayo yamo katika Jedwali la Mabadiliko hayatahesabiwa kwamba yameondolewa hadi majadiliano juu ya mabadiliko hayo yatakapokuwa yamefikia mwisho au Waziri, Kamati ya Bunge au Mbunge aliyetoa mapendekezo yaliyomo katika Jedwali la Mabadiliko atakapoomba kwa Spika mapendekezo yake yaondolewe.

(7) Mtoa hoja aliyependekeza mabadiliko yoyote kufanyika katika Muswada wa Sheria na mapendekezo hayo kuwekwa katika Jedwali la Mabadiliko atapewa nafasi ya kuwasilisha na kufunga hoja yake ya mabadiliko.

(8) Baada ya Mtoa hoja kuhitimisha hoja yake ya mabadiliko, Spika atalihoji Bunge ili kupata uamuzi kuhusu hoja hiyo ya mabadiliko.

(9) Muda wa kusema katika Kamati ya Bunge Zima kwa wachangiaji mbalimbali wanaounga mkono hoja ya kufanya

mabadiliko utakuwa dakika tatu.

(10) Kamati ya Bunge Zima itajadili na kupitisha au kufanya mabadiliko na kupitisha Muswada wa Sheria ibara moja baada ya nyingine, isipokuwa kwamba, Mwenyekiti, akiona inafaa, anaweza kuihoji Kamati itoe uamuzi wake kwa sehemu moja yenye ibara kadhaa au ibara zote zilizomo katika sehemu moja ya Muswada.

Taarifa baada ya Muswada Kusomwa Mara ya Pili

105.-(1) Baada ya Kamati ya Bunge Zima kukamilisha kazi ya kupitia Muswada wa Sheria, Bunge litarejea na Mtoa hoja atatoa taarifa Bungeni kwa maneno yafuatayo:

> *"Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria, ibara kwa ibara na kuukubali bila mabadiliko, naomba kutoa hoja."*

au kama kuna mabadiliko yaliyofanywa kwa maneno yafuatayo:

> *"Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria, ibara kwa ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika, naomba kutoa hoja"*

na kisha atatoa hoja-

> *"Kwamba, Muswada wa Sheria wa …………sasa ukubaliwe",*

au kama kuna mabadiliko yaliyofanywa katika Muswada kwa maneno yafuatayo:

> *"Kwamba, Muswada wa Sheria wa .... Kama ulivyorekebishwa au kubadilishwa katika Kamati ya Bunge zima, sasa ukubaliwe."*

Sura ya 2

(2) Hoja ya kupitisha Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba itaamuliwa kwa mujibu wa ibara ya 98 ya Katiba, kwa sababu hiyo, kura zitapigwa kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja katika hatua ya Muswada huo Kusomwa Mara ya Pili.

Kuondoa Muswada Bungeni

106. Mtoa hoja anayewasilisha Muswada wa Sheria anaweza kuuondoa Muswada huo wakati wowote kabla ya Bunge kuhojiwa kutoa uamuzi wake, baada ya kutoa taarifa kwa Spika.

Muswada Kusomwa Mara ya Tatu na kupitishwa na Bunge

107. Baada ya Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Tatu, utahesabika kuwa umepitishwa na Bunge.

Ridhaa ya Rais na hifadhi ya sheria

108.-(1) Muswada wa Sheria kama ulivyopitishwa na Bunge, utatayarishwa chini ya uangalizi na usimamizi wa Katibu kwa kuingiza mabadiliko yote yaliyofanyika na atawasilisha nakala moja ya Muswada huo kwa Rais mapema ili Rais atoe kibali chake kwa mujibu wa ibara ya 97(1) ya Katiba na pia nakala moja kwa Spika kwa taarifa.

Sura ya 2

(2) Nakala halisi ya sheria iliyopata kibali cha Rais itahifadhiwa na Katibu.

Utaratibu wa Kusoma Muswada wa Sheria

109.-(1) Bunge halitashughulikia hatua zaidi ya moja kwa Muswada wowote wa Sheria katika Mkutano mmoja wa Bunge.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, Bunge linaweza kushughulikia Muswada wa Sheria katika hatua zaidi ya moja endapo-

(a) hoja mahsusi itatolewa kwamba Muswada huo ushughulikiwe katika hatua zaidi ya moja;
(b) Spika ataridhika na hoja hiyo; na
(c) Bunge litaafiki hoja hiyo kwa kupiga kura.

(3) Masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii hayatatumika kwa Muswada wa Sheria ya Fedha, Muswada wa Matumizi ya Fedha na Muswada wowote unaowasilishwa kwa hati ya dharura.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## UTARATIBU WA KURIDHIA MIKATABA YA KIMATAIFA

Hoja ya kuridhia Mkataba

110.-(1) Endapo Jamhuri ya Muungano imeingia mkataba wa kimataifa ambao, kwa masharti yake, unahitaji kuridhiwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 63(3)(e) ya Katiba, Waziri husika au Mwanasheria Mkuu wa Serikali atawasilisha kwa Katibu hoja ya kuridhia Mkataba akiambatisha nakala ya Mkataba unaokusudiwa kuridhiwa.

Sura ya 2

(2) Hoja itakuwa na maelezo kuhusu-

(a) jina la Mkataba na mwaka;
(b) maudhui ya Mkataba;

(c) wajibu wa nchi baada ya kujiunga;
(d) uzingatiaji wa Katiba;
(e) uzingatiaji wa sera za nchi;
(f) manufaa pamoja na athari kama zipo, ambazo Tanzania itapata kutokana na Mkataba huo;
(g) mapendekezo ya kutoridhia baadhi ya masharti iwapo Mkataba una masharti hayo; na
(h) jambo lingine lolote lenye tija kwa Taifa.

Spika kupeleka hoja kwenye Kamati

111.-(1) Baada ya hoja hiyo kupokelewa kwa mujibu wa kanuni ya 110, Spika ataipeleka kwenye Kamati inayohusika na kufanyiwa kazi.

(2) Kamati iliyopelekewa hoja itatoa tangazo au barua ya mwaliko kumwalika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya Kamati hiyo kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa Mkataba husika.

Taarifa ya Kamati

112.-(1) Kamati iliyopelekewa hoja itakapokamilisha kushughulikia hoja hiyo, Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika kwa maandishi kwamba Kamati imemaliza kazi yake.

(2) Baada ya kupokea taarifa, Spika ataagiza hoja hiyo iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni.

Hoja kuwasilishwa Bungeni

113.-(1) Siku ambayo hoja ya kuridhia mkataba imepangwa kwenye Orodha ya Shughuli, mtoa hoja atawasilisha hoja kwamba, Bunge lijadili na kukubali kupitisha Azimio la kuridhia Mkataba ambao atautaja kwa jina.

(2) Hoja ya kuliomba Bunge kujadili na kupitisha Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba itawasilishwa Bungeni kwa maneno yafuatayo:

*"KWA KUWA, ……………….*
*NA KWA KUWA, ……………*
*"KWA HIYO BASI, kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 63(3)(e) ya Katiba, Bunge linaazimia kwamba, Mkataba wa (utatajwa kwa jina) uridhiwe."*

(3) Mwenyekiti wa Kamati iliyojadili hoja na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache watawasilisha maoni yao kabla ya hoja kuanza kujadiliwa.

Majadiliano na uamuzi wa hoja

114.-(1) Majadiliano wakati wa kujadili hoja ya kuridhia Mkataba yatahusu masharti ya mkataba husika.

(2) Baada ya majadiliano kukamilika, Spika atamwita mtoa hoja kuhitimisha hoja yake kabla hajalihoji Bunge kupata uamuzi wake.

(3) Uamuzi wa Bunge unaweza kuwa ni Azimio la-

(a) kuridhia masharti yote ya Mkataba;

(b) kuridhia baadhi ya masharti ya Mkataba iwapo Mkataba unaruhusu kufanya hivyo; au

(c) kukataa kuridhia Mkataba husika.

Hifadhi ya nakala ya Azimio

115. Katibu atawasilisha Serikalini Azimio la Bunge kama lilivyopitishwa na atahifadhi nakala ya Azimio hilo.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## UTARATIBU WA KUTUNGA SHERIA KUHUSU MAMBO YA FEDHA

Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango
Sura ya 2

116.-(1) Kwa mujibu wa ibara ya 63(3) (c) ya Katiba, Serikali itawasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa muda mrefu ambao utajadiliwa mapema iwezekanavyo katika Mkutano wowote wa Bunge.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Bunge katika Mkutano wake wa mwezi Oktoba – Novemba kila mwaka, isipokuwa kwa Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, kwa siku zisizopungua tano, litakaa kama Kamati ya Mipango kwa ajili ya kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata.

(3) Katika Mkutano huo, Bunge pamoja na mambo mengine, litapokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu-

(a) Mwongozo wa kuandaa Bajeti ya Serikali;

(b) vyanzo vya mapato ya Serikali; na

(c) Mapendekezo ya Mpango wa Serikali na vipaumbele kuhusu Mpango huo.

(4) Kabla Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali na Mwongozo wa Kuandaa Bajeti kuwasilishwa Bungeni, Kamati ya Bajeti itajadili mapendekezo ya Mpango na Mwongozo huo.

(5) Spika anaweza kuelekeza Kamati ya Bajeti kwa siku zisizozidi saba kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya

kimkakati iliyoainishwa katika Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha unaoisha kabla ya kuikabidhi Mapendekezo ya Mpango wa Taifa na Mwongozo wa kuandaa Bajeti kwa ajili ya kufanyia kazi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (4) ya kanuni hii.

(6) Mjadala kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa-

(a) utatanguliwa na maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti iliyochambua mapendekezo hayo na maoni ya Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni;
(b) utaendelea kwa siku zisizopungua tano; na
(c) utahitimishwa na Serikali kwa kutoa maelezo mafupi kwamba imepokea Maoni na Ushauri wa Bunge.

(7) Mjadala wa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa utahusu mambo ya jumla na Wabunge watachangia na kuishauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Utekelezaji wa sera za kiuchumi, za kifedha, za kodi na vipaumbele katika mpango wa Bajeti ya Serikali.

Masharti kuhusu Muswada, hoja na maombi ya fedha

117. Bunge halitashughulikia Muswada, hoja au ombi lolote lililotolewa na Mbunge au Kamati ya Kudumu ya Bunge endapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atathibitisha kwamba, matokeo ya Muswada, hoja au ombi hilo yatakuwa ni-

(a) kuweka masharti yanayoanzisha au kuongeza kodi yoyote yanayoweza kuongeza kiwango cha matumizi ya fedha zitakazotolewa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Jamhuri ya Muungano au yanayofuta au kupunguza deni lolote inalodaiwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; au
(b) kubadilisha mishahara, marupurupu au masharti ya utumishi, ikiwa ni pamoja na likizo, usafiri na kupandishwa cheo kwa mtumishi yeyote wa umma au kufanya mabadiliko katika Sheria, Kanuni au taratibu zinazohusu pensheni, kiinua mgongo au marupurupu mengineyo ya mtumishi wa umma au ya mjane, watoto wanaomtegemea au wawakilishi wake.

Kuwasilisha dondoo na randama za vitabu vya Bajeti

118.-(1) Kila ifikapo tarehe kumi ya mwezi Machi kila mwaka, kila Wizara itawasilisha kwa Katibu nakala za dondoo za vitabu vya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha unaofuata, pamoja na nakala za randama za Makadirio hayo kulingana na idadi ya Wajumbe wa Kamati, kwa ajili ya kuziwezesha Kamati za Bunge kufanya uchambuzi wa makadirio hayo.

(2) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), iwapo tarehe kumi ya mwezi Machi itakuwa si siku ya kazi, uwasilishwaji huo utafanywa tarehe inayofuata ya siku ya kazi.

Kuwasilisha mapendekezo ya mpango na Bajeti

119.-(1) Tarehe kumi na moja ya mwezi Machi ya kila mwaka au tarehe ya siku nyingine ya kazi inayofuata iwapo tarehe hiyo itakuwa si siku ya kazi, Waziri anayehusika na masuala ya mipango atawasilisha kwa Wabunge, mapendekezo ya Serikali ya mpango kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), siku hiyo pia, Waziri anayehusika na masuala ya fedha, atawasilisha kwa Wabunge, mapendekezo ya Serikali ya kiwango na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(3) Katika hatua ya uwasilishaji kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) na ya (2), hakutakuwa na mjadala wowote kuhusu mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(4) Baada ya mapendekezo ya mpango na Bajeti ya Serikali kuwasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) na (2), Spika atawasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati ya Bajeti ili yafanyiwe uchambuzi na Kamati hiyo itazishauri Kamati za Bunge za Kisekta pamoja na Serikali kuhusu mapendekezo hayo.

Kamati kukagua utekelezaji wa miradi na uchambuzi wa Bajeti

120.-(1) Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya mpango na kiwango na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa Wabunge, Kamati za Bunge za kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa siku zisizozidi saba.

(2) Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(3) Mara baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa taarifa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), Kamati za Kisekta zitaandaa masuala muhimu ya kibajeti yaliyojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti na kuyawasilisha kwa Spika ambaye, kwa kadri atakavyoona inafaa, atayapeleka katika Kamati ya Bajeti.

(4) Siku moja kabla ya kufanya majumuisho kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (5), Kamati ya Uongozi itafanya kikao cha mashauriano na Kamati ya Bajeti kuhusu mambo muhimu

yaliyojitokeza kwenye Kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(5) Katika kipindi cha siku tatu kabla ya Mkutano wa Bajeti kuanza, na wakati Kamati za Bunge za Kisekta zikiendelea na shughuli zake, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti, itafanya majumuisho kuzingatia ushauri wa Kamati za Bunge za Kisekta kuhusu utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha, na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(6) Baada ya Kamati ya Bajeti kushauriana na Serikali kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (5), Kamati ya Uongozi itafanya kikao na Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kupata taarifa ya matokeo ya mashauriano kati ya Kamati hiyo na Serikali.

Kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara

121.-(1) Katika Mkutano wa Bunge wa Bajeti utakaoanza mapema mwezi Aprili kwa kila mwaka, jumla ya siku zisizozidi hamsini na nane zitatengwa kwa ajili ya Bunge kujadili utekelezaji wa Wizara zote wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha, pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Mjadala katika Bunge la Bajeti kwa kila mwaka utaanza na Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na kufuatiwa na Hotuba za Bajeti za Wizara nyingine zote, kwa utaratibu utakaopangwa na Spika, baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi.

(3) Shughuli za Bajeti zitapewa nafasi ya kwanza kabla ya Shughuli nyingine yoyote, na zitawekwa kwanza kwenye Orodha ya Shughuli za kikao kila siku hadi pale zitakapokuwa zimemalizika, isipokuwa kama Bunge litaamua vinginevyo.

(4) Kabla ya taarifa za utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kujadiliwa Bungeni, zitachambuliwa na Kamati za Bunge za Kisekta, kwa utaratibu uliowekwa na kanuni ya 120(2) na Nyongeza ya Nane ya Kanuni.

(5) Siku ambayo Waziri amepangiwa kuwasilisha hoja ya Makadirio ya Wizara yake, Waziri, Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au mjumbe yeyote atakayeteuliwa kwa niaba yake, na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni kwa Wizara husika Wataweka Mezani nakala ya taarifa zao kwa kuzingatia mpangilio wa Shughuli za Bunge.

(6) Pamoja na kuwasilisha Mezani nakala ya Hotuba ya hoja ya Makadirio ya Wizara, Waziri atawasilisha pia nakala kumi za randama ya makadirio hayo, siku moja kabla ya siku ambayo Hotuba yake imepangwa kusomwa Bungeni.

(7) Wakati utakapofika wa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara inayohusika, hoja itatolewa kwa maneno yafuatayo: -

*"Kwamba sasa Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu."*

(8) Isipokuwa kwa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, muda wa Waziri anayewasilisha Hotuba ya Bajeti utakuwa ni dakika zisizozidi sitini.

(9) Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja.

(10) Wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara, muda wa Wabunge kuchangia utatolewa kulingana na uwiano wa idadi ya Wabunge kutoka katika kila chama.

(11) Idadi ya Wabunge watakaopewa nafasi ya kuchangia Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (10) itaamuliwa na Spika.

(12) Mbunge anayejadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika kumi:

Isipokuwa kwamba, Kambi za Vyama zinaweza kupendekeza kwa Spika kugawa muda huo kwa Wabunge wasiozidi wawili, mapema kabla ya mjadala huo kuanza.

(13) Endapo Spika ataona kuwa muda uliotengwa kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Wizara inayohusika umekaribia kuisha, atafunga mjadala ili kumpatia Waziri Mtoa Hoja nafasi ya kujibu masuala yaliyoibuliwa wakati wa mjadala ndani ya muda wa dakika sitini.

(14) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 178, maneno yoyote ya utangulizi, utambulisho, salamu za pole, pongezi au shukrani, pamoja na kutaja majina ya Wabunge waliochangia hoja havitaruhusiwa kwa Mbunge au Waziri wakati wa kujadili Hotuba ya Bajeti.

Kamati ya Matumizi

122. Mjadala wa jumla kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Wizara utakapomalizika, Bunge litaingia katika Kamati ya Matumizi ili kupitisha Makadirio ya Wizara husika kifungu kwa kifungu.

Mjadala katika Kamati ya Matumizi

123.-(1) Katika Kamati ya Matumizi, Mwenyekiti atawahoji Wajumbe kuhusu kifungu kimoja kimoja cha Makadirio ya Matumizi, na kila kifungu kitaafikiwa peke yake.

(2) Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo

zaidi katika kifungu chochote cha Fungu linalohusika, wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi.

(3) Mbunge atakayeamua kutumia kifungu chenye mshahara wa Waziri, ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahsusi la sera na hatazungumzia zaidi ya jambo moja.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (3), Kamati za vyama zitawasilisha kwa Spika majina ya Wabunge watakaoomba kupata ufafanuzi wa suala mahsusi la sera, na Spika atataoa nafasi kwa Wabunge kwa kuzingatia uwiano.

(5) Muda wa kusema katika Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kuomba au kutoa ufafanuzi hautazidi dakika tano.

Kubadilisha Makadirio katika Kamati ya Matumizi

124.-(1) Katika Kamati ya Matumizi, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika Makadirio ya Matumizi ya Serikali iwapo mabadiliko hayo hayatabadili madhumuni ya Fungu.

(2) Endapo hoja iliyotolewa kwa ajili ya kupunguza kifungu fulani katika Fungu lolote haijapitishwa, hoja nyingine bado inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kupunguza kifungu kingine cha Fungu hilo hilo.

Hoja ya kuondoa shilingi kwenye Makadirio

125.-(1) Kwa kuzingatia utaratibu wa majadiliano uliowekwa na Kanuni, Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha Fungu linalohusika, wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi.

(2) Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote cha Fungu hilo.

(3) Madhumuni ya hoja ya aina hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyeitoa aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahsusi ambalo dhahiri linahusika na kifungu hicho.

(4) Hoja ya aina hiyo itatolewa kwa muda usiozidi dakika tano.

(5) Wabunge wanaweza kuchangia hoja ya kuondoa shilingi moja iliyoanzishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) kwa muda usiozidi dakika tatu kila mmoja.

(6) Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu ya hoja hiyo.

(7) Mbunge aliyetoa hoja ya kuondoa shilingi ndiye atakayefunga mjadala wa hoja hiyo.

(8) Muda utakaotumiwa na Waziri na Mbunge kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (6) na (7) utaamuliwa na Spika.

(9) Endapo Mbunge atashikilia hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu hicho, basi kura itapigwa kwa kuhoji wanaoafiki na wasioafiki hoja hiyo.

(10) Endapo hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote itakubalika, basi kifungu hicho kitakuwa kimepitishwa kikiwa pungufu ya hiyo shilingi moja.

(11) Endapo hoja iliyotolewa kwa ajili ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote cha Fungu linalohusika imekataliwa, hoja nyingine yenye madhumuni ya kuondoa shilingi moja katika kifungu kingine cha Fungu hilo hilo bado inaweza kutolewa.

Kukamilika mjadala katika Kamati ya Matumizi

126.-(1) Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu, Mwenyekiti anaweza kuongeza muda usiozidi dakika thelathini bila kuihoji Kamati ili kukamilisha Shughuli ya kupitisha mafungu yaliyobaki.

(2) Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kumalizika muda ulioongezwa chini ya kanuni ndogo ya (1) na Kamati bado haijamaliza kupitisha mafungu yote, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yanayoendelea na papo hapo atawahoji Wajumbe kuhusu mafungu yaliyosalia, kama yapo.

(3) Baada ya Kamati ya Matumizi kumaliza kazi ya kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara na Bunge kurudia, waziri mtoa hoja atatoa taarifa kwamba-

*"Mheshimiwa Spika, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake"*

na kuomba kwamba:

*"Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge"*

na atahitimisha kwa kusema:

*"Naomba kutoa hoja"*

(4) Baada ya taarifa ya mtoa hoja, Spika atalihoji Bunge ili kupata uamuzi.

Hotuba ya Bajeti ya Serikali Kusomwa Bungeni

127.-(1) Baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa Makadirio ya Wizara zote, ndani ya siku sita kabla ya Hotuba ya Bajeti Kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti

itafanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha, na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kanuni ndogo ya (1), Kamati za Kisekta zitaandaa hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata na kuziwasilisha kwa Spika ambaye, kwa kadri atakavyoona inafaa, atazipeleka katika Kamati ya Bajeti.

(3) Katika kipindi cha kufanya majumuisho kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Bunge litaendelea na shughuli zake nyingine kama zitakavyokuwa zimepangwa na Spika baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi.

(4) Wakati Serikali ikifanya majumuisho kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwa nafasi zao, watakuwa wajumbe wa Kamati ya Bajeti.

(5) Makadirio ya Fedha za Matumizi ya Serikali yatawasilishwa Bungeni na Waziri anayehusika na masuala ya fedha kwa Hotuba kuhusu Makadirio hayo itakayoitwa Hotuba ya Bajeti ya Serikali ambayo itasomwa Bungeni kabla ya tarehe ishirini ya mwezi Juni kila mwaka.

(6) Kikao cha Bunge kwa siku ya kusomwa Hotuba ya Bajeti ya Serikali kitarejea saa kumi kamili alasiri au wakati mwingine utakaoamuliwa na Spika na muda wa Waziri kusoma Hotuba ya Bajeti ya Serikali utaamuliwa na Spika kadri atakavyoona inafaa.

(7) Hoja ya kuwasilisha Makadirio hayo itakua katika maneno yafuatayo:

> *"Kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa ..."*

(8) Siku ya kuwasilisha Bungeni Hotuba ya Bajeti ya Serikali, nafasi itatolewa kwanza kwa Waziri anayehusika na mipango au uchumi kutoa maelezo kuhusu hali ya uchumi kwa ujumla.

(9) Hotuba ya Bajeti ya Serikali na ya Waziri anayehusika na mipango, zitafuatiwa na hotuba za Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni.

(10) Muda wa kusoma maoni ya Kamati na ya Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni, utakuwa dakika zisizozidi thelathini kwa kila hotuba.

Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti

128.-(1) Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Serikali utaendelea kwa siku zisizozidi saba, ambapo dakika zisizozidi kumi zitatolewa kwa kila Mbunge anayetaka kuchangia Hotuba hiyo.

(2) Katika hatua hii, majadiliano yatahusu mambo ya jumla ya hali ya uchumi na Mbunge yeyote hataruhusiwa kupendekeza mabadiliko katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali.

Kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Serikali
Sura ya 2

129.-(1) Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Serikali utakapomalizika, Spika atalihoji Bunge litoe uamuzi wake wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya ibara ya 63(3)(b) na 90(2)(b) ya Katiba.

(2) Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja.

(3) Spika atamwagiza Katibu kuita jina la Mbunge mmoja mmoja ili Mbunge huyo aseme anapiga kura yake upande gani na Katibu atarekodi kura za wanaoafiki kwa kusema NDIYO, wasioafiki kwa kusema HAPANA na wasiotaka kupiga kura kwa kusema SIPIGI KURA.

(4) Baada ya Katibu kukamilisha shughuli ya kuhesabu kura, atamjulisha Spika kuhusu kura zote za *NDIYO*, *HAPANA* na *SIPIGI KURA* na Spika atatangaza matokeo ya kura na Uamuzi wa Bunge.

Muswada wa Fedha za Matumizi

130.-(1) Kabla ya tarehe 30 ya mwezi Juni kwa kila mwaka, baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka unaohusika, Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi utawasilishwa Bungeni na kupitishwa mfululizo katika hatua zake zote.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "Muswada wa Fedha za Matumizi" maana yake ni Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(3) Muswada wa Fedha za Matumizi hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ya Kudumu wala Kamati ya Bunge Zima, na masharti kuhusu Miswada Kusomwa Mara ya Kwanza hayatatumika.

(4) Muswada wa Fedha za Matumizi hautatangazwa kwenye Gazeti kabla haujawasilishwa Bungeni.

Muswada wa Sheria ya Fedha

131.-(1) Baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kupitisha Muswada wa Fedha za Matumizi, Muswada wa Sheria ya Fedha utajadiliwa na kupitishwa kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na

Sehemu ya Nane ya Kanuni.

(2) Marekebisho au mabadiliko ya kupunguza kiwango cha kodi katika ibara yoyote ya Muswada wa Sheria ya Fedha yatakayopendekezwa na Mbunge yeyote hayatakubaliwa iwapo hayatatoa mapendekezo mbadala yanayoziba pengo linalotokana na punguzo linalopendekezwa.

Makadirio ya matumizi ya nyongeza

132. Mapendekezo yoyote kwa ajili ya Matumizi ya Nyongeza ya Fedha za Serikali au kwa ajili ya kutoa fedha yoyote ya nyongeza zaidi ya Fedha za Matumizi ya Mwaka huo-

(a) yataitwa Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi;

(b) yatapelekwa kwenye Kamati ya Matumizi kufuatana na masharti ya ibara ya 99 ya Katiba; na

Sura ya 2

(c) yatafuata masharti ya kanuni zinazohusu Makadirio ya Mwaka ya Matumizi ya Serikali.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## KAMATI ZA BUNGE

Mkutano wa Wabunge wote

133.-(1) Kutakuwa na Mkutano wa Wabunge wote ambao unaweza kuitishwa na Spika siku moja kabla au wakati wa Mkutano wowote wa Bunge.

(2) Mkutano wa Wabunge wote utajadili masuala yote yenye maslahi kwa Wabunge na utaipa Serikali fursa ya kutoa taarifa mbalimbali kwa Wabunge kuhusu hali ya nchi kwa ujumla.

(3) Mwenyekiti wa Mkutano wa Wabunge wote atakuwa ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

(4) Spika anaweza, kwa kadri atakavyoona inafaa, kuitisha kikao cha Spika na Wabunge wote ili kujadili masuala mbalimbali ya kibunge kabla ya Mkutano wa Kamati ya Wabunge wote.

Kamati za vyama vya siasa

134.-(1) Wabunge wa kila chama cha siasa kinachowakilishwa Bungeni wanaweza kuunda Kamati ya Wabunge wa chama kwa kuzingatia Katiba, kanuni na taratibu za chama kinachohusika.

(2) Endapo makubaliano yamefikiwa baina ya vyama viwili au zaidi vyenye Wabunge wachache na idadi sawa ya Wabunge ambao ni zaidi ya asilimia kumi na mbili na nusu basi Wabunge wa Kambi ya Wabunge Walio Wachache wanaweza kuunda Kamati ya Wabunge wote wa Kambi ya Wabunge Walio Wachache.

Vikao vya Kamati za vyama vya siasa

135.-(1) Kamati za vyama vya siasa Bungeni zitajiwekea utaratibu kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao.

(2) Majadiliano yote katika vikao vya Kamati pamoja na mambo mengine yote yanayohusu Kamati hizo yatakuwa na hadhi, kinga na nafuu zote zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria kuhusu majadiliano, kumbukumbu na mambo mengineyo ya Bunge na vikao vyake kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 100(1) na (2) ya Katiba na Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge.

Sura ya 2
Sura ya 296

Bunge linapokaa kama Kamati

136. Kwa kufuata yaliyomo kwenye Orodha ya Shughuli au kwa mujibu wa Kanuni, ukifika wakati wa Bunge au Bunge likihitajika kukaa kama Kamati Spika ataondoka kwenye Kiti chake bila hoja yoyote kutolewa.

Kamati ya Bunge Zima na Kamati ya Matumizi

137.-(1) Masharti ya kanuni ya 93 yatatumika kuhusu Kamati ya Bunge Zima na Kamati ya Matumizi, ila tu kama idadi ya Wabunge waliohudhuria itakuwa bado haifikii nusu ya Wabunge wote baada ya kipindi kilichowekwa na kanuni ya 93(3), Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti, Bunge litarudia na Katibu atahesabu idadi ya Wabunge waliohudhuria na kama idadi yao itakuwa bado haifikii nusu ya Wabunge wote, basi Spika ataahirisha Bunge.

(2) Kanuni za Bunge zinazohusu mwenendo wa Bunge zitatumika katika Kamati ya Bunge Zima na Kamati ya Matumizi, isipokuwa kwamba, katika Kamati hiyo-

(a) hoja ikitolewa haitahitaji kuungwa mkono; na
(b) kwa idhini ya Mwenyekiti, Mjumbe anayetaka ufafanuzi anaweza kuzungumza mara mbili juu ya suala hilo.

(3) Mjumbe yeyote anaweza kuchangia katika hoja ya kutaka ufafanuzi iliyoanzishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2)(b).

(4) Muda wa kusema katika kuchangia hoja ya ufafanuzi hautazidi dakika tano.

(5) Mjumbe yeyote anayetaka kutoa hoja kwamba majadiliano ya Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi yaahirishwe mpaka wakati mwingine, anaweza kutoa hoja hiyo wakati wowote, kwa maneno yafuatayo:

> *"Kwamba Bunge lirejee ili mtoa hoja atoe taarifa kwa Bunge juu ya hatua iliyofikiwa na Kamati na kuomba ruhusa Kamati ikutane tena baadae."*

(6) Bunge litakaporejea kutoka kwenye Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi, mtoa hoja atasimama mahali pake na

kuliarifu Bunge kwamba Kamati haijamaliza kushughulikia hoja iliyopelekwa kwake na kuliomba Bunge kukubali Kamati ikutane tena baadae kuendelea na kazi yake.

(7) Mara tu baada ya Waziri au Mbunge aliyehusika na shughuli zilizokuwa zikifanywa na Kamati kuliarifu Bunge kutokamilika kwa kazi yake, Spika atalitaarifu Bunge siku na wakati ambapo Kamati itaendelea na kazi yake.

(8) Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi itazingatia mambo yale tu yatakayopelekwa na Bunge kwenye Kamati hiyo.

(9) Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi inaweza kuamua, baada ya hoja kutolewa, kwamba shughuli iliyo mbele yake wakati huo irudishwe au ipelekwe kwenye Kamati ya Kudumu inayohusika.

(10) Baada ya Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi kukamilisha shughuli zake, Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti na kurejea kwenye Kiti cha Spika ambapo Bunge litarudia.

Muundo wa Kamati za Kudumu za Bunge

138.-(1) Mbunge yeyote ambaye si Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge inayohusika na kanuni hii.

(2) Waziri mwenye dhamana ya jambo lolote linalopelekwa au kujadiliwa na Kamati, pamoja na Naibu Waziri aliyeteuliwa kumsaidia Waziri huyo, watakuwa wajumbe wa Kamati wakati Kamati itakapokuwa inashughulikia jambo hilo.

(3) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, Mbunge yeyote ambaye ni Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya hatachaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

(4) Wajumbe wa Kamati zote watateuliwa na Spika kwa namna ambayo itawezesha kila Mbunge kuwekwa kwenye Kamati mojawapo.

(5) Wajumbe walioteuliwa kwenye Kamati ya Kanuni za Bunge na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge au Kamati nyingine kwa kadri Spika atakavyoona inafaa wanaweza pia kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati nyingine.

(6) Wakati wa kuteua Wabunge kuwa Wajumbe wa Kamati mbalimbali, Spika-

(a) atateua idadi ya Wabunge inayolingana kwa kila Kamati, isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo katika Kanuni;

(b) atazingatia aina zote za Wabunge na kuwateua Wabunge wa aina mbalimbali kwa kila Kamati, akiongozwa na

kigezo cha asilimia ya kila aina ya Wabunge hao ilivyo Bungeni;

(c) kwa kadri inavyowezekana, atayapa kipaumbele matakwa ya Wabunge wenyewe, lakini hatalazimika kutosheleza kila takwa au ombi; na

(d) atazingatia haja kwa kila Kamati kuwa na Wabunge wenye uzoefu au ujuzi maalum kuhusu kazi za Kamati hiyo.

(7) Katibu atahakikisha kuwa Wabunge wote wanapewa orodha inayoonesha jinsi walivyoteuliwa katika Kamati mbalimbali.

(8) Ujumbe katika Kamati za Kudumu za Bunge utadumu mpaka mwisho wa Mkutano wa Kumi wa Bunge ambao ni nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge.

(9) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (8) ya kanuni hii, Mbunge yeyote anaweza kuteuliwa tena katika Kamati aliyokuwa anaitumikia katika nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge.

(10) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (8) ya kanuni hii, Mbunge atakoma kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge endapo atateuliwa kuwa Waziri au kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika.

(11) Wajumbe wa kila Kamati watawachagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kutoka miongoni mwao ambao kwa muda wote watakaokuwa Wabunge, wataendelea kushika nafasi hizo mpaka mwisho wa kipindi kilichotajwa katika kanuni ndogo ya (8) ya kanuni hii, lakini wanaweza kuchaguliwa tena.

(12) Wenyeviti wa Kamati za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za Umma ambazo ni Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa watachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Kamati hizo ambazo wanatoka katika Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni.

Utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge

139.-(1) Masharti ya kanuni hii yatatumika kwa Kamati zote za Kudumu za Bunge.

(2) Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya Kamati na endapo Mwenyekiti hayupo kwenye kikao, Makamu Mwenyekiti ataongoza shughuli za kikao hicho na ikiwa Mwenyekiti na Makamu wake wote hawapo, wajumbe waliohudhuria watamchagua mjumbe mmojawapo kutoka miongoni mwao kuongoza kikao hicho.

(3) Kamati ya Kudumu itakutana kila inapoitwa na Spika au Mwenyekiti wake baada ya kupata idhini ya Spika.

(4) Mikutano ya kawaida ya Kamati za Kudumu itafanyika Dodoma, Dar es Salaam au Zanzibar.

(5) Kila Kamati itafanya vikao vyake kwa kuzingatia bajeti ya Kamati husika ambayo imeidhinishwa kwa mwaka huo wa fedha.

(6) Akidi ya mkutano wowote wa Kamati ya Kudumu itakuwa theluthi moja ya Wajumbe wote wa Kamati.

(7) Mambo yote yatakayojadiliwa na Kamati yataamuliwa kwa kufuata maoni ya walio wengi kati ya Wajumbe wa Kamati waliohudhuria na kupiga kura.

(8) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya kanuni hii, kila Kamati itajiwekea utaratibu wake, na Kamati inaweza kuwaruhusu Wabunge ambao si Wajumbe wa Kamati au watu ambao si Wabunge kuhudhuria na kushiriki katika shughuli za Kamati, lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

(9) Shughuli za kawaida za Kamati zitaendeshwa kwa uwazi ambapo Kamati itaalika wadau ili kupata maoni na ushauri wao kwa ajili ya kuboresha Muswada au jambo ambalo litakuwa linashughulikiwa na Kamati hiyo.

(10) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (9) ya kanuni hii, shughuli zote za Kamati zinazohusu kuandaa na kutoa mapendekezo ya kuwasilishwa Bungeni zitafanywa kwa faragha.

(11) Maoni ya Kamati yatakuwa ni yale yaliyokubaliwa na wajumbe walio wengi na kuwasilishwa Bungeni na Mwenyekiti au Mjumbe mwingine.

(12) Mjumbe yeyote wa Kamati hataruhusiwa kuzungumzia hadharani maoni ya Kamati kuhusu Muswada au jambo lolote litakalokuwa linashughulikiwa na Kamati kabla maoni hayo hayajawasilishwa rasmi Bungeni.

(13) Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mwakilishi wake, atahudhuria kila mkutano wa kila Kamati ya Kudumu inapokuwa inachambua Muswada wa Sheria.

(14) Kamati ambayo Spika ataipelekea Muswada au suala lolote kwanza, itahesabiwa kuwa ndiyo Kamati inayoshughulikia Muswada huo au suala hilo.

(15) Itakuwa ni lazima kwa kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha Bungeni taarifa ya mwaka ya shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

(16) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (15), Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa zitawasilisha Taarifa kuhusu Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma itawasilisha Taarifa kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya

Umma katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Oktoba-Novemba.

(17) Serikali itawasilisha utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa zilizowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (16) katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Januari-Februari ambapo Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa zitawasilisha Taarifa za utekelezaji wa Maazimio husika Bungeni:

Isipokuwa kwamba katika Mkutano wa Bunge mwingine wowote Kamati hizo zinaweza kupewa nafasi ya kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

(18) Taarifa ya Kamati inapowasilishwa Bungeni, itashughulikiwa kwa kufuata mpangilio wa Shughuli za Bunge.

(19) Spika ataweka utaratibu wa kujadili taarifa za Kamati na endapo Kamati yoyote katika kutekeleza majukumu yake, itaona kuwa kuna mambo ya utekelezaji ambayo yanahitaji kurekebishwa, inaweza kutoa taarifa maalum ya ushauri kwa Waziri mwenye dhamana juu ya mambo hayo ili Waziri aweze kuchukua hatua zinazostahili.

(20) Kamati yoyote inaweza kuunda Kamati Ndogo kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake, kadri itakavyoona inafaa na kila Kamati Ndogo itapangiwa kazi zake na Kamati ya Kudumu inayohusika.

(21) Mjumbe wa Kamati yoyote hataruhusiwa kuzungumzia au kushughulikia jambo lolote lililofikishwa katika Kamati iwapo ana maslahi binafsi ya kifedha katika jambo hilo au idara hiyo isipokuwa anaweza kufanya hivyo baada ya kutaja jinsi anavyohusika na kiwango cha maslahi aliyonayo.

Kamati za Kudumu za Bunge

140.-(1) Kutakuwa na Kamati za Kudumu za Bunge kama zilivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni.

(2) Muundo na majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge yameainishwa kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni.

Majukumu ya nyongeza ya Kamati za Kudumu za Bunge

141. Mbali na majukumu ya msingi ambayo yameorodheshwa kwa kila Kamati ya Kudumu, Kamati yoyote inaweza kupendekeza kwa Spika ipewe majukumu ya nyongeza ambayo yatatajwa katika pendekezo hilo na Spika anaweza kukabidhi jambo lingine lolote kwa Kamati yoyote kadri atakavyoona inafaa, kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Kamati hiyo.

Utaratibu wa kuunda Kamati

142.-(1) Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa

Teule

madhumuni maalum kwa hoja mahsusi itakayotolewa na kuafikiwa.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, baada ya kujadili hoja yoyote, Bunge linaweza kuunda Kamati Teule kwa madhumuni ya kushughulikia jambo lolote lililotokana na hoja hiyo kwa utaratibu ufuatao:

(a) baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa, Mbunge yeyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya kanuni hii anaweza kusimama mahali pake na kutoa taarifa kwa njia ya mdomo kwamba anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule; na

(b) Mbunge ambaye anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule atawasilisha taarifa ya hoja yake kwa njia ya maandishi kwa Katibu na hoja hiyo itashughulikiwa wakati unaofaa kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli kama ulivyoainishwa chini ya kanuni ya 38(4).

(3) Bunge litapeleka jambo linalotokana na hoja iliyokuwa ikijadiliwa Bungeni kwenye Kamati Teule.

(4) Wajumbe wa Kamati Teule watateuliwa na Spika na watakutana kwa ajili ya kumchagua Mwenyekiti wa Kamati hiyo kutoka miongoni mwao.

Akidi na utaratibu wa vikao vya Kamati Teule

143.-(1) Kila Kamati Teule itakuwa na Wajumbe wasiozidi watano.

(2) Akidi ya vikao vya Kamati Teule itakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe wake.

(3) Kamati Teule itafanya kikao chake cha kwanza mahali na saa atakayoamua Mwenyekiti na vikao vingine vitafanyika kwa wakati na mahali popote itakapoamua.

(4) Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya Kamati Teule, na iwapo Mwenyekiti hayupo katika kikao chochote, Wajumbe waliohudhuria watamteua mmoja wao kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.

(5) Endapo kwa sababu yoyote Mjumbe yeyote wa Kamati Teule atashindwa kufanya kazi yake, Spika atamteua Mbunge mwingine kushika nafasi yake.

(6) Majadiliano ya Kamati Teule yatahusu masuala yaliyopelekwa na Bunge katika Kamati hiyo na yatakuwa ya wazi au siri kwa kadri Kamati itakavyoamua kulingana na masuala husika.

Taarifa ya Kamati Teule

144.-(1) Kamati Teule itatoa taarifa Bungeni kuhusu maoni na uchunguzi wake pamoja na kumbukumbu za ushahidi uliopokelewa

na inaweza kutoa taarifa maalum juu ya mambo yoyote ambayo itaona yanafaa kuwasilishwa Bungeni.

(2) Taarifa ya Kamati Teule itawasilishwa Bungeni na Mwenyekiti.

(3) Iwapo baada ya hoja kutolewa, Bunge litaamua kujadili taarifa hiyo, hoja itakayotolewa Bungeni itakuwa ni kwa madhumuni ya kuliomba Bunge likubali mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

(4) Bunge linaweza kuamua vinginevyo kwa kutumia utaratibu wa kubadilisha hoja ambao umeelezwa katika kanuni ya 67.

(5) Katibu wa Kamati Teule ataweka kumbukumbu zinazoonesha majina ya Wajumbe waliohudhuria vikao vya Kamati na uamuzi uliofikiwa.

(6) Kumbukumbu zitakazowekwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (5) ya kanuni hii zitawekwa saini na Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati na zitaambatishwa kwenye Taarifa ya Kamati na kuwasilishwa Bungeni pamoja na taarifa hiyo.

Muundo wa Taarifa za Kamati

145. Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni itakuwa katika muundo ufuatao:

(a) Sehemu ya Utangulizi, ambayo itaonesha-
   (i) hadidu za rejea ambazo Kamati ilipewa;
   (ii) maelekezo yoyote yaliyotolewa kwa Kamati;
   (iii) njia au mbinu zilizotumika na Kamati katika kutekeleza majukumu yake; na
   (iv) masuala mengine kama yapo, ambayo yalijitokeza wakati wa uchunguzi;
(b) Sehemu ya Katikati, ambayo itatoa maelezo kamili kuhusu jambo au mambo yote yaliyofanyiwa Uchunguzi na Kamati; na
(c) Sehemu ya Mwisho, ambayo itatoa maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge.

Kamati ya Pamoja

146.-(1) Bila ya kuathiri masharti mengine kuhusu muundo na majukumu ya Kamati, Spika anaweza kuunda Kamati ya Pamoja itakayojumuisha Kamati za Bunge mbili au zaidi, kwa ajili ya kulifanyia kazi jambo ambalo ataona linahitaji kufanyiwa kazi na Kamati ya Pamoja.

(2) Kamati iliyoundwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1) itafanya kazi kwa kuzingatia hadidu za rejea zitakazotolewa na Spika na itaongozwa na Mwenyekiti

atakayeteuliwa na Spika.

(3) Akidi ya Kikao cha Kamati itakuwa ni theluthi moja ya Wajumbe wa kila Kamati ya Bunge inayounda Kamati hiyo.

(4) Baada ya Kamati kukamilisha kazi yake, Kamati itaandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Spika ambaye ataifanyia kazi kwa namna atakavyoona inafaa.

Kamati Maalum

147.-(1) Spika anaweza kuunda Kamati Maalum kwa lengo la kushughulikia jambo mahsusi.

(2) Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati watateuliwa na Spika kutoka miongoni mwa Wabunge kwa kadri atakavyoona inafaa.

(3) Kamati itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia hadidu za rejea zitakazotolewa na Spika.

(4) Akidi ya kikao cha Kamati itakuwa ni nusu ya wajumbe wa Kamati.

(5) Baada ya Kamati kukamilisha kazi itaandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Spika ambaye ataifanyia kazi kwa namna atakavyoona inafaa.

(6) Katibu wa Kamati Maalum ataweka kumbukumbu zinazoonesha majina ya Wajumbe waliohudhuria vikao vya Kamati na uamuzi uliofikiwa.

(7) Kumbukumbu zitakazowekwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (6) ya kanuni hii zitawekwa saini na Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati na zitaambatishwa kwenye Taarifa ya Kamati.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## UTARATIBU WA KUMWONDOA RAIS MADARAKANI

Taarifa ya hoja ya kumwondoa Rais
Sura ya 2

148. Mbunge yeyote anaweza kuwasilisha kwa Spika Taarifa ya Hoja ya Kumshtaki Rais kwa madhumuni ya kumwondoa Rais madarakani kupitia Azimio la Bunge kwa mujibu wa ibara ya 46A ya Katiba ikiwa inadaiwa kwamba Rais-

Sura ya 2
Sura ya 398

(a) ametenda vitendo ambavyo kwa ujumla vinavunja Katiba au Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

Sura ya 2

(b) ametenda vitendo ambavyo vinakiuka maadili yanayohusu uandikishwaji wa vyama vya siasa yaliyotajwa katika ibara ya 20(2) ya Katiba; au

(c) amekuwa na mwenendo unaodhalilisha Kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano:

Isipokuwa kwamba, hoja ya namna hiyo haitatolewa, ndani ya

miezi kumi na miwili tangu ilipotolewa na kukataliwa na Bunge.

Hoja ya kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi

149.-(1) Bunge halitajadili wala kushughulikia hoja ya kumshtaki Rais, isipokuwa tu kama-

(a) taarifa ya maandishi, iliyowekwa saini na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote itatolewa;
(b) taarifa hiyo itawasilishwa kwa Spika, siku thelathini kabla ya kikao ambacho hoja hiyo inakusudiwa kutolewa Bungeni;
(c) taarifa hiyo pia itafafanua makosa aliyoyatenda Rais; na
(d) taarifa hiyo vilevile itapendekeza kuwa, Kamati Maalum ya Uchunguzi iundwe ili ichunguze mashtaka yaliyowasilishwa dhidi ya Rais.

(2) Wakati wowote baada ya kupokea taarifa iliyowekwa saini na Wabunge na kujiridhisha kuwa masharti ya Katiba kwa ajili ya kuwasilisha hoja hiyo Bungeni yametimizwa, Spika atamruhusu mtoa hoja kuiwasilisha hoja hiyo Bungeni.

(3) Hoja hiyo itakapowasilishwa Bungeni, Spika atalitaka Bunge, bila ya kufanya majadiliano yoyote, lipige kura ya siri ili kupata uamuzi juu ya hoja hiyo.

Wajumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi

Sura ya 2

150.-(1) Endapo hoja ya kumshtaki Rais itaungwa mkono na Wabunge wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote, Spika atatangaza majina ya wajumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi, kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 46A (4) ya Katiba.

(2) Kamati Maalum ya Uchunguzi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo;
(b) Jaji Mkuu wa Zanzibar; na
(c) Wajumbe saba walioteuliwa na Spika kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi baina ya Vyama vya Siasa vinavyowakilishwa Bungeni.

(3) Endapo Bunge litapitisha hoja ya kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi, Rais atahesabiwa kuwa hayupo kazini, na kwa sababu hiyo, kazi na madaraka ya Rais yatatekelezwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 37(3) ya Katiba hadi Spika atakapomfahamisha Rais juu ya Azimio la Bunge kuhusiana na mashtaka yaliyotolewa dhidi yake.

Sura ya 2

Utaratibu wa kazi ya Kamati Maalum ya Uchunguzi

151.-(1) Ndani ya siku saba baada ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kuundwa, itakaa ichunguze na kuchambua mashtaka dhidi ya Rais na itampatia Rais fursa ya kujieleza na kujitetea kuhusu mashtaka yaliyotolewa dhidi yake kwa mujibu wa masharti na utaratibu uliowekwa na Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge na Kanuni.

Sura ya 296

(2) Mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote vile katika muda usiozidi siku tisini, Kamati Maalum ya Uchunguzi itatoa taarifa yake kwa Spika.

(3) Akidi ya mkutano wowote wa Kamati Maalum ya Uchunguzi itakuwa ni Mwenyekiti, Jaji Mkuu wa Zanzibar na Wajumbe wengine wanne kutoka Bungeni.

(4) Baada ya Spika kupokea taarifa ya Kamati Maalum ya Uchunguzi, taarifa hiyo itawasilishwa Bungeni kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni.

Utaratibu katika Kamati ya Bunge Zima kuhusu mashtaka dhidi ya Rais

152.-(1) Endapo kwa mujibu wa Orodha ya Shughuli za Bunge utafika wakati wa Bunge kujadili taarifa ya Kamati hiyo Maalum ya Uchunguzi, basi Bunge litaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima ili kushughulikia taarifa hiyo na Bunge linaweza kumruhusu Mwenyekiti na mjumbe mwingine ambaye siyo Mbunge wa Kamati Maalum ya Uchunguzi kuwasilisha na kuelezea uamuzi wa Kamati yake kwenye Kamati ya Bunge Zima.

(2) Baada ya taarifa ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kuwasilishwa Bungeni, Bunge litaijadili taarifa hiyo na litampa Rais fursa ya kujieleza na kujitetea kuhusu mashtaka yaliyotolewa dhidi yake.

Azimio la kumwondoa Rais

153.-(1) Baada ya kusikiliza utetezi wa Rais, Wabunge watapiga kura ya siri ili kupata uamuzi wa Bunge iwapo mashtaka dhidi ya Rais yamethibitika au mashtaka hayo hayakuthibitika.

(2) Baada ya Kamati ya Bunge Zima kukamilisha kazi zake na Bunge kurudia, Mbunge aliyetoa hoja ya kumshtaki Rais atatoa taarifa ya kukamilika kwa shughuli za Kamati ya Bunge Zima na endapo mashtaka dhidi ya Rais yatakuwa yamethibitika, kwa kuungwa mkono na kura za Wabunge wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote, papo hapo atatoa hoja kwamba, Bunge lipitishe Azimio la kumwondoa Rais madarakani, kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 46A (5) ya Katiba.

Sura ya 2

(3) Endapo Bunge litapitisha Azimio la kumwondoa Rais madarakani, Spika atawafahamisha Rais na Mwenyekiti wa Tume ya

Uchunguzi juu ya Azimio hilo la Bunge na Rais atawajibika kujiuzulu katika kipindi cha siku tatu tangu Bunge lilipopitisha Azimio hilo.

(4) Endapo Rais ataacha kushika kiti cha Rais kutokana na mashtaka dhidi yake kuthibitika na Bunge kupitisha Azimio la kumwondoa madarakani, Rais hatakuwa na haki ya kupata malipo yoyote ya pensheni.

## SEHEMU YA KUMI NA SABA
## UTARATIBU WA KUMWONDOA MAKAMU WA RAIS MADARAKANI

Utaratibu wa kumwondoa Makamu wa Rais madarakani

Sura ya 2

154.-(1) Rais anaweza kuwasilisha Bungeni hati ya kuliomba Bunge lipitishe Azimio la kumwondoa Makamu wa Rais madarakani ikiwa Makamu wa Rais ameacha au ameshindwa kutekeleza kazi za Makamu wa Rais kwa mujibu wa ibara ya 50(3) ya Katiba.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, Mbunge yeyote anaweza kuwasilisha Bungeni hoja ya kutaka kumwondoa Makamu wa Rais madarakani ikiwa Makamu wa Rais-

(a) ametenda vitendo ambavyo kwa ujumla vinavunja Katiba au Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma; (Sura ya 398)

(b) ametenda vitendo vinavyokiuka maadili yanayohusu uandikishaji wa vyama vya siasa vilivyotajwa katika ibara ya 20 (2) ya Katiba; au (Sura ya 2)

(c) amekuwa na mwenendo unaodhalilisha Kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano au Kiti cha Makamu wa Rais,

isipokuwa kwamba, hoja ya namna hiyo haitatolewa ndani ya miezi kumi na miwili tangu hoja ya namna hiyo ilipotolewa na kukataliwa na Bunge.

Hoja ya kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi

155.-(1) Bunge halitajadili wala kushughulikia hoja ya kumshtaki Makamu wa Rais isipokuwa tu kama-

(a) taarifa ya maandishi, iliyowekwa saini na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote imetolewa;

(b) taarifa hiyo itawasilishwa kwa Spika, siku thelathini kabla ya kikao ambapo hoja hiyo inakusudiwa kutolewa Bungeni;

(c) taarifa hiyo itafafanua makosa aliyoyatenda Makamu wa Rais; na

(d) taarifa hiyo itapendekeza kuwa, Kamati Maalum ya Uchunguzi iundwe ili ichunguze mashtaka yaliyowasilishwa dhidi ya Makamu wa Rais.

(2) Wakati wowote baada ya kupokea taarifa iliyowekwa saini na Wabunge na kujiridhisha kuwa masharti ya Katiba kwa ajili ya kuwasilisha hoja hiyo Bungeni yametimizwa, Spika atamruhusu mtoa hoja kuiwasilisha hoja hiyo Bungeni.

(3) Hoja hiyo itakapowasilishwa Bungeni, Spika atalitaka Bunge, bila ya kufanya majadiliano yoyote, lipige kura ya siri ili kupata uamuzi juu ya hoja hiyo.

Wajumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi

Sura ya 2

156.-(1) Endapo hoja ya kumshtaki Makamu wa Rais itaungwa mkono na Wabunge wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote, Spika atatangaza majina ya wajumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi, kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 46A (4) ya Katiba.

(2) Kamati Maalum ya Uchunguzi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo;
(b) Jaji Mkuu wa Zanzibar; na
(c) Wajumbe saba walioteuliwa na Spika kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi baina ya vyama vya siasa vinavyowakilishwa Bungeni.

(3) Endapo Bunge litapitisha hoja ya kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi, Makamu wa Rais atahesabiwa kuwa hayupo kazini, na kwa sababu hiyo, kazi na madaraka ya Makamu wa Rais yatatekelezwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 37(3) ya Katiba hadi Spika atakapomfahamisha Makamu wa Rais juu ya Azimio la Bunge kuhusu mashtaka yaliyotolewa dhidi yake.

Sura ya 2

Utaratibu wa kazi ya Kamati Maalum ya Uchunguzi

Sura ya 296

157.-(1) Ndani ya siku saba baada ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kuundwa, itakaa ichunguze na kuchambua mashtaka dhidi ya Makamu wa Rais na itampatia Makamu wa Rais fursa ya kujieleza na kujitetea kuhusu mashtaka yaliyotolewa dhidi yake kwa mujibu wa masharti na utaratibu uliowekwa na Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge na Kanuni.

(2) Mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote vile katika muda usiozidi siku tisini, Kamati Maalum ya Uchunguzi itatoa taarifa yake kwa Spika.

(3) Akidi ya mkutano wowote wa Kamati Maalum ya Uchunguzi itakuwa ni Mwenyekiti, Jaji Mkuu wa Zanzibar na Wajumbe wengine wanne kutoka Bungeni.

(4) Baada ya Spika kupokea taarifa ya Kamati Maalum ya

Uchunguzi, taarifa hiyo itawasilishwa Bungeni kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni.

Utaratibu katika Kamati ya Bunge Zima kuhusu mashtaka dhidi ya Makamu wa Rais

158.-(1) Endapo kwa mujibu wa Orodha ya Shughuli za Bunge utafika wakati wa Bunge kujadili taarifa ya Kamati hiyo Maalum ya Uchunguzi, Bunge litaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima ili kushughulikia taarifa hiyo na Bunge linaweza kumruhusu Mwenyekiti na mjumbe mwingine ambaye siyo Mbunge wa Kamati Maalum ya Uchunguzi kuwasilisha na kuelezea uamuzi wa Kamati yake kwenye Kamati ya Bunge Zima.

(2) Baada ya taarifa ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kuwasilishwa Bungeni, Bunge litaijadili taarifa hiyo na litampa Makamu wa Rais fursa ya kujieleza na kujitetea kuhusu mashtaka yaliyotolewa dhidi yake.

Azimio la kumwondoa Makamu wa Rais madarakani

159.-(1) Baada ya kusikiliza utetezi wa Makamu wa Rais, Wabunge watapiga kura ya siri ili kupata uamuzi wa Bunge iwapo mashtaka dhidi ya Makamu wa Rais yamethibitika au mashtaka hayo hayakuthibitika.

(2) Baada ya Kamati ya Bunge Zima kukamilisha kazi zake na Bunge kurudia, Mbunge aliyetoa hoja ya kumshtaki Makamu wa Rais atatoa taarifa ya kukamilika kwa shughuli za Kamati ya Bunge Zima na endapo mashtaka dhidi ya Makamu wa Rais yatakuwa yamethibitika, kwa kuungwa mkono na kura za Wabunge wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote, papo hapo atatoa hoja kwamba, Bunge lipitishe Azimio la kumwondoa Makamu wa Rais madarakani, kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 46A(5) ya Katiba.

Sura ya 2

(3) Endapo Bunge litapitisha Azimio la kumwondoa Makamu wa Rais madarakani, Spika atawafahamisha Rais, Makamu wa Rais na Mwenyekiti wa Tume ya Uchunguzi juu ya Azimio hilo la Bunge na Makamu wa Rais atawajibika kujiuzulu katika kipindi cha siku tatu tangu Bunge lilipopitisha Azimio hilo.

(4) Endapo Makamu wa Rais ataacha kushika kiti cha Makamu wa Rais kutokana na mashtaka dhidi yake kuthibitika na Bunge kupitisha Azimio la kumwondoa madarakani, Makamu wa Rais, hatakuwa na haki ya kupata malipo yoyote ya pensheni.

## SEHEMU YA KUMI NA NANE
## HOJA YA KUTOKUWA NA IMANI NA WAZIRI MKUU

Taarifa ya Hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu
Sura ya 2

160.-(1) Mbunge yeyote anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa Spika ya kutaka kuleta hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu kwa mujibu wa ibara ya 53A ya Katiba.

(2) Hoja yoyote ya kutaka kupitisha Azimio la kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu haitatolewa Bungeni endapo-

Sura ya 2

(a) haina uhusiano na utekelezaji wa majukumu ya Waziri Mkuu yaliyoainishwa katika ibara ya 52 ya Katiba;
(b) hakuna madai kwamba Waziri Mkuu amevunja Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
(c) haijapita miezi sita tangu alipoteuliwa; na
(d) haijapita miezi tisa tangu hoja ya namna hiyo ilipotolewa Bungeni na Bunge likakataa kuipitisha.

(3) Hoja ya kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu haitajadiliwa na Bunge isipokuwa tu kama-

(a) taarifa ya maandishi iliyowekwa saini na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote itatolewa kwa Spika, siku zisizopungua kumi na nne kabla ya siku inayokusudiwa kuwasilishwa Bungeni; na
(b) Spika ataridhika kuwa masharti ya Katiba kwa ajili ya kuleta hoja hiyo yametimizwa.

(4) Hoja inayotolewa chini ya kanuni hii na iliyotimiza masharti ya Katiba, itawasilishwa Bungeni mapema iwezekanavyo na itaamuliwa kwa kura za siri.

(5) Hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu itapitishwa tu iwapo inaungwa mkono na Wabunge walio wengi.

(6) Endapo hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu itapitishwa na Bunge kwa kupigiwa kura na Wabunge walio wengi, Spika atawasilisha Azimio hilo kwa Rais na mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote vile ndani ya siku mbili tangu Bunge lilipopitisha Azimio hilo, Waziri Mkuu atajiuzulu na Rais atamteua Mbunge mwingine kuwa Waziri Mkuu.

## SEHEMU YA KUMI NA TISA
## KUMWONDOA SPIKA AU NAIBU SPIKA MADARAKANI

Taarifa ya hoja ya kumwondoa Spika madarakani
Sura ya 2

161.-(1) Mbunge yeyote anayetaka kuwasilisha hoja ya kumwondoa Spika madarakani chini ya ibara ya 84(7)(d) ya Katiba, atawasilisha taarifa ya maandishi ya kusudio hilo kwa Katibu akieleza

sababu za kutaka kuleta hoja hiyo.

(2) Mara tu baada ya kupokea taarifa ya maandishi ya kusudio la kumwondoa Spika kwenye madaraka, Katibu ataipeleka taarifa hiyo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa ajili ya kuijadili.

(3) Endapo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itaridhika kuwa zipo tuhuma mahsusi dhidi ya Spika zinazohusu uvunjaji wa masharti ya ibara ya 84(7)(a), (b), (e), (f), (g) na (h) ya Katiba, Sheria au Kanuni zinazoongoza shughuli za Bunge, basi Kamati hiyo itaidhinisha kuwa hoja hiyo ipelekwe Bungeni ili iamuliwe.

Sura ya 2

(4) Naibu Spika, atakalia Kiti cha Spika wakati wa kujadili hoja ya kutaka kumwondoa Spika madarakani na Spika atakuwa na haki ya kujitetea wakati wa mjadala.

(5) Spika atakuwa ameondolewa kwenye madaraka endapo zitapigwa kura zisizopungua theluthi mbili ya idadi ya Wabunge wote za kuunga mkono hoja hiyo na uamuzi wa Bunge utafanywa kwa kuzingatia kura za siri.

(6) Spika anayetuhumiwa anaweza kujiuzulu nafasi yake kwa kutoa maelezo ya kujiuzulu kwake Bungeni kabla ya uamuzi juu ya hoja ya kumwondoa madarakani.

Utaratibu wa kumwondoa Naibu Spika madrakani
Sura ya 2

162.-(1) Utaratibu wa kumwondoa Naibu Spika madarakani chini ya ibara ya 85(4)(c) ya Katiba utakuwa kama ule wa kumwondoa Spika, isipokuwa tu taarifa ya kusudio la kumwondoa Naibu Spika madarakani inayoeleza sababu kamili za kuleta hoja hiyo, itapelekwa kwa Spika ambaye ataiwasilisha kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa ajili ya kuijadili.

(2) Endapo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itaridhika kuwa zipo tuhuma mahsusi dhidi ya Naibu Spika zinazohusu uvunjaji wa Katiba, Sheria au Kanuni zinazoongoza Shughuli za Bunge, basi Kamati hiyo itaidhinisha kuwa hoja hiyo ipelekwe Bungeni ili iamuliwe.

(3) Spika atakalia Kiti wakati wa kujadili hoja ya kutaka kumwondoa Naibu Spika madarakani na Naibu Spika atakuwa na haki ya kujitetea wakati wa mjadala.

(4) Naibu Spika atakuwa ameondolewa kwenye madaraka endapo zitapigwa kura zisizopungua theluthi mbili ya idadi ya Wabunge wote za kuunga mkono hoja hiyo na uamuzi wa Bunge utafanywa kwa kuzingatia kura za siri.

(5) Naibu Spika anayetuhumiwa anaweza kujiuzulu nafasi

yake kwa kutoa maelezo ya kujiuzulu kwake Bungeni kabla ya uamuzi juu ya hoja ya kumwondoa madarakani.

## SEHEMU YA ISHIRINI
## MPANGILIO WA UKAAJI NA UTARATIBU KUHUSU WAGENI BUNGENI

Mpangilio wa ukaaji Bungeni

163. Spika ataweka utaratibu maalum wa ukaaji wa Wabunge ndani ya Bunge bila kuathiri mpangilio ufuatao:

(a) Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni atakaa kiti cha kwanza akifuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawaziri upande wa kulia wa Spika;
(b) Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni atakaa kiti cha kwanza akifuatiwa na Wasemaji Wakuu wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache upande wa kushoto wa Spika;
(c) endapo hakuna Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache aliyechaguliwa na chama chenye haki ya kuchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni lakini Wabunge wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache wapo, Wabunge hao watakaa upande wa kushoto wa Spika;
(d) Mpambe wa Bunge, watumishi wa Bunge na watumishi wa Serikali wenye shughuli maalum katika Ukumbi wa Bunge, waandishi wa vyombo vya habari na wageni wengine watakaa sehemu ambazo zimetengwa kwa ajili yao;
(e) wageni mashuhuri, Mabalozi na Viongozi wengine watakaa sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili ya wageni wa Spika; na
(f) wageni wa Wabunge na wageni wengine wanaweza kutengewa sehemu maalum ya kukaa.

Ruhusa kwa wageni kuingia Bungeni

164.-(1) Wageni wanaweza kuruhusiwa kuingia kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge katika sehemu yoyote ya Ukumbi huo ambayo itatengwa kwa ajili hiyo.

(2) Wageni wakiwa ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge watalazimika kufuata na kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) watakaa kimya na kwa heshima inayostahili hadi watakapotoka nje ya Ukumbi huo;
(b) wanapaswa wawe wamevaa mavazi ya heshima;

(c) wataingia na kutoka Ukumbini kwa staha;
(d) wasisome kitabu chochote, gazeti, barua au hati nyingineyo ambayo si Orodha ya Shughuli za Bunge;
(e) wasiandike wala kurekodi jambo lolote linalozungumzwa, isipokuwa tu kama ni wawakilishi wa vyombo vya habari;
(f) inapolazimu kuzungumza, wasizungumze kwa sauti ya juu;
(g) wasivute sigara au kiko wakati wowote na mahali pengine ambapo panatumiwa na watu wengine;
(h) wazime simu au vifaa vingine vyovyote vya mawasiliano walivyonavyo;
(i) wasipige picha wala kuingia na kamera au kifaa kingine chenye uwezo wa kupiga picha au kunasa sauti;
(j) wasishangilie wala kuzomea; na
(k) wasifanye jambo au kitendo chochote kinachoweza kuvuruga amani na utulivu Bungeni.

(3) Spika anaweza kumwamuru mgeni yeyote aondoke kwenye Ukumbi wa Bunge endapo atavunja lolote kati ya masharti yaliyotajwa katika kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii.

Utambulisho wa wageni

165.-(1) Spika anaweza kuwatambulisha wageni mahsusi wa kitaifa na kimataifa waliomo katika Ukumbi wa Bunge.

(2) Spika anaweza kumtambulisha mgeni mwingine ambaye ametoa mchango wa kitaifa unaohitaji kuenziwa.

Mamlaka ya kuwaondoa wageni Bungeni

166.-(1) Spika anaweza kuamuru wageni watoke sehemu yoyote ya Ukumbi na maeneo yake na anaweza kuamuru milango ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge ifungwe.

(2) Endapo wakati wa kikao chochote Mbunge atatoa hoja kuwa wageni watoke nje, Spika atalihoji Bunge papo hapo na hoja itaamuliwa bila ya mjadala au mabadiliko yoyote, wakati wowote atakapoona inafaa kufanya hivyo.

(3) Mtumishi yeyote wa Bunge hataruhusiwa kumtoa mgeni au kuagiza mgeni atolewe katika Ukumbi wa Bunge endapo Katibu amemruhusu mgeni huyo kuwa ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Ruhusa kwa waandishi wa habari

167.-(1) Katibu anaweza kutoa ruhusa maalum au ya jumla kwa mwakilishi wa chombo chochote cha habari kuhudhuria vikao vya Bunge katika sehemu ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge iliyotengwa kwa ajili hiyo.

(2) Ruhusa yoyote itakayotolewa na Katibu inaweza

kuwekewa masharti yafuatayo:

(a) chombo husika kitoe maombi rasmi; na

(b) chombo husika kiteue waandishi wenye sifa na maadili ya kuweza kuandika habari za Bunge.

(3) Katibu anaweza wakati wowote kuondoa ruhusa aliyotoa kwa mwakilishi wa chombo chochote cha habari, iwapo chombo hicho kitatoa taarifa yoyote kuhusu Shughuli za Bunge ambayo inapotosha ukweli au vinginevyo inakiuka Kanuni, taratibu au haki za Bunge.

(4) Masharti kuhusu utaratibu wa ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge na shughuli zake umeainishwa katika Nyongeza ya Saba ya Kanuni.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA
## USALAMA WA MAENEO YA BUNGE

Utaratibu wa kuingia maeneo ya Bunge

168.-(1) Spika ataweka utaratibu wa kutoa vitambulisho kwa Wabunge, watumishi wa Bunge, watumishi wa Serikali na kwa mtu mwingine yeyote anayeingia kwenye Ukumbi wa Bunge au maeneo mengine ya Bunge.

(2) Katibu atatoa vitambulisho vya aina tofauti kwa ajili ya Wabunge, watumishi wa Bunge, watumishi wa Serikali, waandishi wa habari na wageni wanaokaribishwa katika Ukumbi wa Bunge au maeneo mengine ya Bunge.

Ukaguzi

169.-(1) Kutakuwa na utaratibu wa kumkagua mtu yeyote anayeingia katika maeneo ya Bunge kwa kuzingatia-

(a) staha na heshima; na

(b) tofauti ya jinsi.

(2) Endapo katika kufanya ukaguzi mtu yeyote atapatikana na kifaa ambacho kwa asili yake ni cha hatari, kifaa hicho atakiacha kwa walinzi waliopo mlangoni.

(3) Mbunge, mtumishi au mgeni yeyote atakayekataa kukaguliwa au kukabidhi kitu chochote ambacho walinzi wataona kwamba ni cha hatari, hataruhusiwa kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge au maeneo ya Bunge.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI
## MASHARTI MENGINEYO

Wajibu wa Mbunge kuhudhuria vikao vya Mikutano ya Bunge

Sura ya 2

170.-(1) Kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake ni wajibu wa kwanza wa kila Mbunge.

(2) Mbunge yeyote atakayeshindwa kuhudhuria Mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ruhusa ya Spika iliyotolewa kwa maandishi, atapoteza Ubunge wake kwa mujibu wa ibara ya 71(1) (c) ya Katiba na Spika ataiarifu Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

(3) Mbunge atakapokosa kuhudhuria nusu ya vikao vya Mkutano mmoja bila ya sababu ya msingi atapewa onyo.

(4) Mbunge yeyote atakayeshindwa kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake kwa sababu maalum atatakiwa kupata kibali cha Spika.

(5) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (4) ya kanuni hii, kibali kitatolewa katika Ofisi za Bunge za Dodoma au Dar es Salaam au Zanzibar.

Lugha rasmi Bungeni

171.-(1) Shughuli za Bunge zitaendeshwa katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza, bila tafsiri ya lugha hizo kutolewa.

(2) Kwa kadri itakavyowezekana, Mbunge atajitahidi kutochanganya lugha zote mbili wakati anasema Bungeni, isipokuwa tu pale anaponukuu.

Taarifa Rasmi za Bunge

172.-(1) Taarifa Rasmi za Majadiliano Bungeni, ikiwa katika lugha iliyotumiwa na msemaji, yakiwa ni maneno halisi aliyoyatamka, itatayarishwa chini ya usimamizi wa Katibu wa Bunge kwa kufuata maagizo yatakayotolewa na Spika kwa ajili hiyo.

(2) Mbunge aliyechangia Bungeni kwa kuzungumza atapewa nakala ya mchango wake mapema iwezekanavyo, ili aweze kusahihisha makosa ya uchapaji, kama yatakuwepo ila hataruhusiwa kubadilisha maana ya maneno aliyoyasema Bungeni.

(3) Mbunge atakayefanya masahihisho kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) atarejesha masahihisho hayo kwa Katibu ndani ya saa ishirini na nne tangu alipopatiwa nakala, na ikiwa hatarejesha ndani ya muda huo itachukuliwa kuwa nakala hiyo haina masahihisho.

Mavazi Rasmi

173.-(1) Mbunge anayeingia kwenye Ukumbi wa Bunge au ukumbi mwingine wowote ambao kikao cha Kamati kinafanyika au maeneo mengine yoyote ambapo shughuli za Bunge zinafanyika, atawajibika kuvaa mavazi nadhifu na yenye kuhifadhi heshima yake,

hadhi ya Bunge na utamaduni wa nchi, kama ilivyoainishwa katika kanuni hii.

(2) Vazi Rasmi kwa Spika na Naibu Spika wa Bunge litakuwa ni joho lenye kuonesha rangi za Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa na baadhi ya mazao makuu nchini, lililoshonwa maalum kwa ajili hiyo, ambalo litavaliwa juu ya vazi lolote ambalo ni vazi rasmi kwa Wabunge.

(3) Vazi rasmi kwa Wenyeviti wa Bunge litakuwa ni joho maalum lenye fito za rangi ya bendera ya Taifa ambalo litavaliwa juu ya vazi lolote rasmi.

(4) Vazi rasmi kwa Wabunge litakuwa lolote kati ya yafuatayo:

(a) Kwa Mbunge mwanamke-
- (i) vazi lolote la heshima yaani ambalo si la kubana mwili, lisiloangaza mwili, lisiloonesha maungo ambayo kwa mila na desturi za kitanzania hayapaswi kuoneshwa na ni refu kuvuka magoti;
- (ii) gauni la kitenge au blauzi inayovaliwa na kitenge au sketi ya rangi yoyote;
- (iii) kilemba cha kadri au mtandio;
- (iv) suti ya kike;
- (v) vazi rasmi la asili la kabila linalotambulika ambalo limevaliwa kwa unadhifu; au
- (vi) vazi linalovaliwa wakati wa eda.

(b) Kwa Mbunge mwanaume-
- (i) suti ya kiafrika au suti ya safari ya mikono mirefu au mifupi yenye ukosi au shingo ya mviringo na yenye fulana au bila fulana ndani, ya rangi moja, isiyokuwa na nakshi pamoja na au bila baraghashia;
- (ii) vazi la kimwambao yaani kanzu rasmi na nadhifu, koti, baraghashia na makubadhi au viatu;
- (iii) suti kamili ya kimagharibi ya rangi ya kadri isiyomeremeta;
- (iv) koti lisilo sehemu ya suti na tai, pamoja na suruali yoyote ya heshima;
- (v) vazi rasmi la asili la kabila linalotambulika ambalo limevaliwa kwa unadhifu; au
- (vi) tarbushi na kilemba cha Singasinga, au kilemba chochote kinachovaliwa kwa mujibu wa masharti ya imani au mila:

Isipokuwa kwamba mavazi ya Mbunge mwanaume yatavaliwa bila kuonesha nguo za ndani na hayatakuwa ya kubana mwili, yanayoangaza mwili au kuonesha maungo ambayo kwa mila na desturi za kitanzania hayapaswi kuoneshwa.

(5) Mbunge hataruhusiwa kuingia katika ukumbi wa Bunge, eneo au ukumbi mwingine ambako kikao cha Kamati kinafanyika akiwa amevaa sare au mavazi yaliyozoeleka au kuashiria moja kwa moja au kwa namna yoyote ile ufuasi au ushabiki wa chama chochote cha siasa kwa alama, nembo, jina la chama au maandishi yanayotumiwa au kutafsiriwa kuwa jina, alama, msemo, mavazi au nembo ya chama.

(6) Vazi Rasmi la Katibu na wasaidizi wake Bungeni litakuwa kama ifuatavyo:

(a) kwa Katibu Mezani mwanaume atavaa suti kamili ya kimagharibi ya rangi nyeusi au bluu na shati jeupe na tai na joho maalum kwa Katibu Mezani;

(b) kwa Katibu Mezani mwanamke-

(i) suti ya rangi nyeusi au ya bluu;

(ii) shati jeupe;

(iii) tai;

(iv) joho maalum kwa Katibu Mezani; na

(v) kilemba cha kadri au mtandio kwa mujibu wa masharti ya imani; na

(c) Makatibu na Wahudumu wa Bunge watavaa mavazi maalum wakati wa shughuli maalum za Bunge.

(7) Mpambe wa Bunge na wasaidizi wake ndani ya Ukumbi wa Bunge watavaa mavazi rasmi ambayo yataamuliwa na Spika.

(8) Spika anaweza kwa sababu maalum, kumruhusu mtu yeyote anayehusika na Shughuli za Bunge kuvaa vazi lisilo rasmi.

Kutoingia Bungeni bila Mavazi Rasmi

174.-(1) Spika anaweza kutoa maelekezo ya kumzuia Mbunge, Mtumishi wa Bunge, Mtumishi wa Serikali au mtu yeyote ambaye hajavaa mavazi rasmi kuingia katika maeneo ya Bunge, ukumbi wa Bunge au ukumbi mwingine ambao kikao cha Bunge au Kamati kinafanyika au eneo ambalo shughuli za Bunge zinafanyika.

(2) Mbunge anaweza kutoa taarifa Bungeni iwapo Mbunge mwingine ataingia katika Ukumbi wa Bunge akiwa amevaa mavazi yasiyoruhusiwa na ikiwa Spika atajiridhisha kuwa Mbunge aliyetajwa hajavaa mavazi rasmi, ataamuru Mbunge huyo atoke katika Ukumbi wa Bunge.

(3) Mbunge anaweza kutoa taarifa katika kikao cha Kamati iwapo Mbunge mwingine ataingia katika ukumbi au eneo ambalo kikao cha Kamati kinafanyika akiwa amevaa mavazi yasiyoruhusiwa na ikiwa Mwenyekiti wa Kamati atajiridhisha kuwa Mbunge aliyetajwa hajavaa mavazi rasmi, ataamuru Mbunge huyo atoke katika kikao.

(4) Mbunge ambaye hakurejea katika kikao cha Bunge au Kamati akiwa amevaa mavazi rasmi baada ya kutolewa, hatahesabiwa kuwa alihudhuria kikao cha siku husika.

Utaratibu wa kupeperusha Bendera

175.-(1) Bendera ya Bunge itapeperushwa-

(a) katika Ofisi za Bunge Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar;
(b) nje ya Ofisi ya Mbunge iliyopo Makao Makuu ya Mkoa, Wilaya na katika Jimbo la Uchaguzi;
(c) ndani ya Ofisi ya Mbunge juu ya meza anayofanyia kazi; na
(d) katika gari binafsi la Mbunge ambapo Bendera hiyo itapeperushwa ikiwa mbele upande wa kushoto nje ya gari la Mbunge likiwa linaendeshwa na dereva wakati Mbunge akiwa ndani ya gari hilo.

(2) Mbunge hatapeperusha bendera ya Bunge katika gari-

(a) anapokuwa katika Mji wa Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar;
(b) anapokuwa anatumia gari la kukodi au la kuazima;
(c) akiwa anaendesha gari; na
(d) anapokuwa anapeperusha bendera ya aina nyingine.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya kanuni hii, bendera ya Bunge itapeperushwa kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi na itashushwa mara ifikapo saa kumi na mbili kamili jioni kila siku.

(4) Bendera ya Bunge itaendelea kupeperushwa katika gari la Mbunge baada ya saa 12:00 Jioni endapo anayepeperusha bendera hiyo atakuwa safarini hadi pale atakapomaliza safari yake.

Kuahirisha Shughuli za Bunge Mbunge anapofariki

176. Endapo Mbunge atafariki wakati Bunge likiwa katika shughuli zake, Spika ataahirisha shughuli za Bunge kwa siku hiyo kwa ajili ya maombolezo.

Kutengua Kanuni

177.-(1) Kwa idhini ya Spika, kanuni yoyote inaweza kutenguliwa kwa madhumuni mahsusi baada ya Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo.

(2) Hoja ya kutengua kanuni haitahitaji kutolewa taarifa.

(3) Maelezo ya hoja ya kutaka kutengua kanuni yoyote itakuwa ni pamoja na maelezo kuhusu madhumuni ya kutaka kanuni hiyo itenguliwe.

(4) Kanuni itatenguliwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa na si vinginevyo.

Salamu za pongezi na pole

178.-(1) Endapo litatokea jambo lolote ambalo mhusika wake au mwathirika wa jambo hilo anastahili kupewa pongezi au pole na Wabunge basi Spika atatoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo kwa niaba ya Wabunge wote.

(2) Baada ya Spika kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote, kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni.

(3) Kwa upande wa Serikali, Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni au Waziri yeyote kwa niaba yake atatoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa niaba ya Serikali.

(4) Baada ya Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni au Waziri kwa niaba yake kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote, kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Waziri hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni.

Mabadiliko katika Kanuni

179.-(1) Bunge linaweza kupitisha Azimio la kufanya mabadiliko katika kanuni yoyote ya Bunge baada ya kupokea mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge.

(2) Mabadiliko yoyote ya Kanuni za Bunge yatawasilishwa Bungeni na Naibu Spika.

(3) Spika, kwa kushauriana na Kamati ya Kanuni za Bunge, atakuwa na madaraka ya kuzifanyia marekebisho au mabadiliko Nyongeza za Kanuni, kulingana na mahitaji ya wakati, kadri atakavyoona inafaa.

Kanuni kuanza kutumika

180.-(1) Mabadiliko yaliyopitishwa hayataanza kutumika mpaka yatakapochapishwa upya katika Gazeti.

(2) Endapo mabadiliko ya Kanuni yatafanyika kupitia Azimio la Bunge, nakala ya Kanuni za Bunge itachapishwa upya.

(3) Endapo yatafanyika mabadiliko ya Kanuni kwa mujibu wa Kanuni ya 179(3), Spika anaweza kuelekeza kuchapishwa nakala ya toleo la Kanuni.

(4) Nakala za Kanuni zilizochapishwa kwa kufuata utaratibu uliofafanuliwa katika kanuni hii zitahesabiwa kuwa nakala halisi za Kanuni za Kudumu za Bunge zilizofanyiwa mabadiliko.

Kufutwa kwa Kanuni za Bunge TS. Na. 626 la 2020

181.-(1) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 zinafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii jambo, amri, uteuzi, agizo au jambo lingine lililofanyika kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 halitakuwa batili na litaendelea kuwa halali hadi litakapobatilishwa, kufutwa au kuagizwa vinginevyo kwa mujibu wa Kanuni.

## NYONGEZA

## NYONGEZA YA KWANZA

### KANUNI ZA UCHAGUZI WA SPIKA NA NAIBU SPIKA

*[Chini ya Kanuni ya 9(1) na 11(4)]*

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Uchaguzi wa Spika na Naibu Spika.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika katika mchakato wa Uchaguzi wa Spika na Naibu Spika.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa pale maelezo yatakapohitaji vinginevyo:-

"chombo cha Uteuzi" ni Chama kinachopendekeza mgombea au wagombea wake;

Sura ya 2

"Katibu" ni Katibu wa Bunge aliyetajwa katika ibara ya 87 ya Katiba na inajumuisha pia mtumishi yeyote wa Bunge aliyeidhinishwa kutekeleza kazi ya Katibu;

"mgombea" ni mtu aliyejitokeza au aliyependekezwa na chama cha siasa kuwa mgombea wa uchaguzi;

"msimamizi wa uchaguzi" ni mtu ambaye kwa mujibu wa Kanuni hizi amepewa mamlaka ya kuendesha na kusimamia Uchaguzi;

"nafasi" ni nafasi wazi ya Spika, iliyotokea ama kutokana na kuvunjwa kwa Bunge au kutokana na nafasi itokeayo kwa nasibu;

Sura ya 2

"Naibu Spika" ni Naibu Spika wa Bunge aliyetajwa katika ibara ya 85 ya Katiba;

"siku ya uteuzi" ni siku ambayo imetangazwa na msimamizi wa uchaguzi kuwa siku ya mwisho ya kupokea majina ya wagombea;

Sura ya 2

"Spika" ni Spika wa Bunge aliyetajwa katika ibara ya 84 ya Katiba; na

"uchaguzi" ni uchaguzi wa Spika au Naibu Spika.

## SEHEMU YA PILI
## MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

Msimamizi wa Uchaguzi

4. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo, uchaguzi wa Spika na Naibu Spika utaendeshwa na kusimamiwa na Katibu wa Bunge, kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Kanuni pamoja na kanuni hizi.

## SEHEMU YA TATU
## KUWASILISHA JINA LA MGOMBEA

Kuwasilisha majina ya wagombea

5.-(1) Inapofika wakati wa uchaguzi wa Spika au Naibu Spika, chama chochote cha siasa chenye kusudio la kushiriki kwenye uchaguzi huo kitawasilisha kwa Katibu wa Bunge jina moja la Mbunge wa chama hicho au mtu mwingine wa chama hicho mwenye sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge ili awe mgombea wake.

(2) Mgombea mhusika au ofisa wa ngazi ya kitaifa wa chama kilichompendekeza, atawasilisha jina la mgombea huyo kwa Katibu ambaye ndiye msimamizi wa uchaguzi.

(3) Jina la mgombea huyo linatakiwa limfikie Katibu ofisini kwake Dodoma, kabla ya saa kumi jioni ya siku ya uteuzi.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA MGOMBEA UCHAGUZI

Masharti kwa mgombea

Sheria Na. 1 ya 2024

6.-(1) Mtu yeyote anaweza kuteuliwa kugombea kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika iwapo tu atakuwa ametimiza masharti yote ya kuwa mgombea wa nafasi hizo, kama yalivyotajwa katika Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

(2) Mgombea yeyote anaweza kumtaarifu Katibu kwa maandishi kwamba anajitoa kugombea, kabla ya shughuli za kupiga kura kuanza Bungeni, na Katibu atalifuta jina la mgombea huyo katika karatasi za kura.

(3) Endapo itatokea mgombea amejitoa wakati karatasi za uchaguzi zikiwa zimekwishaandaliwa, Katibu atalitaarifu Bunge kuhusu kujiondoa huko na Wabunge watapiga kura kwa wagombea waliobaki:

Isipokuwa kwamba, ikitokea kura imepigwa kwa mgombea aliyejitoa kwa mujibu wa fasili ndogo hii, kura hiyo itahesabika kuwa imeharibika.

## SEHEMU YA TANO
## UTARATIBU WA KUPIGA KURA

Kumpigia kura mgombea mmoja

7. Endapo hadi kufikia saa kumi jioni ya siku ya uteuzi kutakuwa na jina moja tu lililowasilishwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi, mgombea huyo atapigiwa kura ya *"Ndiyo"* au *"Hapana",* na iwapo atapata kura nyingi za *"Ndiyo"* atatangazwa na msimamizi wa uchaguzi kuwa amechaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika.

Utaratibu wa kupiga kura

8. Endapo wamependekezwa wagombea wawili au zaidi, uchaguzi utafanyika kwa kufuata utaratibu ufuatao:

(a) kabla ya kikao cha Bunge cha kumchagua Spika au Naibu Spika kuanza, Katibu ataandaa karatasi za kura zitakazoonesha majina ya wagombea wote waliopendekezwa na wakati wa kupiga kura atatoa karatasi moja tu ya kura kwa kila Mbunge;

(b) kila Mbunge atapiga kura ya siri kwa kuweka katika karatasi ya kura alama ya "V" katika mraba pembeni mwa jina la mgombea anayemtaka awe Spika au Naibu Spika, na ataitumbukiza karatasi hiyo katika sanduku la kura;

(c) Mbunge ambaye kabla ya shughuli za uchaguzi kumalizika atakosea katika kuweka alama kwenye karatasi za kura ataruhusiwa kumrudishia Katibu karatasi hiyo, na papo hapo Katibu ataifuta na kuiharibu kisha kumpa Mbunge huyo karatasi nyingine;

(d) baada ya Katibu kuridhika kwamba Wabunge wote waliomo Bungeni wamepiga kura na kutumbukiza karatasi zao za kura kwenye masanduku ya kura, masanduku yote yatakusanywa na kuwekwa mahali panapoonekana na baada ya hapo masanduku hayo ya kura yatapelekwa kwenye chumba maalum na kura hizo zitahesabiwa chini ya usimamizi wa wawakilishi walioteuliwa na wagombea, mmoja kwa kila mgombea; na

(e) endapo zoezi la uchaguzi litaendeshwa kwa mfumo wa elektroniki wa kupiga kura basi kupiga na kuhesabu kura kutakuwa papo kwa papo na matokeo yake yatakuwa halali.

## SEHEMU YA SITA
## MATOKEO YA UCHAGUZI

Matokeo ya uchaguzi

9.-(1) Mgombea atakuwa amechaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika iwapo atapata zaidi ya nusu ya kura za Wabunge wote na iwapo hakutakuwa na mgombea aliyepata zaidi ya nusu ya kura hizo, uchaguzi utarudiwa lakini ni wagombea wawili tu waliopata kura nyingi zaidi ndio watakaopigiwa kura, na katika hatua hiyo, mgombea atakayepata kura nyingi zaidi atatangazwa kuwa mshindi.

(2) Endapo wagombea wawili au zaidi watapata kura sawa katika nafasi ya mwanzo basi wagombea hao tu ndiyo watakaopigiwa kura na mgombea atakayepata kura nyingi zaidi atakuwa ndiye mshindi.

(3) Iwapo wagombea wawili au zaidi watapata kura sawa katika nafasi ya pili na yule wa kwanza hajapata zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa, basi wagombea hao wawili pamoja na yule wa kwanza ndio watakaopigiwa kura na mgombea atakayepata kura nyingi zaidi atakuwa ndiye mshindi.

(4) Endapo awamu ya pili ya upigaji kura itashindwa kumpata mshindi, basi Mwenyekiti au Spika atapiga kura yake ya uamuzi ili mshindi apatikane.

(5) Mara baada ya mshindi kupatikana, Katibu atamtangaza Spika au Naibu Spika aliyechaguliwa na Mwenyekiti au Spika atasitisha mkutano wa uchaguzi na kutaja muda ambao Spika au Naibu Spika ataapishwa.

## NYONGEZA YA PILI

## KANUNI ZA UCHAGUZI WA WAJUMBE WA TUME NA WABUNGE WANAOKWENDA KWENYE VYOMBO VINGINE VYA UWAKILISHI

*(Chini ya Kanuni ya 14 na 15)*

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Uchaguzi wa Wajumbe wa Tume na Wabunge Wanaokwenda katika Vyombo Vingine vya Uwakilishi.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine kuliwakilisha Bunge na pia kwa uchaguzi wa Wabunge wanaogombea kuwa Wajumbe wa Tume.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa pale maelezo yanapohitaji vinginevyo:-

"chama" ni chama cha siasa chenye uwakilishi Bungeni;

"chombo cha uteuzi" ni chama kinachopendekeza mgombea au wagombea wake;

"idadi inayotakiwa" ni idadi ya kura zinazotakiwa kupatikana au idadi ya nafasi zinazotakiwa zijazwe kwenye uchaguzi;

Sura ya 2

"Katibu" ni Katibu wa Bunge aliyetajwa katika ibara ya 87 ya Katiba na inajumuisha pia mtumishi mwingine yeyote wa Bunge aliyeidhinishwa kutekeleza kazi yoyote ya Katibu;

Sura ya 2

"Mbunge" ni mtu aliyechaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa ibara ya 66 ya Katiba kuwa Mjumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano;

"mgombea" ni mtu aliyejitokeza au aliyependekezwa na chama cha siasa kuwa mgombea wa uchaguzi;

"msimamizi wa uchaguzi" ni mtu ambaye kwa mujibu wa Kanuni hizi amepewa mamlaka ya kuendesha na kusimamia Uchaguzi;

"nafasi" ni nafasi wazi ya uwakilishi wa Wabunge kutoka miongoni mwa Wabunge iliyotokana na kuvunjwa kwa Bunge au nafasi itokeayo kwa nasibu;

"nafasi ya nasibu" ni nafasi wazi ya uwakilishi wa Wabunge isiyotokana na kuvunjwa kwa Bunge;

"siku ya uteuzi" ni siku ambayo imetangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwamba ndiyo siku ya mwisho ya kupokea majina ya wagombea;

Sura ya 2

"Spika" ni Spika wa Bunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa ibara ya 84 ya Katiba;

Sura ya 115

"Tume" ni Tume ya Utumishi wa Bunge iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uendeshaji Bunge; na

"uchaguzi" ni uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine kuliwakilisha Bunge au kuwa Wajumbe wa Tume.

## SEHEMU YA PILI
## UTEUZI WA WAGOMBEA

Uteuzi wa wagombea

4. Uteuzi wa wagombea utafuata utaratibu ufuatao:

(a) unapofika wakati wa uchaguzi, kila Mbunge anayetaka kushiriki uchaguzi atawasilisha jina lake kwa Katibu ambaye atakuwa msimamizi wa uchaguzi huo; na

(b) majina ya wagombea wote yatatakiwa kumfikia Katibu ofisini kwake Dodoma, siku moja kabla ya siku ya uteuzi.

## SEHEMU YA TATU
## UTARATIBU WA UCHAGUZI

Uchaguzi wa wagombea wa nafasi za uwakilishi

5.-(1) Uchaguzi wa wagombea wa nafasi za uwakilishi utaendeshwa na kusimamiwa na Katibu kwa utaratibu ufuatao:

(a) wakati wa uchaguzi wa kwanza katika maisha ya Bunge wa nafasi zilizotangazwa, mara tu baada ya wagombea kuwasilisha majina yao, Spika-
   (i) ataagiza majina ya wagombea wote waliojitokeza yasambazwe kwa Wabunge; na
   (ii) atatangaza Bungeni siku na muda ambapo kura zitapigwa.

(b) Katibu atatoa taarifa ya maandishi kuhusu saa ya kupiga kura ambayo itatolewa si chini ya saa ishirini na nne kabla ya muda wa kupiga kura.

(c) endapo itatokea nafasi miongoni mwa Wabunge waliochaguliwa kwa kufuata kanuni hizi kutokana na sababu isiyohusiana na kuvunjwa kwa Bunge au kama nafasi ya namna hiyo haikujazwa, Spika atatoa taarifa ya kutokea kwa nafasi hiyo kwa Wabunge wote Bungeni.

(2) Utaratibu wa kujaza nafasi ambazo zimetengwa maalum kwa ajili ya kundi la Wabunge wanawake au kundi la Wabunge wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni, utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Katibu atatangaza siku ya uteuzi ambayo itakuwa si zaidi ya siku tano baada ya tangazo la Spika kutolewa Bungeni kwa mujibu wa fasili ndogo ya (1) (c) ya fasili hii;

(b) Mbunge yeyote wa kundi linalohusika anayetaka kuwa mgombea wa nafasi hiyo atawasilisha jina lake kwa Katibu, angalau siku moja kabla ya siku ya uteuzi iliyowekwa; na

(c) endapo atajitokeza mgombea mmoja wa nafasi inayohusika, Wabunge watampigia kura za *"Ndiyo"* au *"Hapana."*

(3) Baada ya kupata majina ya wagombea wote, Katibu atatoa matangazo kuhusiana na idadi ya wagombea, siku na muda wa uchaguzi.

(4) Endapo kunatokea nafasi mbili au zaidi za nasibu kwa wakati mmoja, uchaguzi na upigaji kura utaendeshwa kama uchaguzi mmoja.

## SEHEMU YA NNE
## UCHAGUZI WA KUJAZA NAFASI ZA NASIBU

Uchaguzi wa kujaza nafasi za nasibu

6. Kwa madhumuni ya uchaguzi wa kujaza nafasi yoyote ya nasibu, kutakuwa na karatasi moja tu ya kura ambayo itakuwa na orodha ya majina ya wagombea wote waliojitokeza, inayofuata mfululizo wa alfabeti pamoja na jina la chama cha mgombea na kutakuwa na nafasi tupu pembeni ya jina la kila mgombea kwa ajili ya kuweka alama ya kupiga kura.

## SEHEMU YA TANO
## UTARATIBU WA KUPIGA KURA

Utaratibu wa kupiga kura

7.-(1) Kila Mbunge atakayekuwepo ukumbini wakati wa kupiga kura anaweza, katika uchaguzi wa kwanza katika maisha ya Bunge au katika uchaguzi wa kujaza nafasi ya nasibu moja au zaidi-

(a) kupiga kura moja au zaidi kulingana na maelekezo yaliyomo kwenye karatasi ya kura kwa ajili ya wagombea uchaguzi wa nafasi inayoshindaniwa kutoka miongoni mwa wale waliopendekezwa; au

(b) kupiga kura moja kwa kila mgombea uchaguzi mmoja kwa kufuata idadi ya nafasi za nasibu zilizopo katika uchaguzi huo.

(2) Mbunge atapiga kura yake kwa kuweka alama ya "V" katika nafasi wazi ya karatasi ya kura pembeni ya jina la mgombea anayetaka kumpigia kura.

(3) Endapo zoezi la uchaguzi litaendeshwa kwa kupiga kura kwa mfumo wa elektroniki, kupiga na kuhesabu kura kutafanyika papo kwa papo na matokeo yake yatakuwa halali.

## SEHEMU YA SITA
## KUPIGA KURA

Kupiga kura

8.-(1) Utakapofika wakati wa kupiga kura, Spika atasitisha majadiliano ya Bunge na kuelekeza kwamba, kura ipigwe.

(2) Wakati huo huo mambo yafuatayo yatafanyika:

(a) Katibu atatangaza idadi au aina ya chaguzi zitakazofanyika au nafasi zitakazojazwa; na

(b) kila mgombea atapewa muda wa kujieleza na kuomba kura.

(3) Kabla ya kupiga kura, sanduku la kura litaoneshwa kwenye ukumbi kuwa ni tupu, baada ya hapo kila Mbunge atakayekuwepo ukumbini atapewa karatasi moja ya kupiga kura.

(4) Sanduku la kura litawekwa chini ya usimamizi wa Katibu na Wabunge waliochaguliwa kusimamia zoezi la kuhesabu kura mpaka wakati wa kuhesabu kura ambapo Katibu pamoja na hao Wabunge watakuwa na madaraka kuhakikisha kwamba –

(a) sanduku hilo halifunguliwi mpaka wakati wa kuanza kuhesabu kura; na

(b) hakuna kitu kitakachowekwa ndani ya sanduku hilo baada ya karatasi za kura kukusanywa kwa mujibu wa fasili ndogo ya (3).

(5) Baada ya Wabunge kupiga kura, karatasi zitakusanywa na kutumbukizwa kwenye sanduku la kura.

(6) Baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika na karatasi za kura kukusanywa, Spika atachagua Wabunge wawili wasimamie kazi ya kuhesabu kura na majadiliano ya Bunge yatarudia kuanzia pale yalipositishwa.

## SEHEMU YA SABA
## KUHESABU KURA

Kuhesabu kura

9.-(1) Mapema itakavyowezekana baada ya kupiga kura na kabla ya kumaliza kikao kilichopo cha Bunge, Katibu, mbele ya Wabunge wawili waliochaguliwa kusimamia zoezi la kuhesabu kura, atafungua sanduku la kura, atahesabu na ataandika kura alizopata kila mgombea.

(2) Karatasi ya kura itakataliwa na kura haitahesabiwa katika karatasi hiyo ikiwa-

(a) karatasi hiyo siyo rangi rasmi ya karatasi ya kupigia kura iliyotolewa na Katibu;

(b) mpiga kura amepiga kura zaidi au pungufu ya zile zinazotakiwa kupigwa;

(c) kutaonekana kwenye karatasi hiyo maandishi yoyote au alama yoyote iliyowekwa na mpiga kura isiyokuwa ile ya "V"; au

(d) haikuwekwa alama au imewekwa alama isiyoonesha dhahiri ni mgombea yupi ambaye mpiga kura amempigia; isipokuwa kwamba, ikiwa baadhi ya kura kwenye karatasi ya kura ni dhahiri na nyingine si dhahiri, karatasi ya kura hiyo itakataliwa kuhusu tu zile kura zisizokuwa dhahiri na kura zilizo dhahiri zitahesabiwa.

(3) Uamuzi wa Spika kuwa karatasi ya kura ikataliwe yote au sehemu tu utakuwa ni wa mwisho.

## SEHEMU YA NANE
## KUTANGAZA MATOKEO YA KURA

Kutangaza matokeo ya kura

10.-(1) Baada ya kura kuhesabiwa, Katibu atatangaza matokeo ya kura zote kisha atatamka majina ya wagombea waliochaguliwa ambao wamepata idadi kubwa zaidi ya kura na kuwatangaza kwamba wamechaguliwa.

(2) Endapo baada ya kuhesabu kura kutakuwa na sababu ya kurudia uchaguzi kutokana na kutopatikana mshindi katika nafasi yoyote inayohusika katika uchaguzi huo, Spika ataeleza sababu za kutopatikana mshindi na ataagiza kura ipigwe tena ili kupata mshindi kwa nafasi hiyo.

(3) Kura ya uamuzi haitatumika kwenye uchaguzi.

(4) Iwapo imeamuliwa ipigwe kura tena kwa mujibu wa fasili ndogo ya (2), wagombea wanaopigiwa kura watakuwa ni waliopata kura sawa.

(5) Iwapo Spika hawezi kutangaza idadi inayotakiwa ya wagombea waliochaguliwa kwa sababu ya kukosekana kura-

(a) atatangaza kadri ya wingi wa wagombea waliochaguliwa ambao wamepata kura kuwa wamechaguliwa; na

(b) atawaarifu Wabunge wote kuhusu nafasi iliyobaki au zilizobaki na utaratibu wa uchaguzi utaanza upya kwa ajili ya nafasi hiyo au nafasi hizo.

(6) Kila tamko na agizo linalotolewa na Spika kwa mujibu wa fasili hii litatolewa Bungeni.

## SEHEMU YA TISA
## UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU ZA KURA

Utunzaji wa kumbukumbu za kura

11.-(1) Katibu ataandika maneno *"imekataliwa"* na *"kura iliyokataliwa"* kwenye karatasi za kura zilizokataliwa na ataziweka karatasi hizo pamoja na zile zilizokuwa safi kwa muda wa miezi sita baada ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi.

(2) Baada ya hapo, isipokuwa kama Bunge litaamuru vinginevyo, Katibu ataziharibu karatasi hizo.

(3) Karatasi za kura zilizokwishatumika hazitaoneshwa kwa mtu yeyote na Katibu, isipokuwa kwa mujibu wa azimio la Bunge baada ya hoja ya kutaka zioneshwe kupitishwa.

## SEHEMU YA KUMI
## MALALAMIKO DHIDI YA MATOKEO YA KURA

Utaratibu wa kushughulikia Malalamiko

12.-(1) Iwapo mgombea yeyote hataridhika na matokeo ya uchaguzi au jinsi uchaguzi ulivyofanyika, atawasilisha malalamiko yake kwa Spika ndani ya siku moja tangu tarehe ya uchaguzi na Spika ataitisha Kamati ya Kanuni za Bunge kushughulikia malalamiko hayo mapema iwezekanavyo.

(2) Kamati itakapokamilisha kushughulikia jambo hilo Spika ataagiza taarifa iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge kwa ajili ya kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni.

Masharti ya Jumla

13.-(1) Spika atakuwa na mamlaka ya kuelekeza kufanyika kwa jambo lolote litakalojitokeza ikiwa halijawekewa utaratibu chini ya Kanuni.

(2) Uamuzi wa Spika chini ya fasili ndogo ya (1) utazingatia miongozo na taratibu za chaguzi za kibunge.

---

## NYONGEZA YA TATU

---

### THE EAST AFRICAN LEGISLATIVE ASSEMBLY ELECTION RULES

---

*(Made under Order 17 of the Standing Orders and Article 50 of the Treaty for the Establishment of East African Community)*

---

### PART I
### PRELIMINARY RULES

Citation

1. These Rules may be cited as the East African Legislative Assembly Election Rules.

Application

2. These Rules shall apply in the election for East African Legislative Assembly Members hailing from Tanzania.

Interpretation

3. In these Rules, all the parliamentary words and expressions used shall have the same meaning assigned to them in the Parliamentary Standing Orders and, unless the context requires otherwise:-

"candidate" means a person who is nominated to stand for election to the East African Legislative Assembly as provided for in rule 5 of these Rules;

"election" means an election to the East African Legislative Assembly;

"Members" means the Tanzania members of the East African Legislative Assembly elected in terms of rule 14(b) of these Rules;

"nomination" means nomination as a candidate to stand for election to the East African Legislative Assembly;

"returning officer" means the Clerk of the National Assembly;

"Treaty" means the Treaty for the Establishment of the East African Community, 1999; and

"voter" means a Member of Parliament present and voting during the election.

## PART II
## QUALIFICATION OF CANDIDATES

Qualification of candidates

4. A person shall be qualified to be a candidate for election to the East African Legislative Assembly if he is qualified to be elected in accordance with Article 50(2) of the Treaty.

## PART III
## NOMINATION OF CANDIDATES

Nomination of candidates

5.-(1) Where an election is to be held, the returning officer shall by notice published in the Gazette, appoint a nomination day for that election.

(2) The returning officer shall give at least fourteen days notice of such nomination day.

Validity of nomination

6.-(1) In order to be validly nominated as a candidate for the East African Legislative Assembly election, a person shall be nominated in a transparent and democratic manner by the political party which is sponsoring him.

(2) The nomination shall be in the prescribed form annexed to these Rules, signed by the candidate and the Secretary General of the party nominating him, and shall contain the following particulars:

(a) name, educational qualifications, address and occupation of the candidate; and

(b) A certificate by the candidate that he is willing and otherwise qualified to stand for election.

(3) Every nomination paper shall be accompanied by the following documents:

(a) proof of citizenship of the United Republic of Tanzania, provided by the Immigration Department;

(b) a detailed biographical information relating to the candidate signed by the candidate, which shall enable the returning officer to determine whether or not the candidate has proven experience or interest in consolidating and furthering the aims and objectives of

the Community in terms of Article 50(2) of the Treaty; and

(c) an extract of the nomination proceedings of the party organ which approved the final nomination of the candidate, signed by the Chairman and Secretary of that organ which shall enable the returning officer to determine whether or not the relevant political party's proceedings were democratic and transparent in terms of the Political Parties Act.

Cap 258

(4) The candidate or an official of the Party nominating him, shall deliver the nomination form in either language to the returning officer at his office in Dodoma, not later than four O'clock in the afternoon of the nomination day.

(5) Any political Party which is entilted to sponsor candidates may submit to the Returning Officer, the names of three candidates for each vacant seat in the following relevant groups:

Group A: Women Candidates;
Group B: Zanzibar Candidates;
Group C: Minority Parties Candidates; and
Group D: Mainland Candidates.

(6) In the case of a by-election to fill a vacancy-

(a) candidates will be nominated only in respect of the group in which the vacancy has occurred; and

(b) no candidate may be nominated for more than one specified group.

Non-refundable deposit

7. A candidate, or an official of the party nominating him shall, at the time of delivering the nomination paper, deposit a non-refundable deposit of fifty thousand shillings, to cover for the cost of election expenses.

Rejection of nomination papers

8. Objections may be made by the returning officer to the nomination of a candidate, if it is apparent to him from the contents of the nomination papers that the candidate is not qualified to stand for election, the returning officer shall forthwith reject the nomination papers of that candidate.

## PART IV
## ELECTION AND VOTING PROCEDURE

Election day

9. The returning officer shall by notice published in the Gazette*,* appoint an election day which shall be not more than seven days after nomination day, provided that, such election day shall be a day when the National Assembly is sitting in ordinary session.

Withdrawal of candidature

10.-(1) A candidate may withdraw his candidature by notice in writing, signed and delivered by him to the returning officer and a copy to the Secretary General of the party sponsoring him, not later than four o'clock in the afternoon of the day following nomination day, thereafter no withdraws shall be accepted.

(2) Where candidate dies after four O'clock in the afternoon of nomination day and before election day, the election process will continue undisturbed.

Campaign by candidates

11.-(1) An aspiring candidate may introduce himself to the voters and seek their support even before nomination day and may continue to do so after nomination day.

(2) Before the votes are cast on election day, each candidate will be permitted to appear before the voters, duly assembled in an ordinary sitting of the House and address them in English for such length of time and answer such number of questions, if any, as may be determined by the Speaker for that purpose.

Supervision of voting process

12.-(1) The voting shall be conducted under the general supervision of the returning officer.

(2) The returning officer shall issue only one ballot paper to each voter.

(3) The ballot paper shall contain the names of all candidates, arranged alphabetically in the following groups:

Group A: Women Candidates;
Group B: Zanzibar Candidates;
Group C: Minority Parties Candidates; and
Group D: Mainland Candidates.

(4) A voter shall be required to cast a specified number of votes to be announced by the Speaker in each of the groups.

(5) On receiving a ballot paper, each voter shall secretly record his votes by putting a mark against the names of the nine candidates he wishes to vote for.

(6) Each voter shall be required to cast as many votes as there are vacancies, otherwise his whole ballot paper will be regarded as spoilt.

(7) A voter who has accidentally spoiled his ballot paper while the voting is still in progress may surrender the spoilt ballot paper to the returning officer and obtain a replacement thereof.

Votes counting agents

13.-(1) When all the voters have casted their votes, the Speaker shall appoint two counting agents, one from the ruling party and the other from the minority benches, to act as counting agents for all the candidates.

(2) Immediately after all the ballots have votes been collected, the returning officer, with the assistance of Clerk Assistants and before the two counting agents as witnesses, shall count the votes so casted.

(3) In order to enable the National Assembly to proceed with other business, the counting of votes shall take place outside the Assembly Chamber, in a room designated by the Clerk for that purpose within the precincts of the Assembly.

Announcement of elections results

14. When the votes have been counted and the results of the election has been ascertained, the returning officer shall-

(a) report to the Assembly the election results, together with the number of votes recorded for each candidate in each group; and

(b) announce to the Assembly the names of nine persons receiving the majority number of votes in each group and shall declare those persons to have been elected as members of the East African Legislative Assembly.

Custody of ballot papers

15.-(1) The returning officer shall ensure the safe custody of all ballot papers and other documents relating and pertaining to the conduct of the election.

(2) The returning officer shall cause all documents to which this paragraph applies to be destroyed after the expiration of six months from the election day, unless otherwise directed by an order of the High Court arising from any proceedings of a petition relating to the election.

## PART V
## ANNULMENT AND AVOIDANCE OF ELECTION

Annulment and avoidance of election

16. Pursuant to the provisions of Article 52(1) of the Treaty, the election of a candidate as a member of the East African Legislative Assembly may be declared *null* and *void* only on an election petition.

Grounds for annulment and avoidance of election

17. The procedure, jurisdiction and grounds for declaring the election of such member *null* and *void* shall be the same as those provided by law for election petitions in respect of Members of the Parliament of the United Republic of Tanzania.

## PART VI
## GENERAL PROVISIONS

Matters not provided for

18.- (1) If any matter or thing arises which is not specifically provided for in these rules, the Speaker shall make a ruling directing what is to be done in respect of that matter or thing.

(2) In making such a ruling, the Speaker shall be guided by the practices and procedures normally followed in similar situations with regard to Parliamentary elections.

---

## FORMS

---

Fomu ya Uteuzi

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

FOMU YA UTEUZI WA WAGOMBEA WA UCHAGUZI
BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

*(Chini ya fasili ya 6(2) ya Nyongeza ya Tatu)*

**ANGALIZO:** JAZA FOMU KWA HERUFI KUBWA KWA KUTUMIA KALAMU YA WINO WA BLUU AU MWEUSI

## SEHEMU A: TAARIFA ZA MGOMBEA

*(Tafadhali jaza taarifa katika visanduku)*

Cheo: ☐

Jina la kwanza: ☐

Jina la ukoo: ☐

Tarehe ya kuzaliwa: ☐

(picha ya mgombea)

Mahali pa kuzaliwa (Wilaya/Mkoa) ☐

Jinsi: Me ☐ Ke ☐ *(Tafadhali weka alama ya (v) kwenye kisanduku husika)*

Uraia: ☐

Nambari ya Kitambulisho cha Taifa: ☐

Hali ya Ndoa: Nina Ndoa ☐ Sina Ndoa ☐ Mtalaka ☐ Mgane/Mjane ☐

*(Tafadhali weka alama ya (v) kisanduku husika)*

Kazi: ☐

## SEHEMU B: ANUANI YA MGOMBEA

*(Tafadhali jaza taarifa katika visanduku)*

Sanduku la Posta: [ ]

Namba ya Simu: [ ]

Barua pepe: [ ]

Makazi:

Mtaa:…………………………………………..
Kata:…………………………………………...
Wilaya:………………………………………...
Mkoa:…………………………………………

## SEHEMU C: TAARIFA ZA ELIMU YA MGOMBEA

*(Tafadhali jaza taarifa zako za elimu kwa mtiririko)*

| Na. | MWAKA | | JINA LA TAASISI ILIYOTOA CHETI | CHETI |
|---|---|---|---|---|
| | Kuanza | Kumaliza | | |
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |

*Unaweza kutumia karatasi za ziada ikiwa nafasi haitoshi.*

## SEHEMU D: VIAMBATISHO

Mgombea anatakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo kama kiambatisho kwenye fomu ya uteuzi:

1. Nakala za vyeti vya elimu.
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Uthibitisho wa mgombea kwamba yuko tayari na anazo sifa za kugombea.
4. Uthibitisho kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unaotolewa na Idara ya Uhamiaji.
5. Uthibitisho wa malipo ya amana inayotumika kugharimia uchaguzi.
6. Wasifu wa kina wa mgombea uliosainiwa na mgombea.

7. Dondoo ya muhtasari wa mwenendo wa kikao cha chama kilichoidhinisha uteuzi wa mwisho wa mgombea uliosainiwa kikamilifu na Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama. Dondoo hizo zitaambatishwa na nyaraka zifuatazo: *(zitakozotolewa na Katibu Mkuu wa chama cha Mgombea)*
   (a) Fomu ya uteuzi wa mgombea katika ngazi ya chama;
   (b) Orodha ya wanachama walioomba kuteuliwa kugombea nafasi ya Mjumbe;
   (c) Nyaraka zinazoonesha matokeo yanayotokana na uchaguzi wa kidemokrasia; na
   (d) Orodha iliyosainiwa ya wapiga kura wote walioshiriki zoezi la uteuzi wa wagombea.

**SEHEMU E: UTHIBITISHO**

*(Tafadhali jaza taarifa katika visanduku)*

Mimi ______________________ nimeteuliwa na chama

cha siasa kilichosajiliwa cha ______________________

ninakiri kuwa niko tayari, nina sifa na kwamba taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli kwa kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe ______________ Saini ya Mgombea ______________

**SEHEMU F: UTHIBITISHO WA KATIBU MKUU**

*(Tafadhali jaza taarifa katika visanduku)*

Mimi ______________________ Katibu Mkuu

wa chama cha siasa kilichosajiliwa cha ______________________

ninathibitisha kwamba Ndugu ______________________

ameteuliwa kidemokrasia na chama kuwa mgombea wa nafasi ya Mjumbe wa Bunge la Afrika Mashariki.

Saini ya Katibu Mkuu ______________

Tarehe: ______________

(Muhuri wa Chama)

Nomination Form

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PARLIAMENT OF TANZANIA

NOMINATION FORM FOR CANDIDATES TO STAND FOR ELECTION TO THE EAST AFRICAN LEGISLATIVE ASSEMBLY

*(Made under Rule 6(2) of the Third Schedule)*

**NOTE:** FILL THIS FORM IN CAPITAL LETTERS USING A BLUE OR BLACK PEN

## PART A: CANDIDATE'S PARTICULARS

*(Please fill in all the boxes)*

Title: ☐

Firrst Name: ☐

Middle Name: ☐

Surname: ☐

Date of Birth: ☐

Place of Birth: ☐

Candidate's Photograph

Sex: Male ☐ Female ☐ *(Please tick in the relevant box)*

Nationality: ☐

National ID No: ☐

Marital Status: Married ☐ Single ☐ Divorced ☐ Widow/Widower ☐

*(Please tick in the relevant box)*

Occupation: ☐

## PART B: CANDIDATE'S ADDRESS

*(Please fill in all the boxes)*

Postal Address: 

Mobile Number: 

Email: 

Place of Domicile:

Street:…………………………………………
Ward:…………………………………………
District:……………………………………..
Region:……………………………………..

## PART C: CANDIDATE'S EDUCATIONAL BACKGROUND

*(Please fill in your educational background)*

| No. | YEAR | | NAME OF AWARDING INSTITUTION | AWARD |
|---|---|---|---|---|
| | Start | Finish | | |
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |

*You may use extra papers if the space provided is not enough*

## PART D: ATTACHMENTS

The candidate is required to submit the following documents as attachment to the nomination Form:

1. Copies of certificates for all educational qualifications.
2. Candidates' Birth Certificate.
3. A Certificate by the candidate that he/she is willing and otherwise qualified to stand for election.
4. Proof of citizenship of the United Republic of Tanzania provided by the Immigration Department.
5. Proof of payment of the non-refundable deposit to cover for election expenses.
6. A detailed biographical information relating to the candidate, dully signed by the candidate.
7. An extract of the nomination proceedings of the party organ which approved

the final nomination of the candidate signed by the Chairman and Secretary General of the Party accompanied by:

(a) Candidate party's application for nomination form;
(b) A list of all candidates who were contesting to be nominated by the party;
(c) Documents (forms) indicating results of the democratic election for all those who were contesting within the party; and
(d) A signed list of all voters who voted for the nominated candidates.

*(These attachments shall be issued by the Party Secretary General)*

## PART E: CERTIFICATION

*(Please fill in all the boxes)*

I [ ] candidate sponsored by [ ] dully registered political party, do hereby state that I am willing to contest and qualified for the post and that all information provided above are true to the best of my knowledge.

Date: [ ] Candidate's Signature [ ]

## PART F: SECRETARY GENERAL CERTIFICATION

*(Please fill in all the boxes)*

I [ ] Secretary General of [ ] a dully registered political party, Do hereby state that [ ] has been democratically nominated by the party as a candidate for the East African Legislative Assembly elections.

Secretary General Signature [ ]

Date: [ ]

(Political Party Stamp)

## NYONGEZA YA NNE

THE SUBMISSION OF REGULAR REPORTS TO THE PARLIAMENT OF TANZANIA BY THE TANZANIA MEMBERS OF THE EAST AFRICAN LEGISLATIVE ASSEMBLY REGULATIONS

*(Made under Article 65 of the Treaty for the Establishment of the East African Community)*

Citation

1. These Regulations may be cited as the Submission of Regular Reports to the Parliament of the United Republic of Tanzania by the Members of the East African Legislative Assembly Regulations.

Interpretation

2.-(1) These Regulations are made to provide for a procedure for the Members of the East African Legislative Assembly hailing from Tanzania to submit regular reports to the Parliament of the United Republic of Tanzania.

(2) These Regulations shall apply to Members of East African Legislative Assembly hailing from the United Republic of Tanzania

Presentation of annual report

3. The Members of the East African Legislative Assembly shall present an annual report of the activities of the East African Legislative Assembly for the relevant year, to the Parliament of the United Republic of Tanzania through its Standing Committee responsible for foreign affairs.

Time of presentation

4. The annual reports shall be presented at a regular meeting of the Standing Committee at a time to be determined by the Chairman of the Committee.

Presentation of special report and consultations

5. The Tanzania Members of the East African Legislative Assembly may, if they consider it desirable to do so, present any special report or make any appropriate consultations with the Committee, on any matter which is relevant to the work of the East African Legislative Assembly at any other scheduled meeting of the Committee.

Attendance and laying of reports on table

6.-(1) All Tanzania Members of the East African Legislative Assembly shall be present at the time of presentation of any report.

(2) All such reports shall subsequently be laid on the Table of the House and shall be debated upon.

# NYONGEZA YA TANO

## THE PAN – AFRICAN PARLIAMENT (TANZANIA MEMBERS) ELECTION RULES

*(Made under Order 15 of the Standing Orders and Articles 4 and 5 of the Protocol to the Treaty for Establishing of the African Economic Community Relating to the Pan-African Parliament)*

## PART I
## PRELIMINARY PROVISIONS

Citation

1. These Rules may be cited as the Pan – African Parliament (Tanzania Members) Election Rules.

Interpretation

2. In these Rules, unless the context requires otherwise: -

"candidate" means a Member of Parliament who is duly nominated to stand for election to the Pan-African Parliament as provided for in rule 5 of these Rules;

"election" means the election to membership of the Pan-African Parliament;

"election day" means the day on which the election of Members of the Pan-African Parliament is set to be conducted;

"nomination" means nomination as a candidate to stand for election to the Pan-African Parliament;

"nomination day" means the day which shall by notice published by the returning officer, be set to be the last day for receiving application forms from candidates;

"nominator" means a Member of Parliament of the Parliament of the United Republic of Tanzania entitled to vote, who nominates and supports a candidate who aspires to stand and contest for election to the Pan-African Parliament;

"qualification" means the qualification which entitles a person to stand and contest for election to the Pan-African Parliament;

"returning Officer" means the Clerk of the National Assembly;

"Speaker" means the Speaker of the National Assembly; and

"voter" means a Member of Parliament of the United Republic of Tanzania present and voting during the election.

## PART II
## QUALIFICATION OF CANDIDATES

Qualification of Candidates

3. No person shall be qualified to be a candidate for election to the Pan-African Parliament unless he or she is a Member of Parliament of the United Republic of Tanzania, and is fluent in any of the languages approved for use in the proceedings of the Pan-African Parliament.

## PART III
## NOMINATION PROCEDURE

Appointment of nomination day

4.-(1) Where election of Members of the Pan-African Parliament is to be held, the returning officer shall, by written notice circulated to all members of the Parliament of the United Republic of Tanzania, appoint a nomination day for that election, which must be a day during any period when the National Assembly is in ordinary session.

(2) The returning officer shall give at least seven days notice of such nomination day.

Nomination procedure

5. The following shall be the procedure for the nomination of candidates that:

(a) in the case of a General Election of all the five members of the Pan-African Parliament representing Tanzania, the candidates will be nominated in accordance with the following groups:

Group A: Women Candidates;
Group B: Zanzibar Candidates;
Group C: Mainland Candidates; and
Group D: Minority Parties Candidates:

Provided that, whereas group A shall be reserved for women candidates only, the remaining groups shall be open to both men and women candidates.

(b) the number of candidates to be elected in each group shall be as follows:
Group A: One Candidate.
Group B: One Candidate.
Group C: Two Candidates.
Group D: One Candidate.

(c) in the case of a by-election to fill a vacancy, candidates will be nominated only in respect of the group in which the vacancy has occurred; and

(d) no candidate may be nominated for more than one specified group.

Nomination of candidates

6.-(1) In order to be validly nominated to stand as a candidate for election to Pan-African Parliament, a person shall be nominated and supported in writing by not less than ten nominators who are entitled to vote at that election. A nominator may nominate up to four candidates, one for each of the four groups.

(2) The nomination shall be in the prescribed form obtainable from the returning officer, and shall contain working experience of the candidate.

(3) The time for receipt by the returning officer of nomination forms duly completed by the aspiring candidates shall expire at four o'clock in the afternoon of the nomination day and soon thereafter, the returning officer shall give written notification to all Members of Parliament, of the complete list of the all candidates who have been validly nominated for the election in respect of each of the four groups.

(4) After being validly nominated, a candidate may withdraw his candidature by notice in writing signed and delivered by him to the returning officer, not later than four O'clock in the afternoon of the day following the nomination day, thereafter, no withdrawal shall be accepted.

(5) Where a candidate dies at any time after nomination day and before election day, the election process shall continue undisturbed.

(6) After being validly nominated, a candidate may conduct his or her election campaign.

## PART IV
## ELECTION PROCEDURE

Election day

7. The returning officer shall, by written notice circulated to all Members of Parliament, appoint an election day, which must be a day on which the National Assembly is sitting in ordinary session and shall be not more than five days after nomination day.

Voting process

8. The voting process shall be conducted under the general supervision of the Speaker:

Provided that, if the Speaker is a candidate, shall vacate the chair before the commencement of the election proceedings.

Candidates to address voters

9. Before the voting exercise takes place on election day, each Candidate shall be given an opportunity to appear before the voters assembled in an ordinary sitting of the National Assembly and address them in English for such length of time and answer such number of questions, if any, as may be determined by the Speaker for that purpose.

Voting procedure

10. Immediately after address of the candidates, voting shall commence and proceed as follows:

(a) only one ballot paper shall be issued to each voter;
(b) the ballot paper shall contain all names of the Candidates arranged in alphabetical order for each of the groups; and
(c) each voter shall be required to cast the exact number of votes equal to the number of persons to be elected in each group.

Casting of votes

11.-(1) On receiving a ballot paper each voter shall secretly record his or her five votes by placing a tick in the space provided against the name of each candidate, and thereafter shall place the ballot paper in the ballot box.

(2) A voter who has accidentally spoiled his or her ballot paper while voting is still in progress may surrender the spoilt ballot paper to Returning Officer and obtain a replacement thereof.

Appointment of counting Agents and counting of votes

12.-(1) Immediately after all the votes have been placed in the ballot boxes and before the ballot boxes are removed from the Assembly Chamber for counting the votes, the Speaker shall appoint one counting agent for the candidates in each of the groups:

Provided that, any candidate who wishes to appoint his or her own counting agent may do so by submitting the name of that agent to the Speaker immediately after the appointments by the Speaker have been announced.

(2) The counting of votes shall be done by such number of officers of the Assembly as may be appointed by the returning officer, and shall be witnessed by the counting agents.

Place for counting of Votes

13. In order to enable the National Assembly to proceed with other business scheduled for that day, the counting of votes shall take place in a room designated by the Clerk for that purpose within the precincts of the Assembly.

Declaration of election results

14. After the countig of votes is complete and the results ascertained and certified by the returning officer and the counting agents, the returning officer shall immediately submit the results to the Speaker who shall-

(a) report to the Assembly the results of the election together with the number of votes recorded for each candidate in each of the Groups; and
(b) announce to the Assembly the names of five Candidates receiving the highest number of votes in each Group, and shall declare those candidates to have been elected as Members of the Pan-African Parliament.

Custody of ballot papers

15.-(1) The returning officer shall ensure the safe custody of all ballot papers and other documents pertaining to the election.

(2) The returning officer shall cause all documents to which this rule applies to be destroyed after the expiration of six months from the election day.

## PART V
## MISCELLANEOUS PROVISIONS

Matters not provided for

16.-(1) Where anything arises which is not specifically provided for in these Rules, the Speaker shall make a ruling directing what is to be done.

(2) In making a ruling referred under sub-rule (1), the Speaker shall be guided by the procedures and practices normally followed in similar situations with regard to Parliamentary elections.

# NYONGEZA YA SITA

## MWONGOZO KUHUSU MASWALI KWA WAZIRI MKUU

(*Chini ya Kanuni ya 47(1) na (6)*)

Maelezo ya Jumla

1.-(1) Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu kikishaanza Bungeni, hakitakatishwa wala kusitishwa, isipokuwa kutokana na sababu maalum ya dharura.

(2) Maswali yatakayoulizwa kwa Waziri Mkuu wakati wa Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu yatakuwa ni yale yanayohusu Sera za Serikali au jambo lolote lenye manufaa na maslahi kwa jamii na Taifa lililo chini ya madaraka na mamlaka ya kazi ya Waziri Mkuu.

(3) Maswali kwa Waziri Mkuu yatakuwa ni ya papo kwa papo; yaani yataulizwa bila kutolewa taarifa na yatajibiwa kwa mdomo papo kwa papo.

(4) Waziri Mkuu hatalazimika kujibu swali lolote linalohitaji takwimu au majibu yanayohitaji utafiti.

Utaratibu wa kupata fursa ya kumuuliza Waziri Mkuu swali

2. Bila ya kuathiri masharti ya fasili ndogo ya 3(1) ya Mwongozo huu, Mbunge anayetaka kumuuliza swali Waziri Mkuu wakati wa kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, atawasilisha jina lake kwa Katibu, kabla ya saa 2.30 Asubuhi, siku hiyo ya maswali kwa Waziri Mkuu.

Utaratibu wa kuuliza maswali kwa Waziri Mkuu

3.-(1) Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu kinapoanza Bungeni, Spika atamwita Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni na kumpa fursa ya kwanza ya kumuuliza swali Waziri Mkuu.

(2) Baada ya kuuliza na kujibiwa swali lake la kwanza, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni anaweza kumuuliza Waziri Mkuu swali moja la ufafanuzi.

(3) Mbunge yeyote atakayepata fursa ya kumuuliza swali Waziri Mkuu na kujibiwa, anaweza kumuuliza Waziri Mkuu swali lingine moja la ufafanuzi.

(4) Endapo orodha ya majina ya wauliza maswali kwa Waziri Mkuu kwa siku hiyo itafikia mwisho lakini muda wa kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu bado haujamalizika, Spika anaweza kutoa fursa kwa Mbunge yeyote ambaye hakupangwa katika orodha hiyo kumuuliza swali Waziri Mkuu.

(5) Mbunge anayetaka kupewa fursa na Spika kwa mujibu wa fasili ndogo ya (4), atasimama mahala pake ili Spika amwone na kumwita.

(6) Mbunge yeyote aliyepata fursa ya kumuuliza swali Waziri Mkuu wakati wa kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, atakuwa na haki ya kuuliza swali lake lililowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za siku hiyo wakati wa kipindi cha maswali ya kawaida kitakapowadia.

Maswali na majibu kwa Waziri Mkuu

4. Maswali na majibu katika kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu yatakuwa mafupi.

# NYONGEZA YA SABA

## MWONGOZO WA KUSIMAMIA UKUSANYAJI NA UTOAJI WA HABARI ZA BUNGE

*(Chini ya Kanuni ya 167(4))*

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Maelezo ya jumla

1. Mwongozo wa kusimamia ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge una lengo la kukuza demokrasia na uwazi katika shughuli za Bunge, kudumisha mahusiano na wananchi kupitia vyombo vya habari na kuainisha majukumu ambayo yanatekelezwa na Kamati kwa uwazi na faragha.

## SEHEMU YA PILI
## MISINGI NA MASHARTI YA UTOAJI WA HABARI ZA BUNGE

Misingi ya ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge

2. Bila ya kuathiri masharti ya sheria zinazosimamia ukusanyaji na utoaji wa habari, ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge utazingatia misingi ifuatayo:

(a) haki, uwazi na uwajibikaji wa Bunge na Wabunge;
(b) kutoingilia maisha binafsi na faragha ya Mbunge;
(c) kutoingilia uhuru wa Bunge na Wabunge katika kutekeleza majukumu yao;
(d) kuhakikisha kuwa habari zinazotolewa zinazingatia ukweli na hazilengi kupotosha jamii; na
(e) kuhakikisha kuwa habari zinazotolewa haziegemei upande wowote na hazina ubaguzi.

Matangazo ya moja kwa moja kurushwa na Studio ya Bunge

3.-(1) Matangazo ya moja kwa moja ya Vikao vya Bunge na Vikao vya Kamati yatatolewa na Studio ya Bunge.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ndogo ya (1), chombo cha habari au mwandishi wa habari anaweza kuomba kurusha matangazo ya moja kwa moja ya vikao vya Bunge yaliyoandaliwa na Studio ya Bunge.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya fasili ndogo ya (2), chombo cha habari kitarusha matangazo bila mabadiliko na kama yalivyopokelewa kutoka Studio ya Bunge.

Upigaji picha katika Ukumbi na maeneo mengine ya Bunge

4.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya 8 ya Mwongozo huu, upigaji picha katika Ukumbi wa Bunge na maeneo ya Bunge utazingatia heshima, utu na staha.

(2) Vifaa vitakavyotumika katika upigaji picha vitaidhinishwa na Katibu kabla ya kupiga picha katika Ukumbi wa Bunge na maeneo ya Bunge.

(3) Mpiga picha anakapokuwa kwenye Ukumbi wa Bunge ataelekeza kamera yake kwa Spika au Mbunge anayezungumza wakati huo.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ndogo ya (2), mpiga picha anaweza kuacha kuelekeza kamera kwa Spika au Mbunge na kuelekeza sehemu nyingine pale ambapo kuna tukio jingine linalohusiana na shughuli inayoendelea.

Maeneo yasiyoruhusiwa kupiga picha

5.-(1) Upigaji picha hautaruhusiwa katika maeneo yafuatayo:

(a) maeneo ya ukaguzi wa usalama;
(b) benki, mgahawa na zahanati ya Bunge;
(c) maegesho ya magari;
(d) kumbi zote za kupumzikia wageni;
(e) jengo la utawala; na
(f) maeneo mengine yatakayoamuliwa na Katibu.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ndogo ya (1), upigaji picha katika maeneo hayo unaweza kuruhusiwa kwa kibali kitakachotolewa na Katibu.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI KUHUSU UPATIKANAJI WA HABARI KUTOKA KATIKA VIKAO VYA KAMATI ZA BUNGE

Majukumu ya wazi

6. Majukumu yatakayotekelezwa kwa uwazi na ambayo yanaweza kutolewa kwa waandishi wa habari bila kuleta athari kwenye uamuzi wa Kamati ni yafuatayo:

(a) mambo ya kawaida ya kuisimamia na kuishauri Serikali, kama vile kutathmini utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;
(b) maoni yanayotolewa na wadau wanaoalikwa na Kamati, kulingana na utaratibu uliowekwa na Bunge;
(c) majukumu ambayo yanalenga kuwapatia Wabunge elimu, semina, makongamano na ziara za mafunzo; na
(d) maelezo yanayotolewa na Serikali kwenye Kamati za Bunge kwa lengo la kutoa ufafanuzi kwa Wabunge wanapotekeleza majukumu ya Kamati.

Majukumu ya faragha

7. Majukumu yatakayofanywa kwa faragha yatahusu mambo yote ambayo habari zake zikitolewa kwa waandishi wa habari kabla ya wakati wake yanaweza kuathiri uamuzi wa Kamati na pia kusababisha ukiukwaji wa Kanuni za Bunge ni yafuatayo:
(a) kazi zote zinazopelekwa kwenye Kamati na Spika ili kupata mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa na Bunge;
(b) shughuli zote za uchambuzi wa hoja mbalimbali zilizoko mbele ya Kamati;
(c) shughuli zote zinazotekelezwa kwa utaratibu wa kiuchunguzi;
(d) shughuli zote za kiuchunguzi zenye utaratibu uliowekewa masharti zinazotekelezwa na Kamati;
(e) shughuli zote zinazotekelezwa na Kamati ndogo; na
(f) Kamati zinapofanya ziara za kiuchunguzi.

Kamati zinazotekeleza majukumu kwa faragha

8.-(1) Kamati zitakazotekeleza majukumu yake kwa faragha ni Kamati ya Uongozi, Kamati ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu ya Serikali za Mitaa na Kamati ya Bajeti.

(2) Majukumu yenye uwazi wenye mipaka ni yale yenye utaratibu uliowekewa masharti ambayo yanayotekelezwa na Kamati za kiuchunguzi zifuatazo:
(a) Kamati ya Hesabu za Serikali;
(b) Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa;
(c) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; na
(d) Kamati ya Bajeti.

(3) Kwa madhumuni ya fasili hii, taarifa zenye uwazi wenye mipaka zitajumuisha-

(a) taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapowasilishwa Bungeni inakuwa wazi kwa vyombo vya habari; na

(b) mchakato wa Kamati hizi kuwahoji Maafisa Masuuli kuhusiana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali utakuwa wazi hadi hatua ambayo Kamati inataka kufanya uamuzi wa kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa na Bunge, ambapo Kamati itafanya kazi zake kwa faragha.

(4) Iwapo mchakato wa kuhoji Maafisa Masuuli unaofanywa chini ya fasili ndogo ya (3)(b) utakuwa ni wa kiuchunguzi, mchakato utafanyika kwa faragha.

(5) Kamati zinapofanya ziara kwa lengo la kujifunza au kujielimisha, shughuli zake zitafanywa kwa uwazi na Wajumbe wa Kamati watakuwa na uhuru wa kutoa maoni yao ya jumla kwenye vyombo vya habari.

(6) Maoni ya Wajumbe wa Kamati chini ya fasili ndogo ya (4), yatakuwa ni yale ambayo hayaathiri uamuzi utakaotolewa kwa faragha na Kamati baada ya ziara yake.

(7) Waandishi wa Habari katika kutoa taarifa zinazotokana na maoni ya Wajumbe wa Kamati, watapaswa waeleze wazi kwamba maoni hayo ni ya Mbunge binafsi na siyo ya Bunge wala Kamati au Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni.

Utoaji wa Taarifa baada ya Kikao cha Kamati

9.-(1) Pale ambapo Waziri anakutana na Kamati kwenye vikao vilivyopangwa, na inapotokea anakutana na waandishi wa habari baada ya kikao cha Kamati, Waziri huyo atakuwa huru kutoa maoni kuhusiana na jambo lililoshughulikiwa kwenye Kamati.

(2) Mwenyekiti wa Kamati au Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni, inapotokea anakutana na waandishi wa habari, atakuwa huru kutolea maoni jambo lolote lililofanyiwa kazi kwenye Kamati pale ambapo Kamati imekutana kushughulikia jambo fulani.

(3) Maoni yatakayotolewa chini ya fasili ndogo ya (1) au ya (2) hayatahusu uamuzi uliotolewa na Kamati utakaowasilishwa Bungeni.

(4) Kwa madhumuni ya fasili hii, utaandaliwa utaratibu wa kawaida wa namna Wenyeviti wa Kamati watakavyokuwa wanakutana na waandishi wa habari kuzungumzia shughuli itakayotekelezwa au iliyotekelezwa na Kamati na maelezo hayo yanayotolewa kwenye Vyombo vya Habari, kwa namna yoyote, yasiwe ni mapendekezo ambayo Kamati imeazimia kuyawasilisha Bungeni na ambayo yanaweza kuathiri uamuzi wa Kamati.

(5) Endapo itatokea jambo ambalo lina maslahi kwa umma, na wananchi wanataka maelezo, Mwenyekiti wa Kamati atakuwa na uhuru wa kutoa maelezo ya jumla ili mradi maelezo hayo hayatahusiana na uamuzi wa Kamati ambao utakaowasilishwa Bungeni.

## SEHEMU YA NNE
## UKIUKWAJI WA MASHARTI YA MWONGOZO

Ukiukwaji wa Mwongozo Sura ya 296

10.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, chombo cha habari au mtu atakayekiuka Mwongozo huu anaweza kuchukuliwa hatua zifuatazo:

(a) kupewa onyo;
(b) kusimamishwa kwa muda kuchukua na kutoa habari za Bunge; au
(c) kufutiwa kibali cha ukusanyaji wa habari na utoaji wa habari za Bunge.

(2) Mtu au chombo cha habari kitakachokiuka masharti ya Mwongozo huu kitapata fursa ya kusikilizwa na Katibu kabla ya kuchukuliwa hatua zilizoanishwa katika fasili ndogo ya (1).

# NYONGEZA YA NANE

## KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE

*(Chini ya Kanuni ya 140)*

## SEHEMU YA KWANZA
## KAMATI ZA KUDUMU ZISIZO ZA KISEKTA

Kamati za Kudumu zisizo za kisekta

1. Kamati za Kudumu zisizo za Kisekta zitakuwa zifuatazo:
(a) Kamati ya Uongozi;
(b) Kamati ya Kanuni za Bunge; na
(c) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Muundo na majukumu ya Kamati ya Uongozi

2.-(1) Kamati ya Uongozi itakuwa naWajumbe wafuatao:
(a) Spika, ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Naibu Spika, ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;
(c) Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni au Mwakilishi wake;
(d) Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni au Mwakilishi wake;
(e) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na
(f) wenyeviti wa Kamati za Kudumu au Makamu wao.

(2) Katibu atakuwa katibu wa Kamati.

(3) Majukumu ya Kamati ya Uongozi yatakuwa ni kujadili na kumshauri Spika kuhusu mambo yote yanayohusu uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na utaratibu wa kurahisisha uendeshaji wa shughuli za Bunge au za Kamati yoyote.

(4) Katika kutekeleza kazi zilizotajwa katika fasili ndogo ya (3), Kamati ya Uongozi itakuwa na uwezo wa kuweka muda ambao shughuli yoyote iliyopelekwa katika Kamati inayohusika sharti ikamilike na iwapo shughuli iliyopelekwa imewekewa muda kama huo, basi baada ya kuisha muda huo au baada ya kuisha muda wowote ulioongezwa, Kamati inayohusika itahesabiwa kuwa imekamilisha shughuli hiyo, na shughuli hiyo itaendelea kwenye hatua nyingine kana kwamba Mwenyekiti wa Kamati hiyo amemuarifu Spika kumalizika kwa shughuli hiyo.

Muundo na majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge

3.-(1) Kamati ya Kanuni za Bunge itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Spika ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Naibu Spika ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;
(c) Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni au Mwakilishi wake;
(d) Wenyeviti wa Bunge;
(e) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na
(f) Wajumbe wengine watakaoteuliwa na Spika.

(2) Vikao vya Kamati ya Kanuni za Bunge vitaongozwa na Spika, na kama Spika hayupo, vitaongozwa na Naibu Spika.

(3) Majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge yatakuwa ni-

(a) kujadili na kutoa mapendekezo juu ya kufanya marekebisho au mabadiliko katika Kanuni;
(b) kuchunguza na kutoa taarifa juu ya pendekezo lolote la mabadiliko katika Kanuni za Kudumu za Bunge ambalo limepelekwa kwa Kamati hiyo na Spika au na Mbunge;
(c) kuchunguza na kutoa taarifa kuhusu malalamiko dhidi ya uamuzi wa Spika ambayo yamepelekwa katika Kamati hiyo na Spika;
(d) kwa kushauriana na Spika, kuzifanyia marekebisho au mabadiliko Nyongeza za Kanuni;
(e) kumshauri Spika kuhusu masuala ya ukiukwaji wa Kanuni au suala lolote linalohusu utaratibu; na
(f) kushughulikia malalamiko dhidi ya matokeo ya uchaguzi unaofanyika kwa mujibu wa Nyongeza ya Pili ya Kanuni.

(4) Akidi ya kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge itakuwa ni nusu ya wajumbe waliotajwa katika fasili ya 3(1)(c), (d), (e) na (f).

Majukumu ya Kamati ya Haki Maadili na Madaraka ya Bunge

4.-(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki, kinga na madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika;

(b) kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika; na
(c) kushughulikia shauri linalomhusu Mbunge anayewakilisha Bunge kwenye chombo kingine cha uwakilishi au Mjumbe wa Bunge la Afrika Mashariki.

(2) Kamati itakapokamilisha kushughulikia suala husika, Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika kwa maandishi kwamba, Kamati imekamilisha kushughulikia suala husika.

(3) Spika baada ya kupokea taarifa hiyo, ataagiza iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge kwa ajili ya kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni.

## SEHEMU YA PILI
## KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE ZA KISEKTA

Kamati za Kudumu za Kisekta

5. Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta zitakuwa zifuatazo:
(a) Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo;
(b) Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria;
(c) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama;
(d) Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
(e) Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii;
(f) Kamati ya Maji na Mazingira;
(g) Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo;
(h) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii;
(i) Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI;
(j) Kamati ya Miundombinu; na
(k) Kamati ya Nishati na Madini.

Kamati na shughuli za wizara

6.-(1) Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo itasimamia wizara zifuatazo:
(a) Wizara ya Viwanda na Biashara;
(b) Wizara ya Kilimo; na
(c) Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

(2) Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria itasimamia shughuli za-
(a) Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
(b) Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji;
(c) Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira katika masuala ya Muungano;

(d) Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu; na
(e) Wizara ya Katiba na Sheria.

(3) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama itasimamia shughuli za wizara zifuatazo:

(a) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
(b) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na
(c) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

(4) Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itasimamia shughuli za Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

(5) Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii itasimamia shughuli za-

(a) Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu; na
(b) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

(6) Kamati ya Maji na Mazingira itasimamia shughuli za-

(a) Wizara ya Maji; na
(b) Masuala ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira.

(7) Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo itasimamia shughuli za wizara zifuatazo:

(a) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na
(b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

(8) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii itasimamia shughuli za wizara zifuatazo:

(a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na
(b) Wizara ya Maliasili na Utalii.

(9) Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI itasimamia shughuli za:

(a) Wizara ya Afya; na
(b) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

(10) Kamati ya Miundombinu itasimamia shughuli za wizara zifuatazo:

(a) Wizara ya Ujenzi;
(b) Wizara ya Uchukuzi; na
(c) Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

(11) Kamati ya Nishati na Madini itasimamia shughuli za wizara zifuatazo:
(a) Wizara ya Nishati; na
(b) Wizara ya Madini.

Majukumu ya jumla ya Kamati za Kisekta

7.-(1) Majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta yatakuwa yafuatayo:
(a) kushughulikia bajeti ya Wizara au Taasisi inazozisimamia;
(b) kushughulikia Miswada ya Sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
(c) kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
(d) kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

(2) Bila kuathiri majukumu ya jumla ya Kamati za kisekta kama yalivyoainishwa katika fasili ndogo ya (1) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama itatekeleza pia majukumu yafuatayo:
(a) kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;
(b) kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;
(c) kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Bunge la Afrika;
(d) kushughulikia Taarifa zote za wawakilishi katika vyama mbalimbali vya kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama; na
(e) kushughulikia taarifa za hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi na usalama wa raia na mali zao.

## SEHEMU YA TATU
## KAMATI ZA SEKTA MTAMBUKA

Kamati za Sekta Mtambuka

8. Kamati za Sekta Mtambuka zitakuwa zifuatazo:
(a) Kamati ya Bajeti;
(b) Kamati ya Sheria Ndogo; na
(c) Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Majukumu ya Kamati ya Bajeti

9. Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo katika kanuni hizi, Kamati ya Bajeti itatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha;
(b) kusimamia shughuli za Tume ya Taifa ya Mipango;
(c) kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uandaaji wa mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka;
(d) kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya kila mwaka yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;
(e) kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
(f) kuchambua na kushauri kuhusu miswada ya sheria inayowasilishwa Bungeni yenye madhumuni ya kuongeza au kupunguza mapato na Bajeti ya Serikali;
(g) kufanya utafiti na uchambuzi kuhusu sera za kodi, fedha na kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali;
(h) kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;
(i) kutoa ushauri wa jumla kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge;
(j) kuchambua na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali; na
(k) kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali.

Majukumu ya Kamati ya Sheria Ndogo

10.-(1) Kamati ya Sheria Ndogo itakuwa na majukumu ya kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, sheria inayotekelezwa na sheria ndogo husika pamoja na sheria nyingine za nchi.

(2) Kamati itakapokamilisha kazi kwa mujibu wa fasili ndogo ya (1), Mwenyekiti atamjulisha Spika kwa maandishi.

(3) Spika, baada ya kupokea taarifa chini ya fasili ndogo ya (2), anaweza kuelekeza Taarifa ya Uchambuzi wa Kamati iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge kwa ajili ya kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni.

Majukumu ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

11.-(1) Majukumu ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

(b) kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

(2) Msingi wa kazi za Kamati utatokana na taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

## SEHEMU YA NNE
## KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE ZINAZOSIMAMIA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA

Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia Matumizi ya Fedha za Umma

12. Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma zitakuwa zifuatazo:

(a) Kamati ya Hesabu za Serikali; na

(b) Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali

13. Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali yatakuwa yafuatayo:

(a) kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na mashirika ya umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa fasili hii; na

(c) kutoa mapendekezo na ushauri kwa wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa

14. Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

(c) kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba, tatizo la matumizi mabaya ya fedha za umma linapungua.

Msingi wa kazi za Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma

15. Msingi wa kazi za Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa utatokana na Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

*Zimepitishwa kwa Azimio la Bunge la tarehe 11 Juni, 2025 kwa mujibu wa kanuni ya 176 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.*

Dodoma,
11 Juni, 2025

BARAKA I. LEONARD
*Katibu wa Bunge*